




# URATIBU MKUU WA MISALE YA KIROMA



**BARAZA LA MAASKOFU TANZANIA**







# **URATIBU MKUU WA MISALE YA KIROMA**

**2002**

**TEC – BARAZA LA MAASKOFU TANZANIA**

# MAPOKEO YALIYO HAI

Neno la Kanisa - 3

# Yaliyomo

YALIYOMO.....	3
DIBAJI YA TOLEO HILI .....	7
DIKRII YA IDHINI YA TAFSIRI HII.....	8
DIKRII YA IDHINI YA UCHAPISHAJI .....	9
<b>UTANGULIZI .....</b>	<b>12</b>
Ushuhuda wa imani isiyobadilika .....	12
Mapokeo yasiyokatizwa yathibitishwa .....	15
Marekebicho kulingana na Mazingira Mapya.....	16
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>21</b>
<b>UMAARUFU NA UKUU WA ADHIMISHO LA EKARISTI</b>	
<b>TAKATIFU .....</b>	<b>21</b>
<b>SURA YA PILI .....</b>	<b>25</b>
<b>MUUNDO WA MISA, MAMBO YAKE YA MSINGI NA SEHEMU</b>	
<b>ZAKE .....</b>	<b>25</b>
I. MUUNDO WA MISA KWA JUMLA .....	25
II. MAMBO MBALIMBALI YA MSINGI YA MISA .....	25
Somo la Neno la Mungu na Maelezo yake .....	25
Sala na sehemu nyingine zinazomhusu kuhani.....	26
Fomula nyingine zinazojitokeza katika adhimisho .....	27
Namna ya kusema Matini mbalimbali .....	28
Umuhimu wa Kuimba .....	28
Matendo ya Kiishara na hali za mwili.....	29
Kuhusu Ukimya .....	31
III. KUHUSU SEHEMU MOJA MOJA ZA MISA .....	31
A) IBADA-KANUNI ZA KUENZIA .....	31
Kuingia .....	32
Kuisalimu altare na watu waliokusanyika .....	32
Tendo la Toba .....	33
Bwana, Utuhurumie .....	33



Utukufu kwa Mungu juu .....	33
<i>Kolekta: (Sala ya kutimiliza Ibada-Kanuni ya Kuanzia) ....</i>	34
<b>B) LITURUJIA YA NENO .....</b>	<b>35</b>
Ukimya.....	35
Masomo ya Biblia.....	35
Zaburi ya Kuitikizana au Wimbo wa Katikati. ....	36
Shangilio kabla ya Somo la Injili .....	37
Homilia.....	38
Kuongama Imani.....	39
Maombi kwa wote .....	39
<b>C) LITURUJIA YA EKARISTI TAKATIFU.....</b>	<b>40</b>
Kuandaa Vipaji.....	41
Kuombea Dhabihu .....	42
Sala ya Ekaristi .....	43
Ibada-Kanuni ya Komunyo.....	44
Sala ya Bwana .....	45
Ibada-Kanuni ya Kupeana Amani .....	45
Kuumega Mkate.....	45
Ibada-kanuni ya Komunyo .....	46
<b>D) IBADA-KANUNI YA KUMALIZIA MISA .....</b>	<b>48</b>
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>49</b>
<b>KAZI NA HUDUMA KATIKA MISA .....</b>	<b>49</b>
I. KAZI ZA WENYE DARAJA TAKATIFU.....	49
II. MAJUKUMU YA TAIFA LA MUNGU .....	50
III. HUDUMA ZA KIPEKEE .....	51
Huduma Nyinginezo.....	51
IV. MGAWO WA MAJUKUMU NA MAANDALIZI YA ADHIMISHO .....	53
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>55</b>
<b>MITINDO MBALIMBALI YA KUADHIMISHA MISA.....</b>	<b>55</b>
I. MISA INAYOADHIMISHWA PAMOJA NA WATU .....	56
Vifaa vya kuandaliwa .....	56
A) MISA BILA SHEMASI.....	58
Kanuni ya Mwanzo.....	58

Liturujia ya Neno.....	59
Liturujia ya Ekaristi Takatifu.....	61
Ibada-Kanuni ya Kumalizia.....	68
<b>B) MISA AKIWEPO SHEMASI .....</b>	<b>68</b>
Ibada-Kanuni ya Kuanzia .....	69
Liturujia ya Neno.....	69
Liturujia ya Ekaristi Takatifu.....	70
Ibada-Kanuni ya Kumalizia.....	72
<b>C) KAZI ZA AKOLITI .....</b>	<b>72</b>
Ibada-kanuni ya mwanzo.....	72
Liturujia ya Ekaristi Takatifu.....	73
<b>D) KAZI ZA MSOMAJI.....</b>	<b>74</b>
Ibada-Kanuni ya mwanzo .....	74
Liturujia ya Neno.....	74
<b>II. MISA YA KUSHIRIKIANA MAKUHANI WAKONSELEBRANTI .....</b>	<b>74</b>
Ibada-Kanuni ya mwanzo .....	78
Liturujia ya Neno.....	78
Liturujia ya Ekaristi Takatifu.....	78
Namna ya kusema Sala ya Ekaristi .....	79
Sala ya Ekaristi I, au Kanuni ya Kiroma.....	79
Sala ya Ekaristi II.....	80
Sala ya Ekaristi III.....	81
Sala ya Ekaristi IV .....	82
Ibada-kanuni ya Komunyo.....	83
Ibada-kanuni ya Kumalizia.....	86
<b>III. MISA AMBAYO MHUDUMU MMOJA TU ANAHUDHURIA .....</b>	<b>87</b>
Ibada-kanuni ya mwanzo.....	87
Liturujia ya Neno.....	88
Liturujia ya Ekaristi Takatifu.....	88
Ibada-kanuni ya Kumalizia.....	89
<b>IV. KANUNI KUU KADHAA ZINAZOHUSU MITINDO YOTE YA MISA .....</b>	<b>90</b>
Heshima kwa Altare na Kitabu cha Injili.....	90
Kupiga goti na kuinama .....	90
Kuhusu Kufukizia Ubani .....	91

Kuhusu Kusafisha .....	93
Komunyo Katika Maumbo Yote Mawili.....	93
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>97</b>
<b>YANAYOHUSU MAANDALIZI NA MAPAMBO YA MAKANISA</b>	
<b>KWA AJILI YA KUADHIMISHA EKARISTI TAKATIFU .....</b>	<b>97</b>
I. KANUNI ZA JUMLA .....	97
II. MAANDALIZI YA PATAKATIFU KWA AJILI YA KUSANYIKO	
LA KIIBADA .....	99
Altare na mapambo yake .....	99
Mimbari .....	102
Kiti kwa ajili ya kuhani <i>selebranti</i> na viti vingine .....	103
III. MPANGILIO WA KANISA .....	103
Mahali pa waamini .....	103
Mahali pa kikundi cha kwaya na ala za muziki.....	104
Mahali pa kuhifadhia Ekaristi takatifu.....	105
Sanamu/picha takatifu .....	106
<b>SURA YA SITA .....</b>	<b>107</b>
<b>VIFAA VINAVYOHITAJIKA KWA KUADHIMISHA MISA</b>	
<b>TAKATIFU .....</b>	<b>107</b>
I. KUHUSU MKATE NA DIVAI KWA KUADHIMISHA EKARISTI	
TAKATIFU.....	107
II. MAPAMBO YA IBADA KWA UJUMLA .....	108
III. KUHUSU VYOMBO VITAKATIFU .....	108
IV. MAVAZI YA IBADA.....	109
V. ZANA NYINGINE ZINAZOTUMIKA KANISANI .....	112
<b>SURA YA SABA .....</b>	<b>114</b>
<b>KUCHAGUA MISA NA SEHEMU ZAKE .....</b>	<b>114</b>
I. KUCHAGUA MISA.....	114
II. KUCHAGUA SEHEMU ZA MISA .....	116
Masomo .....	116
Kuhusu Sala za Misa .....	119
Sala ya Ekaristi .....	<b>Errore. Il segnalibro non è definito.</b>
Nyimbo.....	120

<b>SURA YA NANE .....</b>	<b>121</b>
<b>MISA NA SALA KWA SHIDA MBALIMBALI NA MISA ZA WAFU .....</b>	<b>121</b>
I. MISA NA SALA KWA SHIDA MBALIMBALI .....	121
II. MISA ZA WAFU .....	123
<b>SURA YA TISA .....</b>	<b>125</b>
<b>MAREKEBISHO YALIYO CHINI YA MAMLAKA YA MAASKOFU NA MABARAZA YAO .....</b>	<b>125</b>
<b>TANBIHI .....</b>	<b>132</b>
<b>FAHARASA .....</b>	<b>143</b>

## URATIBU MKUU WA MISALE YA KIRUMI

### Tafsiri ya


### Instructio Generalis Missalis Romani

Kongregasio inayosimamia Ibada Takatifu na Taratibu za Sakramenti ilitoa kwa Kilatini *Instructio Generalis Missalis Romani* 2002. Uratibu huu ulitolewa hata kabla ya kutoa Misale ya Kirumi toleo la tatu. Lengo ni kuwaandaa Makleri, Wanafunzi Wa Upadri, Nyumba za Malezi na Walei Waamini wote, waweze kujifunza, kufundishwa maana ya Misa Takatifu, namna inavyoadhimishwa na namna ya kila mtu anavyotakiwa kushiriki kikamilifu sehemu zinazomhusu. Kwa namna hiyo hadhi ya adhimisho la Misa Takatifu na uadhimishaji wa ushiriki vitakuwa bora zaidi. Hivyo matunda ya sadaka ya Misa Takatifu yatapatikana zaidi.

Baraza la Maaskofu Katoliki, baada ya kuipitisha tafsiri hiyo kwa Kiswahili na kuipeleka Roma kutambuliwa na baada ya kupata kibali linaagiza mafunzo yaanze katika ngazi mbalimbali za watu mara tu kitabu kitakapotoka. Aidha mafunzo hayo yawe endelevu maana yanahusu kitovu cha fumbo la Kanisa Katoliki.

Sheria yeyote iliyotolewa kinyume chake imefutwa.

Imetolewa katika ofisi ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, Dar es Salaam tarehe 20 Juni 2006.



+Severine NiweMugizi

ASKOFU WA RULENGE

RAISI WA BARAZA LA MAAASKOFU KATOLIKI TANZANIA





CONGREGATIO DE CULTU DIVINO  
ET DISCIPLINA SACRAMENTORUM

Prot. N. 1670/05/L

TANZANIAE

Instante Excellentissimo Domino Severino Niwemugizi, Episcopo Rulengensi, Praeside Coetus Episcoporum Tanzaniae, litteris die 29 septembris 2005 datis, vigore facultatum huic Congregationi a Summo Pontifice BENEDICTO XVI tributarum, textum kiswahili Institutionis generalis Missalis Romani, editionis typicae tertiae, prout exstat in adnexo exemplari, perlibenter approbamus seu confirmamus.

In textu imprimendo inseratur ex integro hoc Decretum, quo ab Apostolica Sede petita approbatio conceditur. Eiusdem insuper textus impressi duo exemplaria ad hanc Congregationem transmittantur.

Contrariis quibuslibet minime obstantibus.

Ex aedibus Congregationis de Cultu Divino et Disciplina Sacramentorum, die 22 decembris 2005.

  
(+ Franciscus Card. Arinze)  
Praefectus

  
( D. Marius Marini )  
Subsecretarius



CONGREGATIO DE CULTU DIVINO  
ET DISCIPLINA SACRAMENTORUM

Prot. N. 1670/05/L

DIOECESIUM TANZANIAE

Textus Institutionis Generalis Missalis Romani,  
editionis typicae tertiae  
lingua kiswahili exaratus

Confirmatum

Ex aedibus Congregationis de Cultu Divino  
et Disciplina Sacramentorum

die 22 decembris 2005

( D. nus Marius Marini )  
Subsecretarius

# **URATIBU MKUU WA MISALE YA KIROMA**

**2002**



# UTANGULIZI

1. Kristo Bwana alipofikia ile saa ya kuadhimisha Karamu ya Pasaka pamoja na wanafunzi wake, karamu ambamo aliweka sadaka ya Mwili na Damu yake, aliagiza kiandaliwe chumba kikubwa cha karamu kilichopambwa (Lk 22:12). Daima Kanisa limeelewa kuwa agizo lile hulihusu lenyewe pia, linapopanga yale mambo yanayotakiwa katika kuandaa roho za watu, mahali, riti, na matini kwa ajili ya kuadhimisha Ekaristi Takatifu. Na hata kanuni za siku hizi ambazo zimeagizwa kulingana na matashi ya Mtaguso Mkuu wa Vatikano II, ikiwa ni pamoja na hii Misale mpya, ambayo Kanisa la Riti ya Kiroma litaitumia tangu sasa katika kuadhimisha Misa, ni uthibitisho tena wa huo uangalifu wa Kanisa, wa imani yake isiyobadilika, na wa upendo wake kwa Fumbo Kuu la Ekaristi Takatifu. Pia ni ushuhuda wa mapokeo ya Kanisa ambayo yameunganika na kuendelea bila kukatizwa, ingawa kuna mambo mapya machache yaliyoingizwa.

## **Ushuhuda wa imani isiyobadilika**

2. Hulka ya Misa ya kuwa sadaka, ilivyotangazwa kwa mkazo na Mtaguso wa Trento<sup>1</sup> ambayo ililingana na mapokeo ya Kanisa, ilitangazwa tena na Mtaguso wa Vatikano II kwa kutamka maneno haya yenye maana sana kuhusu Misa: “Mwokozi wetu, katika Karamu ya mwisho, aliweka sadaka ya Ekaristi takatifu ya Mwili na Damu yake, ambayo kwa sadaka hiyo angeendeleza sadaka ya Msalaba nyakati zote, mpaka atakaporudi, kusudi amdhaminie Kanisa Bibiarusi wake mpendwa, ukumbusho wa kifo chake na ufufuko wake”<sup>2</sup>.

Haya yanayofundishwa hivyo na Mtaguso ndiyo yanayoelezwa tena na tena katika fomula za Misa. Na vivyo hivyo, fundisho hili linaelezwa kwa mkazo kwa sentensi ilivyokuwako tayari, katika Sakramentario ya zamani iliyoitwa “Leoniano” kwa lugha ya kawaida. Sentensi hii inasema: “Kila unapoadhimishwa ukumbusho wa sadaka hii, kazi ya ukombozi wetu hufanyika.”<sup>3</sup> Na haya ndiyo yanayoelezwa kwa uwazi kabisa na uangalifu

katika Sala za Ekaristi; kwani katika Sala hizi kuhani anapotimiza anamnesi ("ukumbusho") kwa kumwelekea Mungu kwa niaba ya watu wote pia, humpa shukrani na kumtolea sadaka iliyo hai na takatifu; yaani matoleo ya Kanisa na kafara ambayo kwa njia yake Mungu mwenyewe alitaka kuridhishwa.<sup>4</sup> Na hapo kuhani husali ili Mwili na Damu ya Kristo viwe sadaka inayompendeza Baba na yenye kuleta wokovu kwa ulimwengu mzima.<sup>5</sup>

Kwa namna hiyo, katika Misale mpya, Kanuni ya Kanisa ya "kusali" (**lex orandi Ecclesiae**) huendana na Kanuni yake yenye kudumu ya "kusadiki."(**lex credendi**) Kwa kanuni hii tunaonywa kwamba, sadaka ni moja, na ni ileile ya msalaba, na ndiyo yenye kurudiwa "kisakramenti" katika Misa, isipokuwa kwa namna tofauti ya kutolea. Ndiyo sadaka aliyoanzisha Kristo Bwana katika Karamu ya mwisho na kuwaagiza Mitume wafanye hivyo kwa ukumbusho wake. Na kwa sababu hiyo, Misa, kwa pamoja, ni: sadaka ya sifa, tendo la shukrani, sadaka ya kuomba huruma na ya malipizi.

**3.** Hali kadhalika, fumbo la ajabu la uwepo wa Bwana katika maumbo ya kiekaristi, limethibitishwa na Mtaguso wa Vatikano II,<sup>6</sup> na kwa hati nyingine za Magisterio ya Kanisa,<sup>7</sup> kwa maana, na kwa namna ileile kama Mtaguso wa Trento ulivyokuwa umeagiza fumbo hilo liaminiwe.<sup>8</sup> Na, fumbo hilihili hutangazwa katika adhimisho la Misa, siyo tu kwa njia ya maneno yenyewe ya *konsekrasio* ambayo kwa njia yake Kristo hufanywa awepo kwa geuzo la mageuzo-uwemo (**transubstantiatio**), lakini pia kwa kutambua na kuhisi uwepo wake, na kuudhahirisha kwa kutoa heshima kuu na kumwabudu, jinsi vinavyoelekezwa vifanyike katika Liturujia ya Ekaristi Takatifu. Kwa sababu hiyohiyo, Siku ya Alhamisi Kuu katika Karamu ya Bwana na kwenye Sherehe ya Mwili na Damu ya Bwana, Wakristo wahimizwe wazidi kuiabudu kwa namna ya pekee Sakramenti hii ya ajabu.

**4.** Aidha, tabia ya ukuhani wa huduma, ambao ni maalum kwa Maaskofu na Mapadri wenye kutolea sadaka katika nafsi yake

Kristo, na kulisimamia kusanyiko la taifa takatifu, hudhihirishwa katika fomula ya ile ibada-kanuni yenyewe; kwa nafasi ya heshima zaidi wanayopewa; na pia kwa kazi yenyewe ya ukuhani wao. Nazo sababu za msingi za jukumu hilo zinatangazwa na kufafanuliwa bayana na kwa kina katika tendo rasmi la shukrani au Prefasio ya Misa ya Krisma, siku ya Alhamisi ya Juma Kuu, siku ambayo inaeleweka wazi kuwa ndiyo siku ya kukumbuka kuwekwa kwa ukuhani. Katika sala ile, inaelezwa kule kushushiwa nguvu ya ukuhani kunakofanyika kwa kuwekwa mikono; na tena uwezo huo unafafanuliwa kwa kutaja kazi pekepeke zinazohusika, na ni uwezo ambao ni maendelezo ya ule uwezo wake Kristo, aliye Kuhani Mkuu wa Agano Jipya.

**5.** Lakini tabia hiyo ya ukuhani wa huduma huufanya ule ukuhani mwingine, ambao nao ni jambo kubwa na muhimu, uonekane katika mwanga wake, yaani ukuhani wa kifalme wa waamini, ambao dhabihu yao ya kiroho hukamilishwa kwa njia ya huduma ya Askofu na ya Mapadri, kwa kuunganishwa na dhabihu ya Kristo aliye Mshenga pekee.<sup>9</sup> Kwa maana adhimisho la Ekaristi Takatifu ni tendo la Kanisa zima; ambamo kila mmoja hutenda kilicho cha mmoja, na yote yaliyo yake, anapofanya kile kinachomhusu yeye, kwa kuzingatia nafasi yake katika taifa la Mungu. Hii ndiyo sababu ya kuangalia kwa makini zaidi mambo kadha wa kadha, ambayo katika mtiririko wa karne, yalikuwa hayatiliwi mkazo sana. Kwa maana, hao watu ndio taifa la Mungu, lililokombolewa kwa Damu ya Kristo, likakusanywa na Bwana na kulishwa kwa neno lake. Hawa ndio watu walioitwa ili kumwinulia Mungu maombi ya familia nzima ya wanadamu; hawa ndio watu wenye kutoa shukrani katika Kristo kwa ajili ya fumbo la wokovu kwa kutoa sadaka yake; hatimaye, ndio watu ambao kwa njia ya Komunyo ya Mwili na Damu ya Kristo, wanaimarishwa katika umoja. Watu hawa, ingawa ni watakatifu kutokana na chimbuko lao, bado wanakua zaidi na zaidi katika utakatifu kwa kushiriki katika fumbo la

Ekaristi Takatifu kwa namna yenye ufahamu, ya utendaji hai, na yenye kuzaa matunda.<sup>10</sup>

## **Mapokeo yasiyokatizwa yathibitishwa**

6. Mtaguso wa Vatikano II ulipotangaza sheria ambazo kwa zenyewe Kanuni ya Misa (**Ordo Missae**) inatakiwa kurekebishwa, kati ya mambo mengine uliagiza pia ibada-kanuni nyingine itengenezwe upya kulingana na “taratibu za kale za Mababa watakatifu”<sup>11</sup>, yaani yatumike maneno yaleyale kama yalivyoandikwa na Mt. Pius V katika Hati yake ya Kitume ‘**Quo Primum**’ ambayo kwa yenyewe Misale ya Trento ilitangazwa mwaka 1570. Kutokana na ulinganifu huu wa maneno, inaweza kuthibitishwa kwamba Misale hizi mbili za Kiroma, hata kama zinatengwa na karne nne zina mapokeo yaleyale, na yenye kulingana. Hata kama vipengele vya msingi vya ndani vya mapokeo vinafikiriwa, itaeleweka pia jinsi ile Misale ya kwanza inavyokamilishwa vizuri na vikubwa na hii ya pili.

7. Wakati wa nyakati zile zilizokuwa za shida sana, ambapo imani ya kikatoliki kuhusu hulka ya Misa ya kuwa sadaka, kuhusu ukuhani wa huduma, na wakati ambapo uwepo halisi na wa kudumu wa Kristo katika maumbo ya Ekaristi Takatifu vilikuwa vinatiliwa mashaka, ilikuwa nia maalumu ya Mtakatifu Pius V kuyalinda mapokeo ya hivi karibuni yaliyokuwa yakipingwa bila haki. Hivyo, aliingiza mabadiliko machache tu katika ibada-kanuni takatifu. Kwa kweli, Misale ile ya 1570 inatofautiana kidogo sana na ile iliyochapwa 1474, ambayo inarudia tena kwa uaminifu ile Misale ya wakati wa Papa Innosenti III. Zaidi ya hayo, magombo ya Maktaba ya Vatikano, ingawa mara nyingine ilisaidia kuingiza tungo bora na sahihi zaidi, hata hivyo, kamwe hazikuruhusu kule "kuchunguza waandishi wa zamani" kuthaminiwe zaidi kuliko yale mafafanuzi ya kiliturujia ya Karne za Kati.

8. Kinyume chake, leo, ile “kanuni ya Mababa Watakatifu” waliyoifuata warekebishaji wa Misale ya Mt. Pius V,

imetajirishwa kwa maandishi yasiyo na idadi ya wasomi. Kwani, baada ya Sakramentario ijulikanayo kwa jina “Gregorianum” kuchapishwa mara ya kwanza mwaka 1571, Sakramentario za zamani za Kiroma na za Kiambrosiana, zilichapishwa mara kwa mara baada ya kuchunguzwa na kuhakikiwa. Ndivyo ilifanyika pia kwa vitabu vya zamani vya Kihispania na vya Kigalia (Kifaransa), ambavyo viliweka hadharani sala nyingi zenye umuhimu usio mdogo kwa upande wa kiroho. Sala hizi hazikuwa zinajulikana hadi wakati huo.

Kwa hali hiyohiyo, sasa mapokeo ya karne za kwanza kabla ya kuundwa Riti za Mashariki na Magharibi, hujulikana vizuri zaidi, kutokana na kugunduliwa hati nyingi hivyo za kiliturujia.

Zaidi ya hayo, maendeleo makubwa katika taaluma ya Mababa watakatifu yametilia mwanga teolojia ya fumbo la Ekaristi Takatifu kwa mwanga wa mafundisho ya Mababa maarufu sana wa nyakati za awali za Ukristo, kama vile Mt. Ireneo, Mt. Ambrosi, Mt. Sirili wa Yerusalemu, na Mt. Yohane Krisostomi.

**9.** Kwa sababu hiyo, “kanuni ya Mababa watakatifu” haidai tu yahifadhiwe yale tuliyopokea, ambayo babu zetu wa karibu wanaturithisha, bali yashikwe na kuthaminiwa zaidi mambo yote ya zama zote za Kanisa, na namna zote ambazo kwa hizo imani yake moja tu ilitangazwa kwa njia mbalimbali za utamaduni wa kibinadamu, na za kijamii zinazotofautiana kati yake, kama zile zilizokuwa katika nchi za Wasemitiki, au Wagriki, au Warumi (Walatini). Mtazamo huu mpana zaidi unatuwezesha kutambua jinsi gani Roho Mtakatifu anawajalia watu wa Mungu uaminifu wa ajabu katika kutunza hazina-tunu ya imani isiyobadilika, ingawa kuna namna nyingi sana za sala na ibada-kanuni.

## **Marekebisho kulingana na Mazingira Mapya**

**10.** Basi Misale hii mpya, ambayo tayari inashuhudia kanuni ya kusali ya Kanisa la Kiroma, pamoja na kulinda hazina-tunu ya imani iliyotolewa tena kwa njia ya Mitaguso ya karibuni,

yenyewe ndiyo inaonyesha hatua muhimu sana katika mapokeo ya kilituruja.

Mababa wa Mtaguso wa Vatikano II waliporudia tena matamko ya kidogma ya Mtaguso wa Trento waliyatamka wakiwa katika nyakati nyingine zilizo tofauti kabisa. Ndiyo maana katika mambo ya kiuchungaji waliweza kutoa maazimio na mapendekezo ambayo karne nne zilizopita yasingeweza kufikiriwa.

**11.** Mtaguso wa Trento tayari uliwahi kung'amua manufaa makubwa ya kikatekesi yanayopatikana katika adhimisho la Misa; lakini haukuweza kukusanya yote yatokanayo na kuyatumia katika maisha kiutendaji. Kwa kweli kulikuwa na maombi kutoka kwa watu wengi kwamba itolewe ruhusa ya kuweza kutumia lugha ya watu katika kuadhimisha sadaka ya Ekaristi. Lakini mbele ya haja hiyo, Mtaguso, kwa kuzingatia mazingira ya wakati ule, uliamua kuwa wajibu wake ulikuwa kusisitiza tena mafundisho ya kawaida ya Kanisa, ambayo yanasema kuwa Sadaka ya Ekaristi, kwanza ni tendo la Kristo mwenyewe, ambalo nguvu yake haiathiriwi hata kidogo na jinsi ya kushiriki kwa waamini. Ndiyo maana Mtaguso ule ulitamka maneno haya ambayo, kwa pamoja ni thabiti na yamesemwa vizuri: "Ingawa Misa inayo mafundisho makubwa ya kuwalea watu wanaoamini, hata hivyo Mababa hawakuona ni vema iadhimishwe kwa lugha za watu wenyeji popote pale."<sup>12</sup> Halafu tena ulitangaza kuwa alaaniwe yeyote anayefikiri kuwa: "ni lazima kukataza Riti ya Kanisa la Roma ambayo inaruhusu sehemu za Sala ya Ekaristi, na maneno ya konsekrasio yatamkwe kwa sauti isiyosikika; au kwamba Misa lazima iadhimishwe tu kwa kutumia lugha ya watu."<sup>13</sup> Hata hivyo, Mtaguso ulipokataza lugha ya watu isitumike katika Misa, wakati huohuo uliagiza wachungaji wa watu watoe katekesi badala yake, kadiri inavyofaa: "Ili kundi la kondoo wa Kristo wasione njaa ... Mtaguso Mkuu unawaamuru wachungaji na wote wenye kubeba majukumu ya kutunza roho za watu, mara nyingi katika maadhimisho ya Misa kwa ajili yao wenyewe, au

kwa ajili ya wengine, watoe maelezo juu ya yale yasomwayo katika Misa. Pia wafafanue, kati ya mengineyo, fumbo moja au jingine la sadaka hii takatifu sana, hasa katika siku ya Dominika na Sikukuu.”<sup>14</sup>

**12.** Mtaguso wa Vatikanu II uliokusanyika ili kulinganisha majukumu yake ya kitume na haja za wakati huu, ulichunguza kwa undani, kama ulivyofanya ule wa Trento, tabia ya kimapundisho na ya kiuchungaji ya Liturujia takatifu.<sup>15</sup> Na, maadam hapakuwepo tena mkatoliki yeyote aliyekuwa anakataa uhalali na uwezeshwaji wa kutumia ibada-kanuni takatifu kwa lugha ya kilatini, Mtaguso uliweza pia kutamka kwamba “si mara chache matumizi ya lugha ya wananchi huweza kuwafaa sana waamini,” na hivyo ukatoa idhini ili itumike.<sup>16</sup> Hamu kubwa ambayo kwa ajili yake kibali hiki kilipokewa popote, ilisababisha maadhimisho yote ya kiliturujia ambamo watu wanashiriki, yaweze kutekelezwa kihalali chini ya uongozi wa Maaskofu na Kiti cha Kitume yafanyike kwa kutumia lugha ya watu, na hivyo kulifanya fumbo linaloadhimishwa kueleweka kikamilifu zaidi.

**13.** Lakini, kwa vile matumizi ya lugha ya wananchi ni chombo tu – ingawa cha maana sana – ili kuweza kutoa kwa uwazi zaidi katekesi ya fumbo, ambayo imo ndani ya adhimisho lenyewe, Mtaguso wa Vatikanu II ulielekeza kuwa yatekelezwe maagizo mengine ya Mtaguso wa Trento, ambayo yalikuwa hayajazingatiwa kila mahali, kama vile, ulazima wa kuwa na homilia siku za Dominika na Sikukuu,<sup>17</sup> na uwezekano wa kuingiza maneno ya maelekezo katikati ya ibada-kanuni takatifu yenyewe.<sup>18</sup>

Kwa yakini, huu Mtaguso maarufu wa Vatikanu II ambao unashauri kwamba “ushiriki katika Misa unakuwa mkamilifu zaidi, pale ambapo waamini, baada ya Komunyo ya kuhani, wanapokea Mwili wa Bwana kutoka sadaka ileile,”<sup>19</sup> ulihimiza hivyo kwa lengo la kuweka katika matendo agizo jingine la Mababa wa Trento kwamba, ili kushiriki Ekaristi Takatifu kwa ukamilifu zaidi, katika kila Misa “waamini waliopo wasipokee

Ekaristi Takatifu kwa tamaa tu, bali pia katika maumbo ya Sakramenti”.<sup>20</sup>

**14.** Kwa msukumo wa roho hiyohiyo na juhudi hiyohiyo ya kichungaji, Mtaguso wa Vatikano II uliweza kutathmini upya yale yaliyoamuliwa na Mtaguso wa Trento kuhusu Komunyo chini ya maumbo yote mawili. Maadamu leo hii misingi ya mafundisho kuhusu utimilifu wa Komunyo ikipokewa chini ya umbo la mkate tu haitiliwi mashaka yoyote, Mtaguso uliruhusu katika nafasi kadha wa kadha Komunyo ipokewe chini ya maumbo yote mawili. Kwa njia hii, kwa vile umbo la kisakramenti linajitokeza zaidi, inatolewa nafasi pekee ya waamini kuelewa zaidi fumbo wanalolishiriki.<sup>21</sup>

**15.** Hivyo, kwa kuyakubali na kuyashika hayo, Kanisa limebaki aminifu katika jukumu lake la kuwa mwalimu wa ukweli, likihifadhi “ya kale,” yaani hazina ya mapokeo. Pia linatimiza kazi yake ya kuchunguza na kuyatumia kwa busara “yale yaliyo mapya” (*rej. Mt 13:52*)

Sehemu mojawapo ya Misale mpya inapanga kwa uwazi zaidi Sala za Kanisa kulingana na mahitaji ya nyakati zetu. Sala za aina hii ni zile Misa za Kuadhimisha Sakramenti na Misa kwa ajili ya Shida Mbalimbali ambazo ndani yake “mapokeo” na “upya” vinaoana barabara. Kwa hiyo, pamoja na kwamba misemo mingi imebaki ni ileile iliyochotwa kutoka mapokeo ya kale ya Kanisa, na iliyozoeleka kutokana na kuchapishwa mara nyingi, vilevile katika Misale ya Kiroma, misemo mingine mingi ilirekebisha kulingana na mahitaji na mazingira ya siku hizi. Misemo mingine tena, kwa mfano, Sala kwa ajili ya Kanisa, kwa ajili ya walei, kwa ajili ya kutakatifuza kazi ya watu, kwa ajili ya jumuiya ya mataifa yote, kwa ajili ya mahitaji yaliyo hasa ya nyakati zetu, hii yote imetungwa upya kabisa, kwa kutumia mawazo, na mara nyingi pia maneno yenyewe ya Hati za Mitaguso ya hivi karibuni.

Aidha, kulingana na hali mpya ya ulimwengu ulivyo sasa, ilionekana kuwa hazina ile tukufu haitadhurika kwa kuzitumia



matini za mapokeo ya kale na kubadili sentensi moja moja, ili misemo yenyewe ilingane zaidi na lugha ya teolojia ya leo, na ipate kushuhudia kwa kweli hali ya sasa ya mafundisho ya Kanisa. Ndiyo maana misemo mingine kuhusu namna ya kuthamini na kutumia mali za dunia, na mingineyo yenye kudokeza muundo wa toba ya nje ilivyokuwa nyakati nyingine za Kanisa, ilibadilishwa.

Hatimaye, kanuni za kiliturujia za Mtaguso wa Trento zimetimilizwa kwa namna hiyo, na kukamilishwa katika sehemu nyingi na kanuni za Mtaguso wa Vatikano II. Na kazi ya Mtaguso huu ilitimiza zile juhudi za kuwahusisha zaidi waamini na Liturujia takatifu, juhudi ambazo zilifanyika kwa kipindi cha karne nne hivi, na kwa ari zaidi katika nyakati za karibuni, hasa kutokana na jitihada ya kiliturujia aliyohimiza Mt. Pius X na waandamizi wake.

## Sura ya Kwanza

### UMAARUFU NA UKUU WA ADHIMISHO LA EKARISTI TAKATIFU

**16.** Adhimisho la Misa takatifu ambalo ni utendaji wa Kristo na taifa la Mungu lililoundwa kihierarkia, ndiyo kiini cha maisha yote ya kikristo, kwa Kanisa lote au kwa Kanisa mahalia; na kwa waamini wote kila mmoja peke peke.<sup>22</sup> Katika adhimisho hilo, ndipo kilele cha utendaji wa Mungu, ambamo Mungu huutakatifuza ulimwengu katika Kristo, na ni kilele cha ibada ambayo wanadamu humtolea Baba, kwa kumwabudu kwa njia ya Kristo Mwana wa Mungu, katika Roho Mtakatifu.<sup>23</sup> Pamoja na hayo, katika adhimisho hili, mafumbo ya wokovu yanakumbukwa katika mzunguko wa mwaka, hivyo kwamba kwa namna fulani mafumbo haya yanafanywa yawepo tena.<sup>24</sup> Nayo matendo mengine matakatifu, na kazi zote za maisha ya Kikristo vinaunganika nalo; vinatiririka kutoka huko, na vinapangwa kuelekea huko.<sup>25</sup>

**17.** Kwa ajili hiyo, ni muhimu sana adhimisho la Misa takatifu au Karamu ya Bwana lifanywe hivyo kwamba wahudumuo vitakatifu na waamini wanashiriki adhimisho hilo kila mmoja kwa kadiri ya hali yake, ili wapate mavuno mengi<sup>26</sup> ambayo Kristo Bwana alitaka kuwapatia kwa kuiweka Sadaka ya Ekaristi takatifu ya Mwili na Damu yake. Naye aliliachia Kanisa Bibiarusi wake mpendwa mno, sadaka hii, kama ukumbusho wa mateso na Ufufuko wake.<sup>27</sup>

**18.** Na hili litafanyika ipasavyo ikiwa hali na mazingira ya kila kusanyiko la kiliturujia vitawekwa maanani, na adhimisho lote litaandaliwa hivi kwamba litawaongoza waamini washiriki kwa utendaji hai na mkamilifu, yaani kwa mwili na roho; liwe limechochewa lipate kuwaka kwa imani, matumaini na mapendo. Kushiriki kwa namna hiyo ndiko kunatamaniwa sana na Kanisa, na tena kunadaiwa na hali yenyewe ya adhimisho,

na ni haki na wajibu walio nao taifa la kikristo kutokana na Ubatizo wao.<sup>28</sup>

**19.** Ingawa uwepo wa waamini na ushiriki wao hai vinaonyesha hulka ya kikanisa ya adhimisho,<sup>29</sup> mara nyingine haiwezekani wawepo. Hata hivyo, adhimisho la Ekaristi Takatifu linabaki bado ni lenye kuleta manufaa yake, na hadhi yake inabaki ileile daima, kwa maana ni tendo la Kristo na Kanisa, ambamo kuhani anatimiza jukumu lake maalum na kuu, na daima hutenda kwa ajili ya wokovu wa watu.

Ndiyo maana yeye mwenyewe huhimizwa kuadhimisha sadaka ya Ekaristi Takatifu hata kila siku, kadiri inavyowezekana.<sup>30</sup>

**20.** Kwa vile adhimisho la Ekaristi Takatifu – hata na Liturujia yote – hufanyika kwa ishara na vitu vinavyogusa mwili, na vyenye kulisha, kuimarisha na kudhihirisha imani<sup>31</sup>, ni lazima kuwa na uangalifu mkubwa sana wa kuchagua kwa busara ile miundo na vitu vya msingi (**elementa**) vilivyopendekezwa na Kanisa. Vichaguliwe na viratibishwe vile ambavyo - kwa kuzingatia mazingira ya watu na mahali - vitafanya ushiriki uwe mkamilifu zaidi, na wa vitendo, pamoja na kukidhi vizuri zaidi mahitaji ya kiroho ya waamini.

**21.** Basi uratibu huu una lengo hili: kwanza kutoa mwongozo wa jumla ambao unaonyesha kwa jumla utaratibu wa maadhimisho ya Ekaristi Takatifu. Pili, kutoa kanuni zinazohusu sehemu mbalimbali za Ekaristi Takatifu.<sup>32</sup>

**22.** Walakini, adhimisho la Ekaristi Takatifu katika Kanisa mahalia kwa kweli ndilo tendo kuu kuliko yote.

Kwani Askofu wa Jimbo, ambaye ni mgawaji wa kwanza wa mafumbo ya Mungu katika Kanisa alilokabidhiwa, ndiye kiongozi, mhimizaji na mtunzaji (mlinzi) wa maisha yote ya kiliturujia.<sup>33</sup> Fumbo la Kanisa hudhihirishwa katika maadhimisho anayoyaongoza yeye, hasa adhimisho la Ekaristi Takatifu, akiwa pamoja na mapadri na mashemasi wake, na waamini

walei. Kwa hiyo maadhimisho hayo makuu ya Misa hayana budi kuwa mfano kwa jimbo zima.

Kutokana na hayo, lazima Askofu afanye juhudi ili mapadri, mashemasi na waamini wakristo walei, wawe na ufahamu wa kweli wa ibada-kanuni na matini za kiliturujia; na hivyo wawezeshwe kutimiza adhimisho la Ekaristi Takatifu kwa utendaji hai na wenye kuleta matunda. Kwa lengo hilo, awe mwangalifu ili maadhimisho yenyewe yafanyike kwa heshima inayostahili na kuyakuza kwa kuongeza uzuri wa mahali patakatifu; na uzuri wa muziki na wa sanaa vichangie kwa vikubwa kadiri inavyowezekana.

**23.** Kwa ajili hiyo pia, katika Uratibu huu wa jumla, na katika Kanuni ya Misa, (**Ordo Missae**), yamewekwa marekebisho na malinganisho kadhaa, ili adhimisho la Misa lifikie kiwango kinachotakiwa na maelekezo na roho ya Liturujia takatifu kwa ukamilifu zaidi, na pia mafanikio ya kiuchungaji yaongezeke.

**24.** Kwa sehemu kubwa, malinganisho haya yanahusu uchaguzi wa ibada-kanuni, au matini fulani, yaani, uchaguzi wa nyimbo, masomo, sala, sentensi au maneno ya kuelekeza na alama zinazotolewa kwa vitendo vya mwili: haya yote yawe yanaweza kuendana vizuri na mahitaji, uwezo na maandalizi ya wale wenye kuhudhuria. Na haya yote ni juu ya kuhani kiongozi kufanya uchaguzi. Lakini kuhani akumbuke kuwa yeye ni mtumishi tu wa Liturujia takatifu, na hivyo haruhusiwi kuongeza, kuondoa au kubadili jambo lolote kwa uamuzi wake binafsi katika adhimisho la Misa.<sup>34</sup>

**25.** Zaidi tena, katika Misale hii, mahali kadhaa panapohusika, inadokezwa malinganisho yanayoweza kufanywa kwa mujibu wa Konstitusio ya Liturujia takatifu kutegemeana na usimamizi wa Askofu wa jimbo, au Baraza la Maaskofu<sup>35</sup> (*rej. Uratibu Mkuu huu nn. 387, 388-393*).

**26.** Kuhusu mabadiliko na malinganisho mazito zaidi, ambayo huhitajika kutokana na mila na fikra za watu, na za mahali, haya huweza kuingizwa kufuatana na nia ya artikulo 40 ya

*Konstitutio* ya Liturujia ya Kiroma <sup>36</sup> na katika Uratibu huu, hapo chini (nn. 395-399).

## **Sura ya Pili**

# **MUUNDO WA MISA, MAMBO YAKE YA MSINGI NA SEHEMU ZAKE**

## **I. MUUNDO WA MISA KWA JUMLA**

**27.** Katika Misa, yaani Karamu ya Bwana, taifa la Mungu linakusanyika katika umoja, likisimamiwa na kuhani anayetenda katika nafsi ya Kristo, ili kuadhimisha ukumbusho wa Bwana, yaani sadaka ya Ekaristi.<sup>37</sup> Kwa sababu hiyo, katika kusanyiko la kimahalia la namna hiyo la Kanisa takatifu, inatimia kwa udhahiri kabisa ile ahadi ya Kristo isemayo: “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao” (Mt 18:20). Kwa maana katika adhimisho la Misa, ambamo sadaka ya msalaba inaadhimishwa,<sup>38</sup> Kristo yupo kweli katika jumuiya ile iliyokusanyika kwa jina lake. Yupo kwa njia ya nafsi ya mhudumu; yupo kwa njia ya neno lake; na yupo katika maumbo ya Ekaristi, ambamo yumo kweli wote mzima, na daima.<sup>39</sup>

**28.** Kwa namna fulani Misa inatokana na sehemu mbili, yaani Liturujia ya Neno na Liturujia ya Ekaristi. Sehemu hizi mbili zimeunganika hivyo kwamba zinaunda tendo moja la kiibada.<sup>40</sup> Maana katika Misa huandaliwa meza ya Neno la Mungu na meza ya Mwili wa Kristo; na kutoka meza hizo waamini wanajengwa na kulishwa.<sup>41</sup> Lakini ibada-kanuni nyingine huanzisha adhimisho na nyingine huhitimisha.

## **II. MAMBO MBALIMBALI YA MSINGI YA MISA**

### **Somo la Neno la Mungu na Maelezo yake**

**29.** Maandiko matakatifu yanaposomwa katika Kanisa, Mungu mwenyewe anaongea na taifa lake; naye Kristo aliyemo katika neno lake, anatangaza Injili.

Kwa hiyo, masomo ya Neno la Mungu, ambayo ni sehemu ya maana sana katika Liturujia, sharti yasikilizwe na wote kwa uchaji. Lakini, ingawa Neno la Mungu katika masomo ya Maandiko matakatifu, linaelekezwa kwa watu wote wa nyakati zote, tena linafahamika kwao, hata hivyo, ufahamu wa ndani zaidi na nguvu ya utendaji wake vinaongezeka kwa njia ya ufafanuzi hai, yaani **homilia**, ambayo ni sehemu ya adhimisho la liturujia.<sup>42</sup>

## **Sala na sehemu nyingine zinazomhusu kuhani**

**30.** Kati ya yale yanayomhusu kuhani, la kwanza ni Sala ya Ekaristi ambayo ni kilele cha adhimisho lote. Kisha zinafuata sala, yaani *Kolekta*, Sala ya kuombea dhabihu na Sala Baada ya kushiriki Komunyo. Sala hizi zinaelekezwa kwa Mungu na kuhani asimamiaye jumuiya, akiwa katika nafsi ya Kristo, kwa jina la taifa lote takatifu na kwa jina la wote waliopo.<sup>43</sup> Kwa hiyo, kwa haki zinaitwa “Sala za yule anayesimamia.”

**31.** Vivyo hivyo, ni kazi ya kuhani, aliye na jukumu la kusimamia jumuiya iliyokusanyika, kutoa mawaidha yaliyomo katika ibadakanuni yenyewe. Pale inapoagizwa na rubrika, kuhani anayeadhimisha huruhusiwa kuyabadilisha kwa namna fulani, ili yalingane na kiwango cha ufahamu wa wale wanaohudhuria. Lakini, daima kuhani azingatie kuhifadhi ile maana ya mawaidha hayo kama ilivyotolewa katika vitabu vya liturujia; na anatakiwa aseme kwa maneno machache. Ni wajibu wa kuhani msimamizi kuongoza tangazo la Neno la Mungu na kutoa baraka ya mwisho. Aidha anaruhusiwa kuwaingiza waamini katika Misa ya siku kwa maneno machache baada ya kuwasalimu watu mwanzoni mwa Misa, na kabla ya tendo la toba. Anaweza kufanya hivyo pia katika Liturujia ya Neno kabla ya masomo na katika Sala ya Ekaristi kabla ya Utangulizi. Lakini kamwe asifanye hivyo wakati wa sala hiyo yenyewe. Hatimaye huweza kumalizia ibada yote takatifu kwa mawaidha yanayofaa kabla ya kuwaaga watu.

**32.** Hulka yenyewe ya sehemu za “msimamizi wa jumuiya” inadai maneno hayo yatamkwe kwa sauti ya kufahamika, yawe wazi, na ya juu, tena yasikilizwe na wote kwa makini.<sup>44</sup> Kwa hiyo sala nyingine au nyimbo zisifanyike wakati kuhani anaposema sehemu hizo; nacho kinanda na vyombo vingine vya muziki vinyamae wakati huo.

**33.** Kwa kweli, kuhani husema sala kama msimamizi kwa jina la Kanisa na la jumuiya yote iliyokusanyika. Lakini anasali sehemu nyingine kwa jina lake binafsi, kusudi aitimize huduma yake kwa uangalifu zaidi na kwa moyo wa ibada. Sala za namna hii, ambazo zinatolewa kabla ya kusoma Injili, wakati wa kuandaa vipaji, na kabla na baada ya kuhani kupokea Ekaristi, zisemwe kwa sauti isiyosikika kwa watu.

### **Fomula nyingine zinazojitokeza katika adhimisho**

**34.** Kwa kuwa adhimisho la Misa kwa hulka na hali yake ni tendo la “kijumuiya,”<sup>45</sup> viitikizano (**dialogia**) kati ya kuhani na waamini waliokusanyika, na pia mashangilio ya shangwe (**acclamationes**), vina maana sana.<sup>46</sup> Kwa hiyo, haya si ishara za nje tu za adhimisho la kijumuiya, bali zinajenga na kukuza uhusiano wa muungano wa ndani (**communio**) kati ya kuhani na waamini.

**35.** Mashangilio au/na vifijo, na viitikizano vya waamini kujibu maamkiano na sala za kuhani, ndivyo vinafanya ile hatua ya ushiriki kimatendo, hatua ambayo katika Misa ya aina yoyote, ni lazima itimilizwe na waamini waliokusanyika, ili kuonyesha na kukoleza utendaji wa jumuiya yote.<sup>47</sup>

**36.** Sehemu nyingine zinazofaa sana kuonyesha na kukuza ushiriki wa waamini kimatendo, na ambazo zinahusisha jumuiya nzima iliyokusanyika, ni hasa tendo la kutubu (**Nakuungamia**), Kukiri Imani (**Nasadiki**); Sala kwa ajili ya mahitaji yote (Sala za waamini); na Sala ya Bwana (**Baba yetu**).

**37.** Hatimaye, kati ya fomula nyinginezo, ziko zifuatazo:



a) Kati ya fomula hizo, kuna Ibada-kanuni, au kitendo kinachosimama chenyewe, kama vile utenzi **Utukufu kwa Mungu Juu**, Zaburi ya majibizano, **Aleluya**, na Aya kabla ya Injili. Nyingine ni **Mtakatifu**, Shangilio la Anamnesi na Wimbo baada ya Komunyo.

b) Ziko na nyingine zinazoandamana na vitendo fulani fulani, kama vile Wimbo wa Maandamano ya kuingia, Wimbo wa kupeleka vipaji, Wimbo wa kumega mkate (**Mwanakondoo**), na Wimbo wa kwenda kushiriki Komunyo.

## **Namna ya kusema Matini mbalimbali**

**38.** Katika matini zinazotakiwa kusemwa kwa sauti ya wazi na ya juu na kuhani au shemasi, au msomaji, au na watu wote, sauti inapaswa kulingana na aina ya matini yenyewe kama ilivyo, yaani kama ni somo, sala, maelekezo, shangilio, au wimbo. Pia sauti ilingane na namna ya adhimisho, na ukuu wa kusanyiko. Licha ya hayo, ni vema kuzingatia pia tabia ya lugha mbalimbali na hali za mataifa.

Kwa hiyo, katika rubrika na sheria zifuatazo, maneno “kusema” au “kutamka” (**dicere vel proferre**), yanapaswa kueleweka kwa kuzingatia kanuni zilizotolewa hapo juu, iwe ni katika kuimba au katika kusema.

## **Umuhimu wa Kuimba**

**39.** Waamini wakristo wanaokusanyika wakiutazamia ujio wa Bwana, wanashauriwa na Mtume waimbe pamoja Zaburi na nyimbo za rohoni (*rej. Kol 3:16*). Kwani kuimba ni dalili ya furaha ya moyoni (*rej. Mdo 2:46*). Ndiyo maana Mtakatifu Agustino kwa haki anasema. “*Kuimba hufanywa na mwenye kupenda*”.<sup>48</sup> Na toka zamani za kale kumekuwa na methali isemayo: “*Anayeimba vizuri, anasali mara mbili.*”

**40.** Kwa hiyo, matumizi ya nyimbo katika adhimisho la Misa, yapewe umuhimu mkubwa, vikiwekwa maanani utamaduni na vipaji mbalimbali vya kila jumuiya ya kiliturujia. Ijapokuwa si lazima kuimba daima sehemu zile zote ambazo kimsingi ni za

kuimbwa (k.m. katika Misa za siku za kawaida), hata hivyo kukosekana kuimba kabisa, kwa upande wa wahudumu na pia kwa waamini, katika maadhimisho ya siku za Dominika na Sikukuu zilizoamriwa, kuchukuliwe kama jambo la kuepokwa kabisa.

Katika kuchagua sehemu za kuimbwa, zichaguliwe zile sehemu zenye maana zaidi hasa zile zinazoimbwa na kuhani, au na shemasi, au na msomaji, na watu wakiitikia; au sehemu zinazoimbwa na kuhani na watu pamoja.<sup>49</sup>

**41.** Nyimbo za **Kigregoriano** zipewe nafasi ya pekee kama mtindo maalum wa Liturujia ya Kiroma, hata kama nyimbo za namna nyingine ni sawa. Aina nyingine za muziki mtakatifu, hasa nyimbo za sauti nyingi (**polyphonia**), hazikatazwi hata kidogo, mradi ziendane na roho ya tendo la kiliturujia, na zikuze ushiriki wa waamini wote.<sup>50</sup>

Ni kweli kwamba waamini kutoka mataifa mbalimbali wanazidi kukutana siku hizi; kwa sababu hiyo yafaa waamini hao wajue kuimba kwa pamoja walau sehemu chache za Kanuni ya Misa kwa lugha ya Kilatini, hasa Kanuni ya Imani na Sala ya Bwana, wakitumia muziki ulio rahisi zaidi<sup>51</sup>.

## **Matendo ya Kiishara na hali za mwili**

**42.** Matendo ya kiishara na hali za mwili toka upande wa kuhani, shemasi, wahudumu, hata watu pia, vinapaswa kuchangia hivyo kwamba adhimisho lote ling'ae kwa uzuri wenye ulinganifu, na kwa heshima yenye ustahivu, ambamo maana kamili na halisi ya sehemu zote mbalimbali inatambulikana; na ushiriki hai wa waliohudhuria unastawishwa na kukolezwa.<sup>52</sup> Kwa hiyo inapasa yafuatwe haya yaliyoainishwa katika Uratibu huu wa jumla, na pia utaratibu wa mapokeo ya Riti ya Kiroma, kwa ajili ya manufaa ya kiroho ya taifa lote la Mungu, kuliko kufuata mwelekeo wa mtu binafsi, au chaguo la mtu peke.

Kuwa na hali ya namna moja ya mwili inayopaswa kushikwa na wote wanaoishiriki, ni ishara ya umoja wa wanajumuiya ya Kikristo waliokusanyika kwa ajili ya Liturujia takatifu; kwani hii inaonyesha nia na mawazo ya washiriki hao; aidha inalisha nia hiyo na mawazo hayo.

**43.** Waamini wanasimama toka mwanzo wa wimbo wa maandamano ya kuingia, au wakati kuhani anapoingia altareni, mpaka mwisho wa Kolekta. Wanasimama kwa wimbo **Aleluya** kabla ya Injili; na muda Injili yenyewe inapotangazwa. Pia, wanasimama wakati wa kuungama Imani na wakati wa maombi kwa wote; na toka mwaliko **Salini Ndugu** kabla ya Sala juu ya Dhabihu, mpaka mwisho wa Misa, isipokuwa nafasi zitakazotajwa hapo chini.

Lakini wanaketi wakati wa masomo kabla ya Injili na kwa Zaburi ya kuitikizana, kwa homilia na wakati vipaji vinatayarishwa. Pia wanaketi, kadiri ya nafasi wakati wa ukimya mtakatifu unaofanyika baada ya kushiriki Komunyo.

Lakini wapige magoti kwenye *konsekrasio*, isipokuwa kwa sababu ya afya, au ya msongamano wa umati wa watu, au kwa sababu nyingine zinazowazuia. Walakini wale ambao hawapigi magoti wakati wa *konsekrasio*, wainame sana kuhani anapopiga goti baada ya *konsekrasio*.

Pamoja na hayo, ni juu ya Baraza la Maaskofu kulinganisha, kwa mujibu wa sheria, ishara na hali za mwili zilizotajwa katika Kanuni ya Misa, na utamaduni na desturi zinazoeleweka za watu.<sup>53</sup> Ila tena, ni lazima ishara zote ziangaliwe zilingane na maana na hulka ya kila sehemu ya adhimisho. Pale ambapo ni kawaida kupiga magoti kwa muda wote kati ya wimbo **Mtakatifu** mpaka mwisho wa Sala ya Ekaristi, desturi hiyo iendelezwe na kusifiwa.

Kwa ajili ya kuwa na namna moja ya ishara na hali za mwili katika adhimisho lilelile, waamini wafuate mialiko ambayo shemasi au mhudumu mlei, au kuhani anatoa, kuendana na miongozo ya Misale.

**44.** Miongoni mwa ishara za kimatendo, vinahesabiwa pia vitendo na maandamano ambayo kwa hayo kuhani pamoja na shemasi na watumishi wanaijongea altare; shemasi anavyokipeleka kitabu cha Injili kwenye mimbari kabla ya kuitangaza Injili; waamini wanavyopeleka vipaji altareni; au wanavyokwenda kupokea Komunyo. Inafaa vitendo vya namna hiyo na maandamano ya aina hiyo vifanyike kwa utaratibu, huku zikiimbwa nyimbo zinazohusika, kulingana na kanuni zilizowekwa kwa kila kitendo.

## **Kuhusu Ukimya**

**45.** Hali kadhalika, ukimya mtakatifu ufanywe wakati wake, kama sehemu ya adhimisho.<sup>54</sup> Aina yake inategemea wakati unapotokea katika kila adhimisho. Kwa mfano, katika tendo la kufanya toba na baada ya mwaliko wa kusali **Tuombe**, kila mmoja anajirudia na kujitazama kwa ndani. Lakini baada ya somo, au baada ya homilia, kila mmoja anatafakari kwa kifupi yale aliyoyasikia. Na baada ya Komunyo, kila mmoja anamsifu Mungu moyoni mwake na kusali.

Hata kabla ya kuanza adhimisho lenyewe, kushika ukimya kanisani, katika sakristia na maeneo ya jirani na hapo, ni jambo lenye sifa, ili wote wajiweke tayari kuadhimisha matakatifu sawasawa, na kwa ibada.

## **III. KUHUSU SEHEMU MOJA MOJA ZA MISA**

### **A) IBADA-KANUNI ZA KUENZIA**

**46.** Ibada-kanuni inayotangulia Liturujia ya Neno, yaani maingilio, maamkiano, tendo la toba, **Bwana utuhurumie, Utukufu** na **Kolekta**, ina hulka ya maingilio, utangulizi na ya maandalizi.

Lengo la ibada hizi ni kuwaandaa waamini waliokutanika pamoja waunde ushirika, ili wawe tayari kusikiliza Neno la Mungu kwa namna inavyotakiwa, na kuadhimisha Ekaristi takatifu jinsi inavyostahili.

Katika maadhimisho fulani fulani ambayo huunganika na Misa kulingana na miongozo ya vitabu vya kiliturujia, Ibada-Kanuni za kuanzia huachwa, au zinafanywa kwa namna tofauti ya kipekee.

## **Kuingia**

**47.** Watu wakiisha kusanyika, wakati kuhani anapoingia pamoja na shemasi na wahudumu, wimbo wa kuingia unaanzishwa. Lengo la wimbo huo ni kufungua adhimisho, kuimarisha umoja wa waliokusanyika, kuelekeza mioyo na akili zao kwenye fumbo la kipindi cha liturujia, au fumbo la sikukuu, pamoja na kusindikiza maandamano ya kuhani na wahudumu.

**48.** Wimbo huo unaimbwa na kikundi cha waimbaji wakipokezana na watu, au kwa namna hiyohiyo unaimbwa na mwimbaji-kiongozi pamoja na watu; au unaimbwa na watu wote, au na kikundi cha waimbaji tu. Yawezekana kutumia antifona na Zaburi yake kama ilivyo katika *Graduale* ya Kirumi au katika *Graduale* Ndogo, au wimbo mwingine unaoendana na tendo takatifu au unaoendana na hali ya siku au kipindi.<sup>55</sup> Matini za nyimbo hizo sharti ziwe zimekubaliwa na Baraza la Maaskofu.

Ikiwa wimbo wa kuingia hauimbwi, antifona iliyo katika Misale husomwa na waamini, au na baadhi yao tu, au na msomaji, au kama hakuna mwingine inasomwa na kuhani mwenyewe, ambaye huweza pia kuitumia kama mawaidha ya mwanzo (*rej. n. 31*) kwa kuirekebisha.

## **Kuisalimu altare na watu waliokusanyika**

**49.** Kuhani na shemasi na wahudumu wafikapo patakatifuni, husalimia altare kwa kuiinamia sana. Lakini, ili kuonyesha heshima inayopasa kwa altare hiyo, kuhani na shemasi huibusu. Na ikiwa ubani unatumika, kuhani anaifukizia ubani altare na msalaba.

**50.** Wimbo wa kuingia ukimalizika, kuhani, akiwa amesimama penye kiti chake, hufanya Ishara ya Msalaba, yeye pamoja na

kundi lote. Halafu kuhani hutoa alama ya uwepo wa Bwana kwa jumuiya iliyokusanyika kwa kuwasalimu. Kwa njia ya huko kusalimu, na watu kuitikia, fumbo la Kanisa lililokusanyika linaonyeshwa wazi.

Baada ya kuwasalimia watu, kuhani au shemasi, au mhudumu mlei, huweza kuwaingiza waamini katika Misa ya siku hiyo kwa maneno machache kabisa.

## **Tendo la Toba**

**51.** Halafu kuhani huwaalika watu wafanye tendo la toba, ambalo baada ya kitambo kidogo cha ukimya, hutimizwa kwa fomula ya maungamo ya jumla, na kuhitimishwa kwa maneno ya maondoleo yasemwayo na kuhani. Maneno haya lakini hayana nguvu ile ya Sakramenti ya Kitubio.

Siku za Dominika, hasa kipindi cha Pasaka, badala ya tendo la toba ilivyo kawaida, inawezekana kubariki maji na kuwanyunyizia waamini, kama kumbukumbu la ubatizo.<sup>56</sup>

## **Bwana, Utuhurumie**

**52.** Baada ya tendo la toba, daima huanza ***Bwana Utuhurumie (Kyrie)***, isipokuwa kama tayari ilikwisha kusemwa katika tendo la toba lenyewe. Kwa vile ni wimbo ambamo waamini wanamsifu Bwana, na kumsihi rehema yake, kwa kawaida unaimbwa na wote, pengine kwa kupokezana kati ya watu wote na kikundi cha waimbaji, au mwimbaji mmoja.

Kwa kawaida ***Kyrie*** huimbwa mara mbili. Hata hivyo inaweza kuimbwa mara nyingi zaidi au kurefushwa kulingana na muundo wa lugha mbalimbali, au usanii wa muziki, au mazingira. *Kyrie* inapoimbwa kama sehemu ya tendo la toba hutanguliwa na maneno mafupi (*tropus*).

## **Utukufu kwa Mungu juu**

**53. *Utukufu*** ni utenzi wa kale sana na wenye kuheshimiwa sana, ambamo Kanisa linalokusanyika katika Roho Mtakatifu, humtukuza Baba na Mwana kondoo, na linawasihi. Maneno ya

utenzi huu hayawezi kubadilishwa na matini nyingine. Wimbo huu huanzishwa na kuhani; au, ikionekana inafaa, huanzishwa na mwimbaji au na kikundi cha waimbaji; halafu huimbwa na waamini wote pamoja, au na watu wakiitikiana na kikundi cha waimbaji, au na kikundi chenyewe cha waimbaji. Ikiwa hauimbwi, ni lazima usemwe na watu wote pamoja, au na makundi mawili yanayopokezana.

Utenzi huu huimbwa au kusemwa siku za Dominika zisizo za Majilio wala za Kwaresima, na pia katika sherehe na sikukuu, na katika maadhimisho ya pekee na yenye fahari zaidi.

### ***Kolekta: (Sala ya kutimiliza Ibada-Kanuni ya Kuanzia)***

**54.** Baada ya ***Utukufu***, kuhani huwaalika watu kuomba. Na wote, pamoja na kuhani, wanakaa kimya kwa muda mfupi ili wajitambue kuwa wako mbele ya Mungu, na pia waweze kufanya maombi yao ya pekee moyoni. Ndipo kuhani anasema ile sala ambayo tumezoea kuiita ***Kolekta***. Kwa sala hii, hali au mwelekeo wa adhimisho unatambulishwa. Kutokana na mapokeo ya zamani ya Kanisa, kwa kawaida sala hiyo huelekezwa kwa Mungu Baba kwa njia ya Yesu Kristo katika Roho Mtakatifu,<sup>57</sup> na hufungwa kwa hitimisho linalotamka Utatu Mtakatifu, yaani kwa mwisho mrefu kwa namna hii:

- Ikielekezwa kwa Baba: ***Kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo Mwanao anayeishi na kutawala nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima na milele.***
- Ikielekezwa kwa Baba lakini mwishoni Mwana anatajwa: ***Anayeishi na kutawala nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima na milele.***
- Ikielekezwa kwa Mwana: ***Unayeishi na kutawala na Mungu Baba, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima na milele.***

Watu hujiunga na Sala hiyo kwa mwitikio wa kukubali na kusifia wakisema: ***Amina.***

Katika Misa daima husemwa *Kolekta* moja tu.

## **B) LITURUJIA YA NENO**

**55.** Masomo yaliyochukuliwa kutoka Maandiko Matakatiifu, pamoja na nyimbo zilizopangwa kati ya masomo hayo hufanya sehemu muhimu na ya maana sana ya Liturujia ya Neno. Halafu, homilia, kukiri imani, Sala kwa mahitaji yote au Sala za waamini, huendeleza na kuhitimisha liturujia hiyo. Kwani katika masomo ambayo hufafanuliwa kwa homilia, Mungu husema na watu wake;<sup>58</sup> analifunua fumbo la ukombozi na wokovu, pamoja na kuzilisha roho. Naye Kristo mwenyewe, kwa njia ya Neno lake anakuwa kati ya waamini.<sup>59</sup> Na hilo taifa lake hulifanya hilo Neno la Mungu liwe ni lao kwa njia ya ukimya na nyimbo; halafu wanaambatana nalo kwa njia ya kukiri imani. Na hilo taifa likiisha kulishwa hivi, katika sala za waamini linainua maombi kwa ajili ya mahitaji ya Kanisa lote, na kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu mzima.

### **Ukimya**

**56.** Liturujia ya Neno hupaswa kuadhimishwa hivi kwamba inaalika tafakari. Kwa sababu hiyo, ni lazima kuepa kila aina ya haraka inayozuia kujikusanya rohoni. Basi, vipindi vifupi vya ukimya vinafaa pia katika Liturujia kuendana na kikundi kilichokusanyika. Kwa njia ya vipindi hivyo, kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, Neno la Mungu linapokewa moyoni, na jibu lake linaandaliwa moyoni lipate kutolewa kwa njia ya sala. Vipindi vya ukimya vinaweza kufanyika na kuleta manufaa, k.m. kabla ya kuanza Liturujia yenyewe ya Neno, baada ya somo la kwanza na la pili, na baada ya homilia kutolewa.<sup>60</sup>

### **Masomo ya Biblia**

**57.** Katika masomo, meza ya Neno la Mungu huandaliwa kwa ajili ya waamini, nazo hazina za Biblia hufunguliwa kwao.<sup>61</sup> Ndiyo maana ni vizuri zaidi kufuata mpangilio wa masomo ya Biblia, ambamo umoja wa Maagano yote mawili na wa historia ya wokovu vinadhihirishwa. Wala hairuhusiwi kutumia masomo



mengine yasiyotoka kwenye Biblia, badala ya masomo na zaburi ya kuitikizana ambavyo vimechukuliwa kutoka Neno la Mungu.<sup>62</sup>

**58.** Katika adhimisho la Misa pamoja na watu, masomo daima husomwa kutoka mimbarini.

**59.** Kadiri ya mapokeo, jukumu la kusoma masomo si la ibada ya kiuongozi, bali ni la kihuduma. Kwa hiyo masomo yasomwe na msomaji. Lakini Injili itangazwe na shemasi, au kama hayupo, na kuhani mwingine. Ikiwa shemasi au kuhani mwingine hawapo, basi kuhani kiongozi mwenyewe atasoma Injili. Na kama hakuna msomaji mwingine yeyote anayefaa, kuhani kiongozi asome pia masomo mengine.

Baada ya kila somo, msomaji hutamka mwaliko, ambao watu waliokusanyika wanajibu. Na hivyo wanatoa heshima kwa Neno la Mungu, walilolipokea kwa imani na moyo wa shukrani.

**60.** Somo la Injili ndiyo kilele cha Liturujia ya Neno. Liturujia yenyewe inatufundisha kwamba ni lazima somo la Injili lipewe heshima ya kipekee kuliko masomo mengine. Heshima hiyo hujitokeza kwa upande wa mhudumu aliyepewa jukumu la kuitangaza kupaswa kuomba baraka, au kusali sala ili kujiandaa. Na heshima hiyo hujitokeza vilevile kwa upande wa waamini wanaotambua na kuungama kwa njia ya viitikio vya kupongeza kwamba Kristo yupo hapohapo na kusema nao; nao wanasikiliza somo la Injili hali wamesimama. Mwishowe heshima hiyo inaonekana kwa ishara za heshima zinazotolewa kwa kitabu cha Injili.

## **Zaburi ya Kuitikizana au Wimbo wa Katikati.**

**61.** Baada ya somo la kwanza, inafuata zaburi ya kuitikizana, ambayo ni sehemu halisi ya Liturujia ya Neno, na yenye nafasi muhimu ya kiliturujia na ya kiuchungaji. Ni hivyo kwa sababu inachochea tafakari juu ya Neno la Mungu.

Zaburi ya kuitikizana iendane na somo lenyewe; na inatakiwa kwa kawaida ichukuliwe kutoka Kitabu cha Masomo.

Ni vizuri zaidi zaburi ya kuitikizana ikiimbwa, walau zile sehemu za viitikio vya watu. Kwa hiyo, mzaburi, au mwimba zaburi, anaimba au kusema vifungu vya zaburi akiwa amesimama kwenye mimbari, au mahali pengine panapofaa. Nayo jumuiya yote iliyoketi na kusikiliza, hushiriki kwa njia ya kiitikio kama kawaida, isipokuwa kama zaburi inaimbwa au kusomwa moja kwa moja bila kiitikio. Lakini, ili kusudi watu waweze kuimba kwa urahisi kiitikio cha zaburi, matini fulani fulani za viitikio na zaburi kwa ajili ya vipindi mbalimbali vya mwaka, au kwa ajili ya kawaida mbalimbali za Watakatifu zimechaguliwa. Hizi huweza kutumiwa badala ya matini ile ihusikayo na somo, kila mara zaburi inapoimbwa. Ikiwa zaburi haiwezi kuimbwa, basi isomwe kwa namna inayofaa zaidi ili kuisaidia tafakari ya Neno la Mungu.

Badala ya ile zaburi iliyoandaliwa katika Kitabu cha Masomo, huwezekana kuchukua kwa ajili ya kuimba, au graduale ya kuitikizana kutoka *Graduale* ya Kiroma, au zaburi ya kuitikizana kutoka *Graduale* ndogo, kama inavyoelekezwa katika vitabu hivyo.

## **Shangilio kabla ya Somo la Injili**

**62.** Baada ya somo linalotangulia moja kwa moja Injili, huimbwa ***Aleluya*** au wimbo mwingine kadiri ya *rubrika* kulingana na Kipindi cha kiliturujia. Shangilio la aina hii, kwa lenyewe linayo hadhi ya ibada-kanuni au tendo linalosimama lenyewe, ambalo waamini waliokusanyika wanalitumia wanapompokea na kumsalimu Bwana anayekuja kusema nao kwa njia ya Injili. Tena kwa tendo hilohilo wanaiungama imani yao. ***Aleluya*** huimbwa na wote wakiwa wamesimama, wakiongozwa na kikundi cha waimbaji, au na mwimbaji mmoja. Na kama ikitakiwa, huweza kurudiwa. Lakini aya ya Aleluya huimbwa na kikundi cha waimbaji, au na mwimbaji mmoja.

a) ***Aleluya*** huimbwa kila wakati nje ya Kwaresima. Aya huchukuliwa kutoka Kitabu cha Masomo, au kutoka *Graduale*.

b) Katika kipindi cha Kwaresima, badala ya **Aleluya** huimbwa aya kabla ya Injili, kama ilivyo katika Kitabu cha Masomo. Inawezekana pia kuimba zaburi nyingine, au “*Tractus*” kama inavyopatikana katika *Graduale*.

**63.** Iwapo kabla ya Injili somo ni moja tu:

a) kipindi ambacho **Aleluya** husemwa, inawezekana kutumia zaburi yenye **Aleluya** ndani yake, au zaburi, pamoja na **Aleluya** yenye aya yake;

b) kipindi ambapo **Aleluya** haisemwi, yawezekana kutumia Zaburi na aya kabla ya Injili, au zaburi tu;

c) kama **Aleluya** au aya kabla ya Injili haziimbwi, zaweza kuachwa.

**64. Sekwenzia**, ambayo ni ya hiari, isipokuwa Siku ya Pasaka na Siku ya Pentekoste, huimbwa kabla ya **Aleluya**.

## Homilia

**65.** Homilia ni sehemu ya Liturujia na huhimizwa sana<sup>63</sup> kwa sababu humo mna malisho yanayohitajika kwa maisha ya kikristo. Homilia lazima iwe ni maelezo juu ya dhamira mojawapo ya masomo ya Maandiko Matakatifu, au juu ya matini nyingine kutoka kawaida ya Misa, au kutoka Misa pekee ya siku, kwa kuzingatia fumbo linaloadhimishwa, na mahitaji maalum ya wasikilizaji.<sup>64</sup>

**66.** Kwa kawaida homilia hutolewa na kuhani kiongozi, au na *konselebranti* aliyekabidhiwa na kuhani kiongozi. Hata mara nyingine kuendana na hali ya mazingira hutolewa pia na shemasi, lakini kamwe isitolewe na mlei.<sup>65</sup> Katika hali ya kipekee na kwa sababu muhimu, huweza kutolewa na Askofu au padri anayehudhuria adhimisho, lakini hakuweza kuwa konselebranti.

Siku za Dominika na Sikukuu zilizoamriwa homilia lazima itolewe katika kila Misa inayoadhimishwa pamoja na watu, na haiwezekani iachwe isipokuwa kwa sababu kubwa sana.

Inashauriwa kuwa siku nyingine ni vema homilia itolewe, hasa siku za Majilio na Kwaresima na siku za kipindi cha Pasaka. Huhimizwa kutolewa vilevile sikukuu nyingine au nafasi nyingine watu wanapofika kanisani kwa wingi.<sup>66</sup>

Inafaa kuwa na muda mfupi wa ukimya baada ya homilia.

## **Kuungama Imani**

**67.** Kanuni ya Imani, au “*Symbolum*” yaani Ungamo la Imani linaelekeza hivi: Taifa lote la Mungu lililokusanyika pamoja, waliitikie Neno la Mungu lililotangazwa katika masomo ya Maandiko Matakatifu na kufafanuliwa katika homilia. Tena, watu hao hao wakiisha tamka Kanuni ya Imani kwa kutumia fomula iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya liturujia, huyakumbuka mafumbo makuu ya imani, na kuyaungama, kabla hawajaanza kuyaadhimisha katika Liturujia ya Ekaristi.

**68.** Kanuni ya Imani yapasa kuimbwa au kusemwa na kuhani pamoja na watu siku za Dominika na za sherehe. Inawezekana kuisema pia katika maadhimisho ya kipekee yenye fahari zaidi.

Ikiwa inaimbwa, kuhani ndiye anayeianzisha; au pengine, ikionekana inafaa, inaanzishwa na mwimbaji au na kikundi cha waimbaji. Lakini itaimbwa na waamini wote pamoja, au na watu kwa kuitikizana na kikundi cha waimbaji.

Isipoimbwa, lazima isemwe na wote pamoja, au na makundi mawili kwa kupokezana.

## **Maombi kwa wote**

**69.** Katika maombi kwa wote au Sala ya Waamini, watu wa Mungu huliitikia Neno la Mungu walilolipokea kwa imani; na, kwa kutekeleza wajibu wa ukuhani wao utokanao na Ubatizo, wanamtotea Mungu maombi kwa ajili ya wokovu wa watu wote. Kwa kawaida ni vema maombi ya namna hiyo yafanywe katika Misa pamoja na watu, kwa ajili ya Kanisa takatifu, kwa ajili ya wale wanaotutawala, kwa ajili ya wale wanaosumbuliwa na

shida mbalimbali, na kwa ajili ya watu wote na wokovu wa ulimwengu mzima.<sup>67</sup>

**70.** Kuhusu mfululizo wa nia, kwa kawaida iwe hivi:

- a) kwa ajili ya mahitaji ya Kanisa,
- b) kwa ajili ya viongozi wa serikali na kwa wokovu wa dunia yote,
- c) kwa ajili ya wale wanaoelemewa na shida yoyote ile,
- d) kwa ajili ya jumuiya yenyewe (mahali pale).

Lakini katika adhimisho la kipekee, kama vile Kipaimara, Ndoa, Mazishi, mpango wa nia waweza kupatanishwa zaidi na tukio hilo la kipekee.

**71.** Ni juu ya kuhani kiongoza-ibada kuongoza maombi akiwa amesimama penye kiti chake. Kwa maneno machache, yeye huwaalika waamini kusali; pia huhitimisha maombi kwa sala. Maombi yanayotolewa yawe na kiasi, ya hiari yenye hekima, na yawe yametungwa kwa maneno machache na yenye kueleza sala ya jumuiya nzima.

Inafaa nia zenyewe zitolewe kutoka kwenye mimbari, au mahali pengine panapofaa; na, zitolewe na shemasi au mwimbaji, au msomaji, au na mwamini mlei.<sup>68</sup>

Nao watu wakiwa wamesimama, wanadhihirisha kuwa maombi hayo ni yao, kwa itikio la pamoja baada ya kila ombi kutajwa, au kwa kusali kimya.

## **C) LITURUJIA YA EKARISTI TAKATIFU**

**72.** Katika Karamu ya mwisho, Kristo aliweka sadaka na karamu ya kipasaka. Kutokana na hilo, sadaka ya msalaba inafanywa iwepo siku zote katika Kanisa, kila mara ambapo, kuhani akimwakilisha Kristo Bwana, hufanya kilekile na kwa namna ileile alivyofanya Bwana mwenyewe, na akawakabidhi wanafunzi wake wafanye vile kwa ukumbusho wake.<sup>69</sup>

Kwa maana, Kristo alitwaa mkate na kikombe, akashukuru, akaumega, akawapa wanafunzi wake akisema, "*Twaeni, mle, wote; huu ndio Mwili wangu; hiki ndicho kikombe cha Damu yangu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi*". Tokea hapo, Kanisa limeshikilia na kuratibu adhimisho lote la Liturujia ya Ekaristi katika sehemu zake lilingane na maneno na matendo hayahaya ya Kristo mwenyewe. Kutokana na hayo:

1) Katika maandalizi ya vipaji, mkate na divai pamoja na maji huletwa altareni, yaani vitu vilevile Kristo alivyovipokea mikononi mwake.

2) Katika Sala ya Ekaristi shukrani hutolewa kwa Mungu kwa ajili ya kazi yote ya wokovu; na vipaji vinafanyika Mwili wa Kristo na Damu yake.

3) Kwa kuumega mkate na kwa njia ya Komunyo, waamini, ingawa ni wengi, hupokea Mwili wa Bwana kutoka mkate mmoja, na Damu ya Bwana kutoka kikombe kimoja, kama vile mitume walivyopokea kutoka mikono ya Kristo mwenyewe.

## **Kuandaa Vipaji**

**73.** Mwanzoni mwa Liturujia ya Ekaristi vipaji ambavyo vitageuzwa kuwa Mwili na Damu ya Kristo, vinaletwa altareni.

Kabla ya yote, altare au meza ya Bwana, ambayo ndipo panakutanika Liturujia yote ya Ekaristi,<sup>70</sup> inatayarishwa, na hii inafanyika kwa kuweka juu ya altare hiyo korporale, purifikatorio, Misale na kikombe (kalisi), isipokuwa kama vifaa hivi vilikwisha tayarishwa kwenye meza ya pembeni (au kredensi, "*abacus*").

Kisha vipaji huletwa. Ni vizuri mkate na divai vitolewe na waamini. Hupokelewa na kuhani au shemasi mahali panapofaa, na kuwekwa altareni. Ingawa waamini hawatoi tena mkate na divai inayotumika katika Liturujia kutoka mali zao, kama walivyokuwa wanafanya hapo zamani, hata hivyo ibada-kanuni ya kuvipeleka vipaji hivyo, bado ina nguvu na maana yake ya kiroho.

Hata fedha au vipaji vingine kwa ajili ya maskini au kwa ajili ya Kanisa vinavyoletwa na waamini au vinavyokusanywa Kanisani, huweza kuletwa. Vipaji hivi viwekwe mahali panapofaa nje ya meza ya Ekaristi Takatifu.

**74.** Maandamano ya kupeleka vipaji husindikizwa kwa “wimbo wa matoleo” (*rej. n. 37, b*). Wimbo huo unaendelezwa walau mpaka vipaji vimekwisha wekwa altareni. Sheria za jinsi ya kuimba wimbo huu ni sawa na zile za wimbo wa kuingia (*rej. n. 48*). Daima inawezekana kuwa na wimbo wakati wa ibada-kanuni ya matoleo, hata bila maandamano ya kuleta vipaji.

**75.** Mkate na divai vinatolewa na kuhani juu ya altare, akitumia fomula zilizowekwa rasmi. Kuhani anaweza kuvifukizia vipaji vilivyowekwa juu ya altare; kisha anafukizia msalaba, pamoja na altare yenyewe ili dhabihu ya Kanisa pamoja na sala yake vidhihirishwe kupaa mbele ya uso wa Mungu kama moshi wa ubani. Halafu, kuhani kutokana na huduma yake takatifu, nao watu kutokana na hadhi yao ya wabatizwa, wanaweza kufukiziwa na shemasi au mhudumu mwingine.

**76.** Mwishowe kuhani hunawa mikono kando ya altare. Kwa ibada-kanuni hii, kuhani huonyesha hamu yake ya kutaka utakaso wa ndani.

## **Kuombea Dhabihu**

**77.** Baada ya kuviweka vipaji altareni na kukamilisha ibada-kanuni zinazoandamana navyo, kuhani huwaalika watu wasali pamoja naye, halafu peke yake husema Sala ya Kuombea Dhabihu. Na kwa sala hii matayarisho ya vipaji hukamilika, na Sala ya Ekaristi inaandaliwa.

Katika Misa husemwa Sala moja tu ya Kuombea Dhabihu ambayo inafungwa kwa hitimisho fupi, yaani: ***Kwa njia ya Kristo Bwana wetu***, au ikiwa mwishoni Mwana anatajwa: ***Anayeishi na kutawala daima na milele.***

Watu huitikia ***Amina***, na kwa mwitikio huo hujiunga na sala hiyo, na kuifanya iwe yao.

## Sala ya Ekaristi

**78.** Sasa kiini chenyewe na kilele cha adhimisho lote kinaanza, yaani Sala yenyewe ya Ekaristi, maana yake Sala ya kutoa Shukrani na ya kutakatifuza. Kuhani hualika Taifa la Mungu liinue mioyo kwa Bwana kwa sala na kwa kutoa shukrani; na analiunganisha naye kwa sala kuu. Hii ni sala ambayo kwa jina la jumuiya yote, kuhani huielekeza kwa Mungu Baba, kwa njia ya Yesu Kristo katika Roho Mtakatifu. Sababu na maana ya sala hii ndiyo hii: kusanyiko lote la waamini lijiunge na Kristo katika kuyasifu makuu ya Mungu, na katika kumtolea sadaka. Sala ya Ekaristi hudai na kuwataka wote waisikilize kwa heshima na ukimya.

**79.** Mambo makuu yanayounda Sala ya Ekaristi huweza kufafanuliwa hivi:

a) Tendo la **Shukrani** (linalofanyika hasa katika Utangulizi) ambapo kuhani kwa jina la taifa lote takatifu anamtukuza Mungu Baba na kumshukuru kwa ajili ya kazi yote ya wokovu, au kwa ajili ya kitu cha pekee kutokana na tabia tofauti ya siku, ya sikukuu, au ya kipindi cha mwaka.

b) **Mashangilio** ya shangwe ya kusifia, ambapo jumuiya yote ikijiunga na majeshi ya mbinguni huimba **Mtakatifu**. Mashangilio hayo ni sehemu ya Sala ya Ekaristi, na husemwa na watu wote pamoja na kuhani.

c) **Epiklesi** (Maombi ya kipeke yake) ambapo kwa maombi ya pekee Kanisa husihi nguvu za Roho Mtakatifu ili vipaji vilivyotolewa na watu viwekwe wakfu, yaani vigeuzwe kuwa Mwili na Damu ya Kristo. Tena linaomba ili kafara isiyo na doa, na ya kuliwa katika Komunyo iwalettee wokovu wale wanaoishiriki.

d) **Simulio juu ya kuwekwa Ekaristi na konsekrasio:** Sadaka hufanyika kwa maneno na matendo yake Kristo. Hii ni sadaka ambayo Kristo mwenyewe alianzisha katika Karamu ya Mwisho, alipotolea Mwili wake na Damu yake katika maumbo ya mkate



na divai, akawapa Mitume ili wale na wanywe, na akawaachia agizo la kudumisha fumbo hili.

e) **Anamnesi** (Ukumbusho): ambamo Kanisa, kwa kutimiza agizo ambalo alipewa na Kristo Bwana kwa njia ya Mitume, humkumbuka Kristo mwenyewe kwa kutaja hasa Mateso yake matakatifu, kufufuka kwake kwa utukufu, na kupaa kwake mbinguni.

f) **Kutolea**: ambamo katika ukumbusho huohuo, Kanisa hilihili lililokusanyika hasa hapahapa, na wakati huu sawia, linamtolea Baba, katika Roho Mtakatifu, sadaka hii iliyo safi. Lakini linanua pia kwamba, waamini, siyo tu watoe sadaka safi, bali na wao wajifunze kujitoa wenyewe,<sup>71</sup> na watimilizwe siku kwa siku kwa njia ya Kristo mshenga, katika umoja na Mungu na umoja kati yao, ili Mungu awe yote katika yote.<sup>72</sup>

g) **Maombezi**: Kwa njia ya maombezi huelezwa kuwa Ekaristi Takatifu huadhimishwa katika umoja wa Kanisa lote, yaani la duniani na la mbinguni; na matoleo hufanyika kwa ajili yake na kwa ajili ya viungo vyake vyote, yaani walio hai na marehemu, ambao wameitwa kushiriki ukombozi na wokovu uliopatikana kwa njia ya Mwili na Damu ya Kristo.

h) **Masifu (Doksolojia) ya Mwisho**: hii ni kutaja kutukuzwa kwake Mungu, ambako huthibitishwa na huhitimishwa na mashangilio ya watu wanaoitikia: ***Amina***.

## **Ibada-Kanuni ya Komunyo**

**80.** Kwa vile adhimisho la Ekaristi ni karamu ya kipasaka, ni vema sana, kulingana na agizo la Bwana mwenyewe, Mwili na Damu yake vipokelewe na waamini walio katika hali ya kufaa kama chakula cha roho. Hii ndiyo maana ya kuumega mkate na ibada-kanuni nyingine za maandalizi zinazowaandaa waamini moja kwa moja wapate kukomunika.

## Sala ya Bwana

**81.** Katika Sala ya Bwana, tunaomba tupate mkate wa kila siku, ambao kwa Wakristo huashiria hasa mkate wa Ekaristi. Vilevile tunaomba tusafishwe dhambi ili yaliyo matakatifu yapate kutolewa kweli kwa walio watakatifu. Kuhani anawaalika waamini wasali, na waamini wote husema sala pamoja na kuhani. Lakini kuhani peke yake anaongeza *Embolismo* (Nyongeza), na watu huihitimisha kwa doksolojia. Embolismo, kwa kupanua lile ombi la mwisho la Sala yenyewe ya Bwana, inaomba jumuiya yote ya waamini iwekwe huru kutoka nguvu za maovu yote.

Mwaliko, Sala yenyewe, *Embolismo na Doksolojia* ambayo kwa yenyewe watu huhitimisha haya, vinaimbwa au vinasemwa kwa sauti wazi.

## Ibada-Kanuni ya Kupeana Amani

**82.** Baada ya hayo, inafuata ibada-kanuni ya kupeana amani ambamo Kanisa huomba amani na umoja kwa ajili yake na kwa ajili ya familia nzima ya wanadamu. Tena waamini wanathibitishiana ushirika wa kikanisa na mapendano, kabla ya kuishiriki Sakramenti ya Ekaristi.

Kuhusu ishara yenyewe ya kutakiana amani, namna yake ipangwe na Mabaraza ya Maaskofu, yakizingatia tabia na desturi za mataifa. Lakini inafaa kila mmoja atoe ishara ya amani kwa heshima kwa wale tu walio karibu naye zaidi, pale alipo.

## Kuumega Mkate

**83.** Kuhani huumega mkate, akisaidiwa kama ikitakiwa, na shemasi au *konselebranti*. Kitendo cha kuumega mkate kilichofanywa na Kristo katika karamu ya mwisho, ndicho kilifanya tendo lote la Ekaristi liitwe kwa jina hilo nyakati la Mitume. Tendo hilo la kuumega mkate, huonyesha jinsi waamini, ambao ni wengi wanavyofanywa mwili mmoja (*1Kor 10:17*) kwa kushiriki mkate huo mmoja wa uzima ambao ndiye

Kristo aliyekufa na kufufuka kwa ajili ya wokovu wa dunia. Kuumega mkate kunaanzishwa baada ya kupeana ishara ya amani, na kumalizwa kwa heshima inayopasa pasipo kurefushwa bila sababu; wala kusipewe uzito kuliko inavyostahili. Ibada-kanuni hii hufanywa na kuhani na shemasi tu.

Kuhani huumega mkate na kutia kipande cha hostia katika kikombe ili kuonyesha umoja wa Mwili na Damu ya Bwana katika kazi ya wokovu, yaani umoja wa Mwili wa Yesu Kristo aliye hai na mtukufu. Sala ya kusihi **Mwana Kondoo wa Mungu** kwa kawaida huimbwa na kikundi cha waimbaji au na mwimbaji mmoja, na watu wakiitikia, au inasemwa tu kwa sauti ya kusikika wazi. Sala hiyo hulisindikiza tendo la kumega mkate, hivyo kwamba inaweza kurudiwa tena na tena mpaka ibada-kanuni ya kumega mkate imemalizika. Mwana kondoo ya mwisho inahitimishwa kwa maneno **utujalie amani**.

## **Ibada-kanuni ya Komunyo**

**84.** Kuhani hujitayarisha kwa sala ya faragha ili apokee Mwili wa Kristo na Damu yake kwa mafaafaa ya kiroho. Waamini nao hufanya vivyo hivyo kwa kusali kimya.

Halafu kuhani anawaonyesha waamini mkate wa Ekaristi juu ya patena, au juu ya kikombe na kuwaalika kwenye karamu ya Kristo. Papo hapo, akiungana na waamini, hukiri hali ya unyenyekevu akitumia maneno ya kiinjili.

**85.** Ni jambo la kutamaniwa sana kwamba waamini, kama vile kuhani mwenyewe anavyotakiwa afanye, wapokee Mwili wa Bwana kutoka hostia zilizogezwa katika Misa hiyohiyo; na vivyo hivyo washiriki kikombe, katika yale matukio yaliyopangiwa kikombe (*rej. n. 283*). Kwa namna hiyo, hujitokeza vizuri zaidi, hata kwa njia ya ishara zenyewe, kuwa Komunyo ni kushiriki sadaka hiyo inayoadhimishwa hapohapo.<sup>73</sup>

**86.** Wakati kuhani anapokea Ekaristi Takatifu, wimbo wa Komunyo huanzishwa. Kusudi lake ni kuonyesha umoja wa kiroho wa wale wanaopokea, kwa njia ya umoja wa sauti; kutoa ushuhuda wa furaha iliyo moyoni, na kuweka wazi zaidi hulka ya “kijumuiya” iliyoko katika maandamano ya kwenda kupokea Ekaristi Takatifu. Nyimbo zinaendelea huimbwa muda wote waamini wanapopokea Ekaristi Takatifu.<sup>74</sup> Lakini pakiwa na utenzi wa kuimbwa baada ya Komunyo, wimbo wa Komunyo uachwe mapema.

Pia kuwe na utaratibu ili waimbaji nao wapate nafasi ya kukomunika.

**87.** Kwa ajili ya wimbo wa Komunyo, kuna uwezekano wa kutumia *antifona* kutoka *Graduale* ya Kirumi, iwe ni pamoja na zaburi au bila zaburi, au *antifona* pamoja na zaburi kutoka *Graduale Ndogo*; wimbo mwingine unaofaa na umekubaliwa na Baraza la Maaskofu. Wimbo huu huimbwa na kikundi cha waimbaji peke yao, au na kikundi cha waimbaji pamoja na watu; au na mwimbaji mmoja pamoja na watu.

Lakini kama hakuna kuimba, *antifona* iliyoandikwa katika Misale husemwa na waamini wote, au na baadhi ya waamini, au na msomaji; au kama hakuna mwingine, inasemwa na kuhani mwenyewe baada ya kukomunika yeye mwenyewe, kabla ya kugawa Komunyo kwa waamini.

**88.** Kugawa Komunyo kukimalizika, kuhani na waamini husali kwa kimya moyoni kwa muda fulani. Ikionekana inafaa, kusanyiko lote pia linaweza kuimba kwa pamoja zaburi au wimbo mwingine wa masifu, au utenzi.

**89.** Kwa kutimiliza sala ya Taifa la Mungu na pia kuhitimisha Ibada-kanuni yote ya Komunyo, kuhani husali Sala baada ya Komunyo. Kwa sala hii kuhani humsihi Mungu awajalie matunda ya fumbo lililoadhimishwa.

Katika Misa husemwa Sala moja tu baada ya Komunyo. Sala hii huhitimishwa kwa hitimisho fupi kwa namna hii:

- ikiwa inaelekezwa kwa Baba: ***Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.***
- Ikiwa inaelekezwa kwa Baba, lakini mwishoni Mwana anatajwa: ***Anayeishi na kutawala daima na milele.***
- Ikiwa inaelekezwa kwa Mwana: ***Unayeishi na kutawala daima na milele.***

Kwa kujibu kwa shangilio ***Amina***, watu huikubali sala hiyo na kuifanya iwe yao.

## **D) IBADA-KANUNI YA KUMALIZIA MISA**

**90.** Ifuatayo ndiyo Ibada-Kanuni ya kumaliza Misa:

- a) Matangazo mafupi, kama ni ya lazima;
- b) Salamu au maamkio ya kuagana na Baraka ya kuhani. Baraka hii katika siku fulani fulani na matukio fulani fulani huweza kuongezewa Sala juu ya watu, au fomula yenye sherehe;
- c) Kuwaaga watu kunakofanywa na shemasi au kuhani, ili kila mmoja arudi kwenye kazi yake njema, akimsifu na kumtukuza Mungu;
- d) Kuibusu altare, kunakofanywa na kuhani, na pia shemasi. Na mwisho kuinama sana mbele ya altare kunakofanywa na kuhani, shemasi na wahudumu wengine.

## Sura ya Tatu

### KAZI NA HUDUMA KATIKA MISA

**91.** Adhimisho la Ekaristi ni tendo la Kristo pamoja na Kanisa, yaani taifa takatifu lililounganishwa pamoja na kusimamiwa na Askofu. Kwa sababu hiyo, tendo hilo linahusu Mwili wote wa Kanisa; tena linaudhihirisha na kuujenga mwili huo. Aidha, kila mmoja wa wanakanisa anahusika kwa namna moja au nyingine, kadiri ya utofauti wa daraja, wa wajibu, na wa kushiriki kiutendaji.<sup>75</sup> Kwa namna hii, watu wakristo, ambao “ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu,” wanadhihirisha mpangilio wao unaoshikamana na wa *kihierarkia*.<sup>76</sup> Kwa hiyo, wanakanisa wote, iwe ni wahudumu waliopewa Daraja takatifu, au waamini wakristo walei, wafanye yote na yale tu yanayowahusu katika kutimiza majukumu au utumishi wao.<sup>77</sup>

#### I. KAZI ZA WENYE DARAJA TAKATIFU

**92.** Kila adhimisho halali la Ekaristi huongozwa na Askofu, kwa nafsi yake yeye mwenyewe au kwa njia ya mapadri ambao ni wasaidizi wake.<sup>78</sup>

Askofu akiwepo katika Misa, na hapo waamini wamehudhuria, inafaa sana yeye mwenyewe aadhimishe hiyo Ekaristi na kuwashirikisha mapadri kama wakonselebranti katika tendo hilo takatifu. Hii inafanyika si kwa ajili ya kuongeza fahari ya nje ya ibada-kanuni, bali kwa ajili ya kuonyesha kwa uwazi zaidi fumbo la Kanisa, yaani Kanisa kama “Sakramenti ya umoja”.<sup>79</sup>

Lakini kama Askofu haadhimishi Ekaristi Takatifu, naye humteua mwingine kufanya adhimisho hilo, basi inafaa yeye mwenyewe - akiwa amevaa msalaba wa kifuni, *stola* na *pluviale* juu ya *alba* – asimamie Liturujia ya Neno, na atoe baraka mwisho wa Misa.<sup>80</sup>

**93.** Hali kadhalika, padri ambaye katika Kanisa hupewa uwezo wa Daraja takatifu wa kutolea sadaka katika nafsi ya Kristo,<sup>81</sup>

husimamia watu waamini waliokusanyika mahali na saa palipoamuliwa sawia; huongoza sala yao; huwatangazia ujumbe wa wokovu na hujiunga na watu katika kumtolea Mungu Baba sadaka kwa njia ya Kristo katika Roho Mtakatifu. Na tena huwapa ndugu zake mkate wa uzima wa milele, akishiriki naye mkate huo pamoja nao. Kwa hiyo anapoadhimisha Ekaristi, hana budi kumtumikia Mungu na watu kwa heshima na unyenyekevu. Na, kwa namna anavyotenda na anavyotamka Neno la Mungu, awasadikishie waamini uwepo hai wa Kristo.

**94.** Baada ya padri, shemasi, kutokana na uwezo wa Daraja takatifu aliyopewa, hushika nafasi ya kwanza kati ya wale wanaohudumia katika adhimisho la Ekaristi. Kwa maana Ushemasi mtakatifu umepata heshima kubwa katika Kanisa tangu zamani za Mitume.<sup>82</sup> Katika Misa Shemasi anazo sehemu zake za kipekee zifuatazo: kutangaza Injili, na pengine kuhubiri Neno la Mungu; kuwaongoza waamini katika sala ya maombi kwa watu wote; kumhudumia kuhani; kuandaa altare na kutumikia katika adhimisho la sadaka; kuwagawia waamini Ekaristi; hasa katika umbo la divai; na kuelekeza waamini kuhusu ishara na hali za mwili.

## **II. MAJUKUMU YA TAIFA LA MUNGU**

**95.** Katika adhimisho la Misa, waamini hufanywa wawe taifa takatifu, taifa lililokombolewa, na ukuhani wa kifalme, ili wapate kumshukuru Mungu na kumtolea sadaka isiyo na doa, siyo tu kwa mikono ya kuhani, bali pia wao wenyewe pamoja na kuhani, na wajifunze kujitoa wenyewe kuwa sadaka.<sup>83</sup> Tena inawapasa wawe na jitihada ya kuonyesha hali hiyo kwa maisha mazito ya ndani ya kiroho, na kwa mapendo kwa ndugu wanaoshiriki pamoja nao katika adhimisho hilo.

Kwa sababu hiyo, waepe aina zote za ubinafsi au utengano, wakitambua kwamba wanaye Baba mmoja tu mbinguni, na hivyo wao wote ni ndugu.

**96.** Basi wanaunda mwili mmoja kwa kusikiliza Neno la Mungu, kwa kushiriki katika sala na nyimbo, hasa kwa kutolea pamoja sadaka, na kwa kushiriki pamoja katika meza ya Bwana. Umoja huu huonekana vizuri katika ishara na hali za mwili ambazo waamini huzishika na kuzitekeleza pamoja.

**97.** Na tena, waamini wasikatae kuhudumia taifa la Mungu kwa furaha, kila mara wanapombwa kutimiza huduma fulani na jukumu fulani la pekee katika adhimisho.

### **III. HUDUMA ZA KIPEKEE**

#### **Huduma ya *Akoliti* na *Msomaji* waliowekwa rasmi**

**98. Akoliti** huwekwa rasmi ili kuhudumia altareni na kumsaidia kuhani na shemasi. Wajibu wake wa pekee ni kutayarisha altare na vyombo vitakatifu. Na, ikiwa ni lazima, huwagawia waamini Ekaristi, akichukuliwa kama mhudumu asiye wa kawaida.<sup>84</sup>

Katika kuhudumia altareni, *akoliti* anazo kazi zake maalumu (*rej. n. 187-193*) ambazo yeye anatakiwa kuzifanya.

**99. Msomaji** huwekwa kwa ajili ya kusoma masomo ya Maandiko Matakatiifu, isipokuwa Injili. Msomaji huweza pia kutaja nia za maombi kwa wote, na kusoma Zaburi ya kati ya masomo, ikiwa hakuna mwimba zaburi.

Katika adhimisho la Ekaristi, msomaji ana kazi yake maalum (*rej. n. 194-198*) ambayo yeye hupaswa kuitimiza.

#### **Huduma Nyinginezo**

**100.** Ikiwa hakuna *akoliti* aliyewekwa rasmi, wanaweza kuchaguliwa wahudumu walei kwa ajili ya kuhudumia altareni na kumsaidia kuhani na shemasi. Wahudumu hawa huweza kuchukua msalaba, vinara, chetezo, mkate, divai, maji, hata huweza kuteuliwa kugawa Ekaristi kama wahudumu wasio wa kawaida.<sup>85</sup>

**101.** Ikiwa hakuna msomaji aliyewekwa rasmi, walei wengine huweza kuteuliwa ili kusoma masomo ya Maandiko Matakatiifu.



Hawa wawe kweli watu wa kufaa kutimiza huduma hii, wenye uwezo, na wawe wameandaliwa kwa uangalifu, ili waamini, kutokana na kusikia masomo matakatifu, wajenge mioyoni mwao upendo<sup>86</sup> hai wa kufurahia utamu wa Maandiko Matakatifu.

**102.** Ni kazi ya **mzaburi** kusoma zaburi au wimbo mwingine wa kibiblia uliowekwa kati ya masomo. Kusudi aweze kutimiza sawasawa kazi yake, mzaburi lazima awe na ufundi wa kuimba zaburi, na uwezo wa kutamka sawasawa na kusoma vizuri.

**103.** Kikundi cha waimbaji au **kwaya** hutimiza wajibu wake wa kiliturujia kati ya waamini, na ni wajibu wao kuona kwamba sehemu zinazowahusu hufanyika sawasawa kuendana na namna mbalimbali za nyimbo. Ni kazi yao pia kuchochea ushiriki wa waamini katika kuimba.<sup>87</sup> Haya yanayosemwa mintarafu kikundi cha waimbaji, yanawahusu pia wanamuziki wengine, hasa mpiga kinanda, kadiri mazingira yatakavyohitaji.

**104.** Ni vema kuwepo **mwimbaji** au **mwalimu wa kwaya** wa kuongoza na kusimamia uimbaji wa watu. Zaidi ya hayo, ikiwa hakuna kwaya, ni juu ya mwimbaji huyo kupanga nyimbo mbalimbali, ambazo watu watahamasishwa kuzishiriki.<sup>88</sup>

**105.** Hawa wafuatao pia wanatimiza majukumu ya kiliturujia:

a) **Msakristia**, ambaye kazi yake ni kuandaa kwa uangalifu vitabu vya kiliturujia, mavazi, na vitu vingine vinavyotakiwa katika adhimisho la Misa.

b) **Mtoa maelezo**: huyu hutoa kwa kifupi maelezo na maagizo kwa waamini inapotakiwa, ili kuwaandaa kwa adhimisho na kuwasaidia walielewe vizuri zaidi. Maneno ya ushauri wa mtoa maelezo lazima yatayarishwe kwa uangalifu, yawe wazi na yasiyozidi kipimo. Katika kutekeleza kazi hii, mtoa maelezo asimame mahali panapofaa akiwaelekea waamini, lakini si kwenye mimbari.

c) Wale wanaokusanya matoleo kanisani.

d) Wale ambao, mahali pengine, wanawapokea waamini mlangoni mwa Kanisa na kuwaonyesha mahali pao pa kufaa, pamoja na kupanga maandamano ya waamini hao (*wasimamizi*).

**106.** Inafaa, walau katika makanisa ya kikatedrali na makanisa mengine makubwa, pawepo mhudumu mwenye uwezo na ustadi, au msimamizi wa taratibu za ibada ambaye huwajibika kuona kwamba matendo ya ibada yanapangwa vizuri, na kutekelezwa kwa heshima, kwa utaratibu na uchaji, na wahudumu waliowekwa wakfu pia na waamini walei.

**107.** Huduma za kiliturujia ambazo si za kipekee kwa mapadri au mashemasi, na ambazo zimeelezwa hapo juu (*nn. 100-106*), zinaweza kukabidhiwa kwa kutumia baraka ya kiliturujia au kwa uteuzi wa muda, hata kwa walei wanaofaa walioteuliwa na paroko au na msimamizi wa kanisa husika.<sup>89</sup> Kuhusu huduma ya kumtumikia padri altareni, zifuatwe sheria zilizowekwa na Askofu katika jimbo lake.

#### **IV. MGAWO WA MAJUKUMU NA MAANDALIZI YA ADHIMISHO**

**108.** Kuhani mmoja yuleyule hupaswa kutimiza daima huduma yake ya kuwa kiongoza-ibada wa Misa ileile katika sehemu zake zote, isipokuwa zile ambazo ni za kipekee kwa Askofu anapokuwepo katika Misa hiyo (*rej. juu n. 92*).

**109.** Kama wapo watu kadhaa wanaoweza kutimiza huduma ileile moja, hakuna kipingamizi cha kugawana. Huweza kugawana sehemu mbalimbali za kazi ileile, na kila mmoja atimize sehemu yake. Kwa mfano, Shemasi mmoja huweza kuchukua sehemu za kuimbwa, na mwingine afanye kuhudumia altareni. Kama kuna masomo kadhaa, ni vema kuyagawanya miongoni mwa wasomaji, na vivyo hivyo kwa mambo mengine. Ila, haifai kabisa kugawa sehemu iliyo moja katika adhimisho kwa watu kadhaa. Kwa mfano, somo moja lilelile lisomwe na

wasomaji wawili, mmoja baada ya mwingine, isipokuwa Somo la Mateso ya Bwana.

**110.** Ikiwa katika Misa ya pamoja na watu kuna mhudumu mmoja tu, huyo peke yake huweza kutimiliza huduma mbalimbali.

**111.** Ni lazima kuwe na maandalizi makamilifu ya kila adhimisho la kiliturujia kulingana na Misale na vitabu vingine vya kiliturujia, kwa roho ya ushirikiano mzuri na umakini. Haya yafanyike kati ya wote wanaohusika na ibada-kanuni, mambo ya uchungaji na uimbaji, wakiongozwa na msimamizi wa Kanisa husika, pamoja na kuwasikiliza pia waamini katika mambo yale yanayowahusu moja kwa moja. Lakini kuhani anayeongoza adhimisho, daima anayo haki ya kupanga yale yanayomhusu mwenyewe.<sup>90</sup>

## Sura ya Nne

### MITINDO MBALIMBALI YA KUADHIMISHA MISA

**112.** Katika Kanisa mahalia, nafasi ya kwanza – kutokana na umuhimu wake – ipewe Misa inayoongozwa na Askofu, akizungukwa na mapadri wake, mashemasi na wahudumu walei.<sup>91</sup> Katika Misa hiyo, Taifa la Mungu hushiriki kikamilifu kwa vitendo, kwa sababu hapo ndipo Kanisa linajidhihirisha wazi kwa namna ya pekee.

Katika Misa anayoadhimisha Askofu, au katika Misa ambayo yeye anaisimamia pasipo kuadhimisha Ekaristi, zifuatwe Kanuni zilizotolewa katika Mwongozo wa Ibada za Kiaskofu.<sup>92</sup>

**113.** Misa yenye umuhimu mkubwa pia ni ile inayoadhimishwa pamoja na jumuiya fulani, hasa ya parokia, kwa maana huwakilisha Kanisa lote la kiulimwengu, lenye kuonekana wakati huo na mahali hapo sawia. Huu ndiyo ukweli hasa katika adhimisho la pamoja siku ya Dominika.<sup>93</sup>

**114.** Katika Misa zinazoadhimishwa na jumuiya fulanifulani, nafasi ya pekee hutolewa kwa ile “Misa ya Shirikani” (**Misa conventualis**), ambayo ni sehemu ya sala rasmi ya kila siku, au Misa iitwayo “ya jumuiya”. Ingawa Misa hizi hazidai muundo wa pekee wa kuadhimisha, hata hivyo hufaa sana ziwe za muundo wa kuimba, na hasa kwa kushiriki kikamilifu kwa wanashirika wote, wawe ni watawa au makanoni (**canonici**). Hapo pia, kila mmoja atekeleze jukumu lake kadiri ya Daraja au huduma aliyopewa. Inafaa pia mapadri wote, ambao hawapaswi kuadhimisha Misa peke yao kwa ajili ya manufaa ya kichungaji ya waamini, washiriki katika Misa hizo kadiri inavyowezekana. Aidha, mapadri wote walio wanashirika wa Shirika moja na wanalazimika kuadhimisha Misa peke yao kwa ajili ya manufaa ya waamini, wanaweza bado kushiriki Misa ya Shirika au “ya jumuiya” siku hiyohiyo.<sup>94</sup> Kwani, ni jambo bora

zaidi kwa mapadri wanaohudhuria kwenye adhimisho la Ekaristi Takatifu, isipokuwa wanao udhuru kwa sababu kubwa, watekeleze kwa kawaida huduma iliyo ya kipekee ya Daraja yao, na hivyo washiriki kama wakonselebranti, wakiwa wamevaa mavazi ya ibada. Vinginevyo wavae mavazi rasmi ya kikwaya (**choralem**), au *kota* juu ya kanzu.

## I. MISA INAYOADHIMISHWA PAMOJA NA WATU

**115.** Misa ya pamoja na watu ni ile ambayo waamini wanahudhuria inapoadhimishwa. Inafaa adhimisho la namna hiyo, kadiri inavyowezekana, hasa siku za Jumapili (Dominika) na Sikukuu zilizoamriwa, liwe na nyimbo pamoja na idadi ya kufaa ya wahudumu.<sup>95</sup> Lakini huweza kuadhimishwa pia bila kuimba, au hata akiwepo mhudumu mmoja tu.

**116.** Katika adhimisho la Misa, kama shemasi yupo, yeye atimize majukumu yake kama kawaida. Pamoja na kuwepo kuhani kiongozi, inafaa pawepo na *akoliti* anayemsindikiza, msomaji, na mwimbaji. Lakini ibada inayoelezwa hapa chini, huruhusu pia idadi kubwa zaidi ya wahudumu.

### Vifaa vya kuandaliwa

**117.** Altare hutandikwa walau kitambaa kimoja cheupe. Juu yake, au karibu yake pawekwe vinara viwili vyenye mishumaa inayowaka, au vinne, hata sita, hasa kama ni kwa Misa ya Jumapili (Dominika) au Sikukuu iliyoamriwa. Ikiwa Askofu wa Jimbo ndiye anaadhimisha Misa hiyo, kuwekwe kinara cha saba chenye mshumaa unaowaka. Hali kadhalika pawepo Msalaba wenye sanamu ya Yesu msulibiwa juu ya altare, au karibu na altare hiyo. Pengine vinara hivyo na Msalaba huo huweza kuletwa wakati wa maandamano ya kuingia. Kitabu cha Injili (tofauti na kitabu chenye masomo mengine), chaweza kuletwa wakati wa maandamano, na kuwekwa juu ya altare.

**118.** Vitu Vingine vya Kuandaliwa ni:

a) karibu na kiti cha kuhani pawepo Misale, na kama ni lazima, kitabu cha nyimbo;

b) kwenye mimbari pawe na kitabu cha masomo,

c) juu ya meza pembeni pawepo kikombe, *korporale*, *purifikatorio*, *pala*; kama ni lazima *patena* na *siborio*. Vilevile pawepo mkate (hostia) kwa ajili ya komunyo ya kuhani kiongozi, shemasi, wahudumu wengine, na waamini; pawepo viriba vya divai na maji, kama hivi vyote havikuandaliwa viletwe na waamini wakati wa matoleo; chombo cha maji ya kubariki iwapo kutakuwa na kunyunyizia watu; kisahani kwa ajili ya Komunyo ya waamini, pamoja na vifaa vingine vyote vitakiwavyo kwa ajili ya kuosha mikono,

Ni vema kikombe kifunikwe kwa kitambaa (**velum**) ambacho kinaweza kuwa cha rangi ya siku hiyo, au cheupe.

**119.** Huko sakristia, kuendana na aina mbalimbali za maadhimisho, yaandaliwe mavazi ya ibada (*rej. n. 337-341*) kwa ajili ya makuhani (mapadri), mashemasi na wahudumu wengine.

a) kwa ajili ya kuhani: alba, stola na kasula au *planeta*;

b) kwa ajili ya shemasi: alba, stola na dalmatika. Hii huweza kuachwa kama haipo, au kama ibada inafanywa kwa sherehe ndogo;

c) kwa ajili ya wahudumu wengine: alba au mavazi mengine yaliyo halali kisheria.<sup>96</sup> Wote wanaovaa alba watumie mshipi (**cingulum**) na kitambaa cha mabegani (**amictus**), isipokuwa kama kutokana na mtindo wa alba hakihitajiki.

Ikiwa kunafanyika maandamano ya kuingia, vitu vifuatavyo viandaliwe: kitabu cha Injili, katika siku za Dominika; chetezo na kibweta chenye ubani (kama ubani unatumiwa), Msalaba wa maandamano, na vinara vya mishumaa inayowaka.

## A) MISA BILA SHEMASI

### Kanuni ya Mwanzo.

**120.** Waamini wakiisha kusanyika, kuhani na wahudumu wakiwa wamevaa mavazi ya ibada, huenda altareni kwa utaratibu huu:

a) mtumishi akichukua chetezo kinachofuka moshi, kama ubani unatumika;

b) watumishi wanaochukua mishumaa inayowaka, na katikati yao mtumishi mwingine anayechukua Msalaba wenye sanamu ya Kristo Msulubiwa;

c) waakoliti na watumishi wengine;

d) msomaji ambaye huweza kuwa amechukua Kitabu cha Injili kwa kukiinua juu kidogo. Kwenye maandamano kisichukuliwe kitabu cha aina nyingine cha masomo.

e) Anafuata kuhani atakayeadhimisha Misa.

Ikiwa ubani hutumika, kabla ya kuanza maandamano, kuhani anatia ubani katika chetezo na kuubariki bila kusema neno.

**121.** Wimbo wa kuingia huimbwa wakati maandamano yanapofanyika kuelekea altareni (*rej. nn. 47-48*).

**122.** Wanapofika altareni, kuhani na watumishi huiinamia sana altare.

Msalaba wenye sanamu ya Kristo Msulubiwa uliochukuliwa katika maandamano, huweza kusimikwa karibu na altare ili uwe ndio msalaba wa altareni. Msalaba huu lazima uwe ni huo mmoja tu; vinginevyo uwekwe mbali mahali panapofaa. Mishumaa inawekwa juu ya altare, au karibu na altare. Kitabu cha Injili yafaa kiwekwe juu ya altare.

**123.** Kuhani hukwea altareni na huiheshimu kwa kuibusu. Kisha, inapokuwa inatakiwa, anaufukizia msalaba, na altare akiizunguka.

**124.** Kisha kufanya hayo, anaenda kwenye kiti. Wimbo wa kuingia unapomalizika, wote wakiwa wamesimama, kuhani na waamini wanafanya ishara ya msalaba. Kuhani husema: ***Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.*** Waamini huitikia ***Amina.***

Kisha, huwaelekea waamini, hali amefumbua mikono na kuwasalimu waamini waliopo akitumia mojawapo wa fomula zilizopendekezwa. Kuhani mwenyewe, au mhudumu mwingine, kwa maneno machache sana, anaweza kuwaingiza waamini katika Misa ya siku hiyo.

**125.** Hufuata tendo la toba. Baada ya hilo, husemwa au huimbwa ***Bwana Utuhurumie*** kulingana na *rubrika (rej. n. 52).*

**126. Utukufu** husemwa au huimbwa kuendana na ilivyoagizwa katika adhimisho husika (*rej. n.53*).

**127.** Kisha, kuhani akiwa amefumba mikono, huwaalika watu kusali akisema: **Tuombe.** Wote, pamoja na kuhani, husali kimya kwa kitambo kidogo. Halafu, kuhani hali amefumbua mikono, husema ***Kolekta.*** Anapomaliza waamini hujibu kwa uchangamfu: ***Amina.***

## **Liturujia ya Neno**

**128.** ***Kolekta*** ikiisha kusomwa, wote huketi. Kwa maneno machache sana, kuhani huweza kuwaingiza waamini katika liturujia ya neno. Msomaji huenda kwenye mimbari, halafu hutangaza Somo la Kwanza kutoka kwenye kitabu cha Masomo kilichoandaliwa na kuwekwa mahali hapo kabla ya Misa. Wote husikiliza. Mwisho msomaji hutamka kwa sauti ya kuonyesha shangwe: ***Hilo ndilo Neno la Bwana.*** Wote hujibu: ***Tumshukuru Mungu.***

Kisha huweza kukaa kimya kwa kitambo cha kufaa, ili wote waweze kutafakari kwa kifupi hayo waliyosikia.

**129.** Halafu mwimba-zaburi, au msomaji mwenyewe husema beti za Zaburi; na, kwa kawaida, waamini husema kiitikio.



**130.** Kama kuna somo la pili kabla ya Injili, msomaji hulitangaza na wote husikiliza, na mwisho hujibu kwa uchangamfu, kama ilivyoelezwa juu (n.128). Halafu ikionekana inafaa pawe na muda mfupi wa ukimya na tafakari.

**131.** Hatimaye wote husimama na kuimba **Aleluya** au wimbo mwingine unaotakiwa kuendana na kipindi cha Liturujia (rej. nn. 62-64).

**132.** Wakati **Aleluya** au wimbo mwingine unapoimbwa, kuhani hutia ubani katika chetezo, ikiwa unatumika, na kuubariki. Kisha, akifumba mikono na kuinama sana mbele ya altare, husema bila kusikika, **Ee Bwana, unitakase moyo wangu.**

**133.** Ikiwa Kitabu cha Injili kiko juu ya altare, kuhani hukichukua na kwenda nacho kwenye mimbari akiwa ametanguliwa na watumishi ambao wanaweza kuwa wanachukua chetezo na mishumaa. Huchukua kitabu akiwa amekiinua juu kidogo. Wote waliohudhuria huwa wamesimama wakiielekea mimbari ili kuonyesha heshima ya pekee kwa Injili ya Kristo.

**134.** Kwenye mimbari kuhani hufungua kitabu, na, akiwa amefumba mikono, husema **Bwana awe nanyi.** Wote huitika: **Awe pia nawe.** Halafu anasema: **Somo katika Injili ...**Anaposema hivyo kufanya ishara ya Msalaba katika kitabu kwa kidole gumba; na pia juu yake mwenyewe kwenye paji la uso, midomoni, na kifuani. Wengine wote hufanya vivyo hivyo. Waamini wote hushangilia kwa sauti wakisema: **Utukufu kwako, ee Bwana.** Halafu kama ubani unatumika, kuhani hufukizia kitabu (rej. n. 276-277) . Kisha huitangaza Injili na humalizia kwa kutamka mwaliko wa shangwe: **Hilo ndilo Neno la Bwana.** Wote hujibu **Sifa kwako, ee Kristo.** Kuhani hubusu kitabu akisema kwa sauti isiyosikika: **Dhambi zetu ziondolewe kwa Injili hii iliyosomwa.**

**135.** Ikiwa hakuna msomaji, kuhani mwenyewe husoma masomo yote na zaburi akiwa amesimama kwenye mimbari. Kama ubani unatumika, anatia ubani na kuubariki papo hapo.

Halafu anainama sana na kusema: ***Ee Bwana, unitakase moyo wangu.***

**136.** Kisha, kuhani akisimama karibu na kiti chake, au penye mimbari penyewe, au mahali pengine pa kufaa na penye nafasi, hutoa homilia. Homilia ikiisha, panaweza kuwa na muda mfupi wa ukimya na tafakari.

**137.** Kanuni ya Imani huimbwa au husemwa na kuhani pamoja na waamini wote wakiwa wamesimama. Kwenye maneno ***Alifanyika Mwili***, n.k. wote huinama sana. Katika Sherehe ya Kutangazwa Bwana (Machi 25) na ya Kuzaliwa Bwana (Desemba 25) wote hupiga magoti.

**138.** Baada ya kukiri **Kanuni ya Imani**, kuhani, hali amesimama penye kiti chake na amefumba mikono, huwaalika waamini kwa maneno machache, ili kutoa maombi kwa ajili ya wote. Kisha shemasi, au mwimbaji, au msomaji au mtu mwingine hutoa maombi mbele ya waamini kwenye mimbari au mahali pengine panapofaa. Waamini kwa upande wao huitikia kwa kuomba na kusihi. Hatimaye kuhani hufumbua mikono na kuhitimisha maombi kwa sala.

### **Lituruja ya Ekaristi Takatifu**

**139.** Baada ya maombi kwa ajili ya wote kumalizika, wote huketi; na, kama kuna maandamano ya kuleta vipaji, huanza wimbo wa matoleo (*rej. n. 74*).

*Akoliti* au mtumishi mwingine mlei huweka juu ya altare: *korporale, purifikatorio*, kikombe, pala na Misale ya Altare.

**140.** Ni vizuri waamini waonyeshe ushiriki wao katika Misa kwa kutoa mkate na divai kwa ajili ya adhimisho la Ekaristi, au vipaji vingine kwa ajili ya mahitaji ya Kanisa na maskini.

Kuhani hupokea matoleo ya waamini, akisaidiwa na watumishi au mhudumu mwingine. Mkate na divai hutolewa kwa kuhani kiongozi ambaye mwenyewe anaviweka juu ya altare; lakini vipaji vingine huwekwa mahali pengine panapofaa (*rej n. 73*).

141. Kuhani akiwa altareni huchukua patena yenye mkate, na kwa mikono yote miwili, huiinua juu kidogo juu ya altare, na kusema kwa sauti ndogo (isiyosikika mbali) **Utukuzwe, ee Bwana**. Halafu anaweka patena na mkate juu ya korporale.

142. Halafu kuhani, akisimama pembeni mwa altare, hutia divai na maji kidogo kwenye kikombe akisema kwa sauti ndogo: **Kwa maji haya**. Divai na maji huletwa na mhudumu. Kisha hurudi katikati ya altare, hukichukua kikombe kwa mikono yote miwili, hukiinua kidogo juu, akisema kwa sauti ndogo **Utukuzwe, ee Bwana**. Hatimaye hukiweka kikombe juu ya korporale, na ikiwezekana hukifunika kwa *pala*.

Iwapo wimbo wa matoleo hauimbwi wala kinanda hakipigwi, kuhani anaweza kuyatamka maneno ya matoleo kwa sauti ya kusikika. Nao waamini hujibu wakisema: **Atukuzwe Mungu milele**.

143. Baada ya kukiweka kikombe juu ya korporale, kuhani huinama sana na kusema: **Ee Bwana, utupokee sisi tunaokunyenyekaa**.

144. Kisha, kama ubani unatumika, kuhani hutia kwenye chetezo na kuubariki bila kusema neno. Halafu hufukiza vipaji, msalaba na altare. Na hatimaye mhudumu husimama pembeni mwa altare na kumfukiza kuhani. Nao waamini hufukizwa.

145. Baada ya sala **Ee Bwana utupokee sisi tunaokunyenyekaa**, au baada ya kufukizwa, kuhani huenda pembeni mwa altare; kunawa mikono, akisema kwa sauti ndogo: **Ee Bwana, unioshe** wakati mhudumu anammwagia maji mikononi.

146. Kuhani hurudi katikati ya altare. Halafu husimama akiwatazama watu. Huielekeza mikono yake kwa watu, akiipanua na kuifunga, na kuwaalika watu akisema: **Salini ndugu**. Waamini huinuka na kujibu, wakisema: **Bwana aipokee sadaka**. Kisha kuhani hupanua mikono na kutamka Sala juu ya vipaji. Sala inapomalizika waamini wanajibu, wakisema: **Amina**.

147. Halafu kuhani huanza Sala ya Ekaristi. Kulingana rubrika (*taz. n. 365*) huchagua moja ya sala zilizo katika Misale ya Kiroma au zilizokubalika na Kiti Kitakatifu. Kwa hulka yake, Sala ya Ekaristi husemwa tu na kuhani aliye na Daraja takatifu. Waamini huunganika na kuhani kwa njia ya imani na ukimya, isipokuwa kwa ushiriki uliowekwa katika Sala ya Ekaristi, yaani maitikizano ya Utangulizi, **Mtakatifu**, shangilio baada ya mageuzo, na **Amina** inayofunga doksolojia, au mashangilio mengine aliyoidhinishwa na Baraza la Maaskofu na kukubaliwa na Kiti Kitakatifu.

Inafaa kuhani aimbe zile sehemu za Sala ya Ekaristi zilizowekewa muziki (noti).

148. Kuhani huanza Sala ya Ekaristi, akipanua mikono. Anaimba na kusema: **Bwana awe nanyi**. Waamini wanaitika: **Awe pia nawe**. Halafu huku amenyanyua mikono anaendelea kusema: **Inueni mioyo**. Waamini wanasema: **Tumeiinua kwa Bwana**. Halafu kuhani anafumba mikono, akisema: **Tumshukuru Bwana Mungu wetu**. Nao watu wanajibu: **Ni vema na haki**. Kisha kuhani anaendelea na Utangulizi, huku amefumbua mikono, na anaimba au kusema pamoja na wale waliopo kwa sauti ya wazi: **Mtakatifu** (*rej. n. 79b*)

149. Kisha kuhani huendelea na Sala ya Ekaristi kadiri ya maelekezo ya *rubrika* ambazo ziko katika kila Sala ya Ekaristi.

Ikiwa kuhani *selebranti* ni Askofu, katika Maombi, baada ya maneno **Baba Mtakatifu wetu J.**, huendelea na kusema: **na mimi mtumishi wako nisiyestahili**. Lakini kama Askofu huadhimisha nje ya jimbo lake, baada ya maneno **Baba Mtakatifu wetu J.**, huendelea akisema: **na mimi mtumishi wako nisiyestahili, na ndugu yangu J., Askofu wa Kanisa hili la J.**

Askofu wa jimbo, au yeyote ambaye, kwa mujibu wa sheria hulingana naye (kwa cheo), anatakiwa atajwe kwa fomula hii: **pamoja na mtumishi wako Baba Mtakatifu wetu J. na Askofu (au Vikari, Prelati, Prifekti, Abate) wetu J. .**

Maaskofu waandamizi na wasaidizi waweza kutajwa pia katika Sala ya Ekaristi, lakini siyo Maaskofu wengine wanaobahatika kuhudhuria ibada inayohusika. Ikitokea kwamba wengi wanatakiwa watajwe, itumike fomula hii kwa jumla: **Askofu wetu J. pamoja na Maaskofu wasaidizi wake.**

Katika kila Sala ya Ekaristi, fomula hizo zirekebishwe kwa kuzingatia kanuni za sarufi ya lugha.

**150.** Mara tu kabla ya *konsekrasio*, mtumishi huweza kugonga kengele, kama inafaa, kwa ajili ya kutoa ishara kwa waamini. Kadhalika huweza kugonga kengele katika kila onyesho (la hostia na la kikombe) kuendana na desturi ya mahali.

Ikiwa ubani unatumika, mtumishi hufukizia hostia na kikombe wakati vinapoonyeshwa kwa waamini baada ya *konsekrasio* ya kila moja kufanyika.

**151.** Baada ya *konsekrasio*, kuhani akiisha kusema **Tutangaze Fumbo la Imani**, waamini hushangilia kwa shangwe kwa kutumia mojawapo ya fomula zilizowekwa.

Kuhani anapofika mwishoni mwa Sala ya Ekaristi, anatawaa patena yenye hostia pamoja na kikombe, anaviinua vyote na kusema *doksolojia* yeye peke yake **Kwa njia yake**. Anapomaliza, waamini huitikia kwa tamko la shangwe kuu **AMINA**. Kisha kuhani huweka patena na kikombe juu ya korporale.

**152.** Baada ya Sala ya Ekaristi kumalizika, kuhani anafumba mikono na husema maneno ya mwaliko kabla ya Sala ya Bwana. Halafu anafumbua mikono na kusema Sala ya Bwana pamoja na waamini.

**153. Sala ya Bwana** inapomalizika, akiwa amefumbua mikono, kuhani husema peke yake Sala ya *Embolismo* (Sala ya kuongezea): **Ee Bwana tunakuomba utuopoe**. Anapomaliza waamini hushangilia kwa maneno: **Kwa kuwa ufalme ni wako**.

**154.** Baada ya hapo, kuhani, akiwa amefumbua mikono, husema kwa sauti ya wazi sala **Ee Bwana Yesu Kristo uliyewaambia Mitume.** Anapomaliza, akiwa amewaelekea waamini, anawatangazia amani, huku akifumbua na kufumba mikono: **Amani ya Bwana iwe daima nanyi.** Waamini huitika. **Iwe pia nawe.** Kadiri ya nafasi, kuhani huongeza: **Tutakiane amani.** Kuhani huweza kuwapa watumishi ishara ya amani, lakini wawe wamebaki daima patakatifuni, ili kupa mvurugano katika maadhimisho. Afuate utaratibu huohuo, ikiwa kutokana na sababu maalum, angetaka kuwapa waamini wengine wachache ishara hiyo ya amani. Lakini, wengine wote, kulingana na utaratibu ulioidhinishwa na Baraza la Maaskofu, wapeane ishara ya amani, ya ushirika na ya upendo. Wakati wa kupeana amani huweza kusema **Amani ya Bwana iwe daima nawe,** na huitika: **Amina.**

**155.** Kisha kuhani hutwaa hostia na kuiweka juu ya *patena*. Anavunja kipande na kukitia ndani ya kikombe, akisema kwa sauti inayosikika kwake mwenyewe: **Huku kuchanganya.** Wakati huo kwaya ya waimbaji na waamini wengine huwa wanasema au kuimba **Mwana Kondoo wa Mungu** (*rej. n. 83*).

**156.** Hapo kuhani hufumba mikono na kuinama kidogo mbele ya altare na kusema kwa sauti inayosikika kwake mwenyewe Sala ya Komunyo: **Ee Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu mzima,** au **Ee Bwana Yesu Kristo, usikubali.**

**157.** Akisha kusema Sala ya Komunyo, kuhani hupiga goti, halafu anachukua hostia iliyogeuzwa katika Misa hiihii na kuiinua kidogo juu ya *patena* au juu ya kikombe, na kusema akiwaelekea watu: **Tazama Mwana kondoo wa Mungu.** Halafu, akiungana na waamini, huendelea: **Ee Bwana sistahili.**

**158.** Baada ya hayo, kuhani, akiwa amesimama kuiielekea altare, anasema kimyakimya: **Mwili wa Kristo unilinde nipate uzima wa milele,** na hapo, kwa uchaji anapokea Mwili wa Kristo. Kisha anatwaa kikombe na kusema kimyakimya: **Damu**

**ya Kristo inilinde nipate uzima wa milele.** Hivyo kwa uchaji hupokea Damu ya Kristo.

**159.** Wakati kuhani anapokea Ekaristi Takatifu wimbo wa Komunyo unaanzishwa (*rej. n. 86*).

**160.** Halafu kuhani hutwaa *patena* yenye hostia au *siborio* na huenda kukomunisha waamini, ambao kwa kawaida huja kwa maandamano.

Waamini hawaruhusiwi kujitwalia hostia takatifu wenyewe, wala kikombe kitakatifu. Vivyo hivyo hawaruhusiwi kupokezana mikononi. Waamini hupokea Ekaristi wakiwa wamepiga magoti au wamesimama, kulingana na ilivyoagizwa na Baraza la Maaskofu.

Lakini pale wanapopokea wakiwa wamesimama, hupendekezwa kuwa kabla ya kuipokea Ekaristi takatifu, watoe ishara ya kufaa ya heshima, kuendana na maelekezo yaliyotolewa.

**161.** Ikiwa waamini wanakomunishwa kwa umbo la mkate tu, basi kuhani huinua kidogo hostia na kumwonyesha yule anayepokea na kumwambia **Mwili wa Kristo**. Mwenye kukomunika anajibu: **Amina**, na kupokea Sakramenti mdomoni, au pale inaporuhusiwa hata mkononi, anavyochagua mpokeaji. Mwenye kukomunika akiisha kupokea hostia takatifu, lazima aimeze yote mara moja.

Lakini kama Komunyo inatolewa katika maumbo yote mawili, yafuatwe maelekezo yaliyotolewa mahali pengine (*rej. nn. 284-287*).

**162.** Katika kukomunisha, mapadri wengine ambao wamehudhuria ibada hiyo, huweza kumsaidia kuhani kiongozi kukomunisha. Ikiwa wanaokomunika ni wengi sana, na hao mapadri hawapo, kuhani anaweza kuwaita wahudumu wa dharura wamsaidie. Hawa ni waakoliti waliowekwa rasmi, au waamini wengine ambao walipewa rasmi huduma hiyo.<sup>97</sup>

Kukitokea shida maalum kuhani anaweza kwa muda ule wa dharura kuteua waamini wanaostahili.<sup>98</sup>

Wahudumu hao wasijongee altareni kabla ya kuhani kupokea Komunyo. Na, daima hupokea chombo chenye Ekaristi Takatifu kutoka kwa kuhani kiongozi, wakawagawie waamini wenzao Ekaristi Takatifu.

**163.** Baada ya kumaliza kukomunisha, kuhani mwenyewe huinywa mara moja pale altareni divai iliyogeuzwa kama imebaki. Lakini hostia zilizogeuzwa kama zimebaki, huzila papo hapo, au huzipeleka mahali pa kuhifadhia Ekaristi Takatifu.

Kuhani akiisha rudi altareni, hukusanya vipande vya hostia, kama vipo; halafu akiwa amesimama pembeni mwa altare au penye meza pembeni, husafisha *patena* au *siborio* juu ya kikombe. Hali kadhalika hukisafisha kikombe, akisema kwa sauti ndogo ***Ee Bwana, sakramenti tuliypokea kinywani*** na hukipangusa kikombe kwa *purifikatorio*. Ikiwa vyombo vitakatifu vimesafishiwa altareni, mhudumu huvipeleka kwenye meza ya pembeni. Inaruhusiwa kuvifunika vizuri vyombo vinavyopaswa kusafishwa na kuviacha altareni au kwenye meza ya pembeni juu ya *korporale*, hasa kama ni vingi, na kuvisafisha mara tu baada ya Misa, waamini wakiisha ondoka.

**164.** Baada ya hayo kuhani huweza kwenda kwenye kiti chake. Wote huweza kufanya sala ya kimya kwa muda mfupi; au wanaweza kuimba Zaburi au wimbo mwingine wa masifu, au utenzi (*rej. n. 88*).

**165.** Kisha kuhani anasimama penye kiti chake au altareni. Akiwa amewaelekea waamini na mikono imefumbwa, husema: ***Tuombe***. Halafu anafumbua mikono na kusema Sala baada ya Komunyo. Kabla ya kusema sala hiyo, anaweza kukaa kimya kwa muda mfupi, isipokuwa kama alikwisha kufanya hivyo baada ya Komunyo. Mwisho wa sala, watu huitikia kwa shangwe: ***Amina***.



## **Ibada-Kanuni ya Kumalizia**

**166.** Ikiwa kuna matangazo machache kwa ajili ya waamini, haya hufanyika inapomalizika Sala baada ya Komunyo.

**167.** Baada ya matangazo, kuhani, akiwa amefumbua mikono, huwaaga hivi waamini na kusema: ***Bwana awe nanyi.*** Waamini hujibu: ***Awe pia nawe.*** Kuhani anafumba mikono, na mara anaweka mkono wake wa kushoto kifuani, na papo hapo anainua mkono wa kulia na kusema: ***Awabariki Mungu Mwenyezi*** na anafanya Ishara ya Msalaba juu ya waamini akisema: ***Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.*** Wote hujibu: ***Amina.*** Katika siku na nafasi maalumu, baraka hiyo inaweza kukuzwa kwa kutanguliwa na sala juu ya watu, au fomula za fahari zaidi, kadiri *rubrika* zinavyoruhusu.

Askofu hubariki watu kwa fomula inayomhusu Askofu, pamoja na kufanya ishara ya Msalaba juu ya watu mara tatu.<sup>99</sup>

**168.** Kuhani, mara baada ya kutoa baraka, hufumba mikono na kusema: ***Nendeni na Amani.*** Wote huitika: ***Tumshukuru Mungu.***

**169.** Kisha kuhani hutoa heshima kwa altare kwa kuibusu. Halafu anaiinamia sana pamoja na wahudumu wengine. Wote wanaondoka pamoja.

**170.** Endapo baada ya Misa hufuata ibada nyingine ya kiliturujia, ibada ya kumalizia, yaani kubariki, kuaga na kuwaruhusu waamini, huachwa.

## **B) MISA AKIWEPO SHEMASI**

**171.** Shemasi akiwepo kwenye adhimisho la Ekaristi na amevaa mavazi matakatifu, basi atekeleze huduma yake. Wajibu wake hasa ni:

- a) kumsaidia kuhani na kuwa karibu naye,
- b) kwenye altare kuhudumia kikombe na kitabu;

- c) kutangaza Injili, na kama akiagizwa na kuhani *selebranti*, kutoa homilia (*rej. n. 66*);
- d) kutoa maelekezo kwa waamini pale inapotakiwa, na kutaja nia za maombi kwa wote;
- e) kumsaidia kuhani *selebranti* kugawa Komunyo, pamoja na kusafisha na kuviweka sawa vyombo vitakatifu;
- f) pia kujazia huduma ya watumishi wengine kama hawapo.

## **Ibada-Kanuni ya Kuanzia**

**172.** Wanapokwenda altareni shemasi huwa amechukua Kitabu cha Injili, akiwa amekiinua kidogo na kumtangulia kuhani; vinginevyo hutembea kando ya kuhani wanapoandamana.

**173.** Anapofika altareni, anaijongea altare ameshika Kitabu cha Injili, bila kuinama. Hukiweka Kitabu vizuri juu ya altare. Halafu, pamoja na kuhani wanatoa heshima kwa altare kwa kuibusu.

Lakini ikiwa hakuchukua Kitabu cha Injili, huinama sana mbele ya altare, na pamoja na kuhani, anatoa heshima kwa altare kwa kuibusu.

Kisha, endapo ubani hutumika, humsaidia kuhani kutia ubani katika chetezo na kuufukizia msalaba na altare.

**174.** Baada ya kufukizia altare, shemasi huenda kwenye kiti pamoja na kuhani. Hukaa kando ya kuhani na kumhudumia kila inapotakiwa.

## **Liturujia ya Neno**

**175.** Wakati inapoimbwa *Aleluya* au wimbo mwingine, kama chetezo kinatumika, shemasi humsaidia kuhani kutia ubani. Halafu anainama sana mbele ya kuhani na kumwomba baraka kwa kusema kwa sauti ndogo: ***Baba unibariki.***

Kuhani humbariki akisema: ***Bwana awe moyoni mwako.*** Shemasi hufanya ishara ya Msalaba na kuitikia: ***Amina.*** Kisha hukiendea Kitabu cha Injili ambacho kiliwekwa juu ya altare; na, baada ya kuiinamia altare, hukichukua kitabu mpaka mimbarini,

akiwa amekiinua kidogo. Huwa ametanguliwa na mtumishi mwenye chetezo kinachofuka moshi, pamoja na watumishi wengine wanaochukua mishumaa inayowaka. Hapo shemasi huwasalimu waamini akisema, na akiwa amefumba mikono: **Bwana awe nanyi.** Kisha kwenye maneno **Somo katika Injili ilivyoandikwa na ...**, huchora kwa kidole gumba alama ya msalaba juu ya kitabu, na pia juu yake mwenyewe katika paji la uso, mdomoni na kifuani. Halafu hufukizia kitabu na kutangaza Injili. Anapomaliza Injili, husema kwa uchangamfu na shangwe: **Hilo ndilo Neno la Bwana.** Wote huitikia: **Sifa kwako Ee Kristo.** Kisha anatoa heshima kwa kitabu kwa kukibusu pale penye somo lenyewe, akisema kwa sauti ndogo: **Kwa maneno ya Injili.** Kisha hurudi kwa kuhani.

Iwapo shemasi anamhudumia Askofu, hukipeleka kitabu kwake ili akibusu au hukibusu yeye mwenyewe na kusema kwa sauti ndogo: **Kwa maneno ya Injili.** Katika Misa za sherehe kubwa, Askofu akiona inafaa huweza kuwabariki watu kwa Kitabu cha Injili.

Kisha Kitabu cha Injili huweza kuwekwa kwenye meza ya pembeni, au mahali pengine pa kufaa na penye staha.

**176.** Kama hakuna msomaji mwingine anayefaa, shemasi husoma pia masomo mengine.

**177.** Katika Sala za Maombi, baada ya utangulizi wa kuhani, shemasi hutaja nia za maombi ya waamini, kwa kawaida akisimama kwenye mimbari.

## **Lituruja ya Ekaristi Takatifu**

**178.** Baada ya maombi kwa wote, kuhani hubaki ameketi kwenye kiti chake. Wakati huo shemasi huandaa altare kwa matoleo akisaidiwa na mtumishi, kwani kwa kawaida ni wajibu wa shemasi kushughulikia vyombo vitakatifu. Pamoja na kufanya hayo shemasi humsaidia kuhani kupokea vipaji vya waamini. Halafu humpatia kuhani *patena* yenye mkate utakaogeuzwa kuwa Mwili wa Yesu. Kisha humimina divai na

maji kidogo katika kikombe akisema kwa sauti ndogo: ***Kwa fumbo la maji haya*** halafu anampa kuhani hicho kikombe. Lakini inawezekana kufanya matayarisho hayo ya kikombe kwenye meza ya pembeni. Ikiwa ubani unatumika, shemasi humsaidia na kumsindikiza kuhani katika kufukizia vipaji, altare na msalaba. Mwisho, yeye mwenyewe au mtumishi humfukizia kuhani, na baadaye waamini.

**179.** Wakati wa Sala ya Ekaristi, shemasi husimama karibu na kuhani, ila nyuma yake kidogo, ili ikibidi awe tayari kumsaidia kufunua kikombe au Misale.

Lakini, tangu *epiklesi* hadi kuinuliwa kikombe wakati wa *konsekrasio*, shemasi hubaki amepiga magoti. Wakiwepo mashemasi zaidi ya mmoja, mmojawapo huweza kuweka ubani kwenye chetezo wakati wa *konsekrasio* na kufukizia hostia na kikombe vinapoonyeshwa.

**180.** Wakati wa *doksolojia* ya mwisho wa Sala ya Ekaristi, shemasi husimama kando ya kuhani. Yeye huinua kikombe, wakati kuhani huinua *patena* yenye hostia, mpaka waamini wamemaliza kuitikia: ***Amina***.

**181.** Kuhani akiisha sema sala ya amani, na ***Amani ya Bwana iwe daima nanyi***, nao waamini wamekwisha itikia ***Iwe pia nawe***, shemasi huweza kuwaalika waamini watakiane amani. Husema hivyo akiwa amewaelekea waamini, na amefumba mikono: ***Tutakiane amani***. Lakini yeye mwenyewe hupokea amani kutoka kwa kuhani na huweza kuwatakia amani wahudumu wengine waliosimama karibu zaidi naye.

**182.** Kuhani akiisha kukomunika, shemasi naye hupokea Komunyo katika maumbo yote mawili kutoka kwa kuhani. Kisha humsaidia kuhani kuwakomunisha waamini. Iwapo Komunyo inatolewa katika maumbo yote mawili, shemasi anawahudumia wanaokomunika katika kikombe. Akimaliza kukomunisha, kwa heshima anakunywa mara damu yote ya Kristo iliyobaki. Ikiwa lazima, mapadri na mashemasi wengine waliopo wanasaidia.

**183.** Huduma ya kugawa Komunyo ikimalizika, shemasi hurudi altareni pamoja na kuhani. Anakusanya vipande vya hostia, kama vipo, halafu huchukua kikombe na vyombo vingine vitakatifu na kuvipeleka kwenye meza ya pembeni. Hapo huvisafisha na kuviweka vizuri kama itakiwavyo; na wakati huo kuhani hurudi kwenye kiti chake. Lakini inaruhusiwa kuviacha vyombo vinavyopaswa kusafishwa juu ya *korporale* kwenye meza pembeni vikiwa vimefunikwa vizuri na kuvisafisha mara baada ya Misa, waamini wakiisha kuagwa.

### **Ibada-Kanuni ya Kumalizia**

**184.** Baada ya kuhani kusema Sala baada ya Komunyo, shemasi huwatangazia waamini matangazo machache, kama yapo, isipokuwa kama kuhani anataka kuyatangaza yeye mwenyewe.

**185.** Ikiwa inatumika Sala juu ya watu, au fomula nyingine yenye fahari zaidi, shemasi husema: ***Inameni kwa ajili ya baraka.*** Kuhani akiisha kutoa baraka shemasi huwaaga waamini, akiwa amewaelekea na amefumba mikono na kusema: ***Nendeni na amani.***

**186.** Hatimaye, shemasi pamoja na kuhani hutoa heshima kwa altare kwa kuibusu. Kisha huiinamia sana na kuondoka kama walivyoingia.

### **C) KAZI ZA AKOLITI**

**187.** Kazi ambazo akoliti au mtumishi huweza kuzifanya ni za aina mbalimbali. Tena zaweza kutokea wakati mmoja kwa pamoja. Kwa hiyo inafaa kazi hizo zigawanywe vizuri kati ya akoliti kadhaa. Ikiwa kuna *akoliti* mmoja tu, basi atekeleze tu zile zilizo muhimu zaidi, na nyingine zigawanywe kati ya wahudumu wengine.

### **Ibada-kanuni ya mwanzo**

**188.** Katika maandamano ya kwenda altareni *akoliti* huweza kuchukua msalaba kati ya watumishi wawili wenye mishumaa

inayowaka. Anapofika altareni huusimamisha msalaba karibu na altare, ili uwe msalaba wa altareni; vinginevyo huuweka vizuri mahali pa kufaa mbali na altare. Kisha hukaa mahali pake katika patakatifu.

**189.** Kwa muda wote wa adhimisho, ni wajibu wa akoliti kuwaendea kuhani na shemasi kila inapotakiwa, ili awapelekee kitabu na kuwasaidia katika mambo mengine yaliyo ya lazima. Kwa hiyo, kadiri inavyowezekana inafaa akae mahali ambapo huweza kutekeleza huduma yake kwa urahisi, iwe ni kwenye kiti, au altareni.

### **Liturujia ya Ekaristi Takatifu**

**190.** Baada ya maombi kwa wote ikiwa hakuna shemasi, kuhani akiwa bado kwenye kiti chake, *akoliti* aweke *korporale*, *purifikatorio*, kikombe, pala na Misale juu ya altare. Kisha humsaidia kuhani kupokea vipaji vya waamini, kama vipo. Pia, ikiwa inafaa, hupeleka mkate na divai altareni na kumpatia kuhani. Ikiwa ubani unatumika, yeye humpa kuhani chetezo na kumsaidia katika kuvifukizia vipaji, msalaba na altare. Kisha humfukiza kuhani, halafu waamini.

**191.** *Akoliti* aliyewekwa rasmi, kama ni lazima, huweza kumsaidia kuhani kugawa Komunyo, akiwa kama mhudumu asiye wa kawaida.<sup>100</sup> Lakini ikiwa Komunyo inatolewa katika maumbo yote mawili, na hakuna shemasi, *akoliti* ndiye anayesaidia kupokeza kwa kikombe. Au ikiwa kukomunisha kunafanyika kwa mtindo wa kuchovya, *akoliti* ndiye anayeshika kikombe.

**192.** Hali kadhalika, *akoliti* aliyewekwa rasmi, akiisha kugawa Komunyo, humsaidia kuhani au shemasi kuvisafisha na kuviweka vizuri vyombo vitakatifu. Endapo shemasi hayupo, *akoliti* mwenyewe huvipeleka vyombo vitakatifu kwenye meza ya pembeni na kuvisafisha na kuvipanga kama kawaida.

**193.** Adhimisho la Misa likimalizika, *akoliti* na wahudumu wengine, pamoja na kuhani na shemasi, hurudi sakristia kwa

maandamano, kwa utaratibu uleule waliotumia wakati wa kuingia altareni.

## **D) KAZI ZA MSOMAJI**

### **Ibada-Kanuni ya mwanzo**

**194.** Wakati wa maandamano ya kwenda altareni, ikiwa shemasi hayupo, msomaji akiwa amevalia mavazi yanayotakiwa, huweza kuchukua Kitabu cha Injili kwa kukiinua juu kidogo. Huwa amemtangulia kuhani; vinginevyo huandamana na wahudumu wengine.

**195.** Anapofika altareni, huiama sana pamoja na wengine. Ikiwa amechukua Kitabu cha Injili, hukwea altareni na kukiweka kitabu hicho juu ya altare. Kisha huchukua nafasi yake patakatifuni pamoja na wahudumu wengine.

### **Liturujia ya Neno**

**196.** Msomaji huyasoma masomo yanayotangulia Injili, akiwa mimbarini. Na ikiwa mwimba zaburi hayupo, msomaji ndiye anayeongoza zaburi ya kuitikizana ambayo hufuata somo la kwanza.

**197.** Iwapo shemasi hayupo, msomaji kutoka mimbarini huweza kutangaza nia za maombi kwa wote baada ya utangulizi wa kuhani.

**198.** Tena, iwapo nyimbo haziimbwi wakati wa kuingia au wakati wa Komunyo, vilevile kama antifona zilizopendekezwa katika Misale hazisomwi na waamini, msomaji huweza kuzisoma wakati wake (*rej. nn 48, 87*).

## **II. MISA YA KUSHIRIKIANA MAKUHANI WAKONSELEBRANTI**

**199.** Misa ya kushirikiana makuhani wengi (wakonselebranti) ambayo ndiyo inaonyesha barabara umoja wa ukuhani, wa sadaka, na wa taifa lote la Mungu inatakiwa na ibada-kanuni

zenyewe ifanyike: katika Misa ya Daraja ya Uaskofu au Upadri, katika kumbariki Abate, na katika Misa ya Krisma.

Aidha, ni jambo la kusifiwa sana kuwa na Misa ya aina hii katika maadhimisho yafuatayo, isipokuwa kama manufaa ya waamini yanadai vingine, au yanapendekeza vingine:

- a) Misa ya Jioni katika Karamu ya Bwana Alhamisi Kuu.
- b) Misa ya Mtaguso, ya Mikutano Mikuu ya Maaskofu, na ya Sinodi.
- c) Misa ya Shirikani (*Konventuali*); Misa kubwa katika makanisa na vikanisa.
- d) Misa wakati wa mikutano mbalimbali ya mapadri wa jimbo, au wa mashirika.<sup>101</sup>

Hata hivyo, kuhani huweza kuadhimisha Ekaristi peke yake, isipokuwa hawezi kufanya hivyo wakati uleule na kwenye kanisa au kikanisa kilekile wakati inapoadhimishwa Misa ya *konselebrasio*. Lakini padri peke yake haruhusiwi kutolea sadaka ya Misa siku ya Alhamisi Kuu katika Karamu ya Bwana, wala katika Mkeshwa wa Pasaka.

**200.** Mapadri wageni wakaribishwe kwa furaha kwenye *konselebrasio* ya Ekaristi, mradi wamejitambulisha kuwa wanayo hadhi ya ukuhani.

**201.** Mahali penye makuhani wengi, *konselebrasio* inaweza kufanyika hata mara nyingi katika siku ileile, ikiwa kuna ulazima au umuhimu wa kichungaji wa kufanya hivyo; lakini ni lazima ifanyike nyakati tofauti, au katika mahali patakatifu mbalimbali.<sup>102</sup>

**202.** Kwa mujibu wa sheria, ni juu ya Askofu kupanga utaratibu wa *konselebrasio* katika makanisa yote na vikanisa vyote katika jimbo lake.

**203.** *Konselebrasio* ambayo mapadri wa jimbo fulani wanaadhimisha na Askofu wao, ina heshima ya kipekee. Hii huweza kufanyika katika Misa za Kituo (*stationalis*) ambazo ni



hasa Sherehe Kubwa za Mwaka wa Liturujia, Misa ya Daraja ya Askofu mpya wa jimbo, au ya Mwandamizi au ya Msaidizi; Misa ya Kubariki Mafuta ya Krisma; Misa ya Jioni katika Karamu ya Bwana. Huweza kufanyika pia katika Misa za Watakatifu Waasisi wa Kanisa mahalia, au Wasimamizi wa Jimbo; katika Tarehe za Kumbukumbu za Askofu, na mwisho, kwenye Sinodi au Ziara ya Kichungaji.

Kwa sababu hiyohiyo, *konselebrasio* inahimizwa kila mara mapadri wanapokusanyika na Askofu wao, kwa mfano, wakati wa mazoezi ya roho au wa mikutano fulani. Katika nafasi hizo ile ishara ya umoja wa ukuhani, na vilevile umoja wa Kanisa ambalo ndiyo kiini kabisa cha kila *konselebrasio*, unajitokeza kwa namna iliyo dhahiri kabisa.<sup>103</sup>

**204.** Kwa sababu ya mahitaji ya pekee, kama vile umaarufu wa ibada, au wa sikukuu, inaruhusiwa kuadhimisha Misa isiyo ya kushirikiana katika *konselebrasio* siku hiyohiyo, hata zaidi ya mara moja katika nafasi zifuatazo:

a) kuhani aliyeadhimisha Misa isiyo ya *konselebrasio* siku ya Alhamisi ya Juma Takatifu, au akishiriki Misa ya Kubariki Mafuta Matakatifu, huweza pia kuadhimisha Misa ya Jioni katika Karamu ya Bwana pasipo *konselebrasio*, au kwa kushiriki katika *konselebrasio*;

b) kuhani aliyeadhimisha Misa ya Kesha la Pasaka kwa kushiriki *konselebrasio*, au bila *konselebrasio*, huweza bado kuadhimisha katika siku ya Pasaka bila *konselebrasio* au katika *konselebrasio*;

c) katika Sherehe ya Kuzaliwa Bwana, makuhani wote huweza kuadhimisha Misa tatu bila *konselebrasio* au katika *konselebrasio*, ili mradi wazingatie vipindi maalum vilivyopangwa;

d) katika siku ya Kuwakumbuka Waamini Marehemu wote makuhani wote wanaweza kuadhimisha Misa tatu wakiwa mmoja mmoja au kwa *konselebrasio* ikiwa maadhimisho

yanafanyika nyakati tofauti kulingana na maagizo yaliyowekwa kuhusu kutimiza lengo la Misa ya pili na ya tatu;<sup>104</sup>

e) kuhani anayeshiriki Misa ya *konselebrasio* katika Sinodi, ziara ya kichungaji pamoja na Askofu au wakili wake, au katika mikutano mbalimbali ya mapadri, anaweza kuadhimisha tena Misa kwa manufaa ya waamini. Uwezekano huo upo pia, kwa kuzingatia mazingira, kuhusu mikutano ya watawa.

**205.** Misa ya *konselebrasio* kwa mtindo wowote ule, huratibishwa kulingana na kanuni za kawaida za Misa (*rej. nn. 112-198*), yakizingatiwa au kubadilishwa haya yanayoelezwa hapa chini.

**206.** Padri yeyote yule haruhusiwi kujiunga na Misa ya *konselebrasio* ambayo imekwisha anza.

**207.** Kwenye patakatifu (madhabahuni) viandaliwe vifaa vifuatavyo:

a) Viti na vijitabu vya makuhani wakonselebranti;

b) Kwenye meza ya pembeni pawe na kikombe kikubwa cha kutosha, au vikombe kadhaa vya kutosha.

**208.** Ikiwa hakuna shemasi katika Misa ya *konselebrasio*, kazi zake maalumu zitekelezwe na baadhi ya makuhani wakonselebranti.

Na kama hata watumishi wengine hawapo zile huduma zao zaweza kukabidhiwa waamini wengine wanaofaa; vinginevyo zifanywe na baadhi ya makuhani *wakonselebranti*.

**209.** Huko sakristia, au mahali pengine panapofaa makuhani *wakonselebranti* huvaa mavazi ya Misa kama wanapoadhimisha kila mmoja peke yake. Ikitokea shida kubwa, kwa mfano idadi kubwa ya *wakonselebranti* na upungufu wa mavazi ya kiliturujia, *wakonselebranti* wanaweza kuacha kuvaa kasula au *planeta*, wakavaa stola juu ya alba; lakini *selebranti kiongozi* lazima daima avae kasula.

## **Ibada-Kanuni ya mwanzo**

**210.** Mambo yote yakiisha andaliwa kama inavyotakiwa, maandamano hufanyika kama kawaida, kupitia kanisani kwenda altareni. *Wakonselebranti* humtangulia *selebranti kiongozi*.

**211.** Wafikapo altareni, *selebranti* kiongozi na *wakonselebranti* huinama sana; hutoa heshima kwa altare kwa kuibusu; halafu huenda kwenye viti walivyoandaliwa. Lakini yeye *selebranti* kiongozi hufukizia ubani msalaba na altare kama inapotakiwa, halafu huenda kwenye kiti chake.

## **Lituruja ya Neno**

**212.** Wakati wa Lituruja ya Neno, makuhani *wakonselebranti* hukaa kwenye nafasi zao, na huketi au husimama jinsi anavyofanya *selebranti kiongozi*.

Wimbo wa ***Aleluya*** ukishaanza wote husimama isipokuwa Askofu, kama anaadhimisha. Huyu akiwa anaadhimisha, hutia ubani katika chetezo bila kusema neno na kumbariki shemasi (au padri *konselebranti* kama shemasi hayupo) atakayetangaza Injili. Lakini ikiwa Misa ya *konselebrasio* inaongozwa na padri, kuhani *konselebranti* anayeenda kutangaza Injili, haombi wala hapokei baraka kutoka kwa *selebranti kiongozi*.

**213.** Kwa kawaida homilia hutolewa na *selebranti kiongozi*, au mmojawapo wa *wakonselebranti*.

## **Lituruja ya Ekaristi Takatifu**

**214.** Maandalizi ya vipaji (*rej. nn. 139-146*) hufanywa na kuhani kiongozi; *wakonselebranti* huendelea kukaa mahali pao.

**215.** *Selebranti kiongozi* akiisha kusema Sala ya Kuombea Dhabihu, *wakonselebranti* hujongea altareni, na kusimama wakiizunguka altare, kwa namna ambayo hawazuii matendo yanayofanyika altareni kuonekana vizuri kwa waamini, wala hawamzuii shemasi kuijungelea altare anapohitajiwa kutimiza huduma yake.

Shemasi anatakiwa kutimiza huduma yake karibu na altare kuhusiana na kikombe na Misale. Lakini kadiri inavyowezekana, asimame mbali kidogo na altare, nyuma ya wakonselebranti wanaomzunguka selebranti kiongozi.

## **Namna ya kusema Sala ya Ekaristi**

**216.** *Prefasio* husemwa au huimbwa na *selebranti kiongozi* peke yake; lakini ***Mtakatifu*** husemwa au huimbwa na *wakonselebranti* wote pamoja na waamini na kikundi cha waimbaji.

**217.** ***Mtakatifu*** ikimalizika, wakonselebranti huendelea na Sala ya Ekaristi jinsi ilivyoelezwa hapo chini. Selebranti kiongozi peke yake hufanya ishara za kimatendo isipokuwa kama imeelekezwa vingine.

**218.** Sehemu ambazo husemwa na *wakonselebranti* wote kwa pamoja, na hasa maneno ya *konsekrasio*, ambayo wote hutakiwa kuyatamka, husemwa kwa namna ambayo, *wakonselebranti* hutamka kwa sauti ndogo hivyo kwamba sauti ya *selebranti kiongozi* inaweza kusikika wazi. Kwa jinsi hiyo, maneno haya huweza kusikiwa na waamini kwa urahisi zaidi.

Sehemu zile ambazo zinatakiwa kusemwa na wakonselebranti wote kwa pamoja, na zimetwiwa noti za muziki katika Misale, hufaa sana ziimbwe.

## **Sala ya Ekaristi I, au Kanuni ya Kiroma**

**219.** Katika Sala ya Ekaristi I, au Kanuni ya Kiroma, ***Ee Baba Mwema*** husemwa na *selebranti kiongozi* peke yake, hali amefumbua mikono.

**220.** Kuwakumbuka wazima ***Ee Bwana uwakumbuke***, na ***Tunashirikiana*** huweza kusemwa na *konselebranti* mmoja mmoja kati ya *wakonselebranti*. Kila mmoja husema peke yake kwa sauti ya kusikika, hali amefumbua mikono.

**221.** ***Kwa hiyo, ee Bwana***, husemwa na *selebranti kiongozi* peke yake, hali amefumbua mikono.

**222.** Toka *Ee Mungu tunakuomba*, hadi *Ee Mungu Mwenyezi tunakuomba kwa unyenyekevu selebranti kiongozi* peke yake ndiye anayetokeleza vitendo, lakini *wakonselebranti* wote husali pamoja naye, kwa sauti kwa utaratibu huu:

- a) *Ee Mungu tunakuomba*: wananyosha mikono juu ya vipaji;
- b) *Siku iliyotangulia*, na *Vivyo hivyo*, huwa wamefumba mikono;
- c) Husema maneno ya Bwana wakiwa wamenyosha mkono wa kuume juu ya mkate na juu ya kikombe, iwapo huonekana inafaa. Lakini hostia na kikombe vinapoonyeshwa, huihua macho kuvitazama, na hatimaye huihama sana.
- d) *Kwa hiyo ee Bwana*, na *Uwe radhi* wanafumbua mikono.
- e) *Ee Mungu Mwenyezi tunakuomba kwa unyenyekevu*, huihama wamefumba mikono mpaka penye maneno *Nasi tutakaopokea*. Hapo huihuka na kufanya ishara ya msalaba penye maneno: *tujazwe kila baraka na neema ya mbinguni*.

**223.** Kuwakumbuka marehemu *Ee Bwana uwakumbuke pia*, na, *Nasi pia wakosefu*, visemwe na konselebranti mmoja mmoja kila mmoja peke yake, tena aziseme sala hizo kwa sauti ya kusikika, akiwa amefumbua mikono.

**224.** Penye maneno *Nasi pia wakosefu*, *wakonselebranti* wote hujipiga kifua.

**225.** *Ee Bwana, kwa njia ya Kristo unaumba daima mema yote* husemwa na *selebranti kiongozi* peke yake.

## **Sala ya Ekaristi II**

**226.** Katika Sala ya Ekaristi II, *Ee Bwana, kweli u mtakatifu*, husemwa na *selebranti kiongozi* peke yake akiwa amefumbua mikono.

**227.** Toka *Tunakusihhi uzitakase dhabihu hizi*, mpaka *Tunakuomba, kwa unyenyekevu* zinasemwa na *wakonselebranti* wote pamoja, namna hii:

a) ***Tunakusih*** ***uzitakase dhabihu hizi*** husemwa wakiwa wamenyosha mikono juu ya vipaji;

b) ***Yeye alipojitoa***, na ***Vivyo hivyo*** husemwa wakiwa wamefumba mikono;

c) Husema maneno ya Bwana wakiwa wamenyosha mkono wa kuume juu ya mkate na kikombe, ikiwa inaonekana inafaa. Lakini hostia na kikombe vinapoonyeshwa wanainua macho kuvitazama, na mwishowe huinama sana.

d) Husema ***Kwa hiyo tunakuomba***, na ***Tunakuomba kwa unyenyekevu*** wakiwa wamefumbua mikono.

**228.** Maombi kwa ajili ya waamini walio hai ***Ee Bwana ulikumbuke Kanisa***, na maombi kwa ajili ya wafu ***Uwakumbuke pia ndugu zetu***, yafaa yasemwe na ***konselebranti*** mmoja mmoja. Kila mmoja peke yake ayaseme maneno hayo kwa sauti inayosikika, akiwa amefumbua mikono.

### **Sala ya Ekaristi III**

**229.** Katika Sala ya Ekaristi III ***Ee Bwana, kweli u mtakatifu*** husemwa na ***selebranti kiongozi*** peke yake, akiwa amefumbua mikono.

**230.** Kuanzia ***Basi tunakusih ee Bwana***, mpaka ***Tunaomba uiangalie***, husemwa na ***wakonselebranti*** wote kwa pamoja, namna hii:

a) ***Tunakusih uzitakase dhabihu hizi***, husemwa wakiwa wamenyosha mikono juu ya vipaji.

b) ***Usiku ule alipotolewa***, na, ***Vivyo hivyo*** hufumba mikono.

c) Husema maneno ya Bwana wakiwa wamenyosha mkono wa kuume juu ya mkate na juu ya kikombe, iwapo inafaa. Lakini hostia na kikombe vinapoonyeshwa, wanainua macho na kuvitazama kisha huinama sana.

d) Husema ***Kwa hiyo, Ee Bwana, tunapokumbuka*** na ***Tunaomba uiangalie***, wakiwa wamefumbua mikono.

231. Maombi **Yeye atufanye**, na **Tunakuomba, ee Bwana sadaka** inafaa yasemwe na *konselebranti* mmoja mmoja; kila mmoja peke yake ayaseme maneno hayo akiwa amefumbua mikono.

### **Sala ya Ekaristi IV**

232. Katika Sala ya Ekaristi IV toka **Tunakusifu, ee Baba mwema** mpaka **Yeye aliyekufa na kufufuka kwa ajili yetu**, husemwa na *selebranti kiongozi* peke yake akiwa amefumbua mikono.

233. Kuanzia **Basi, ee Bwana, tunakuomba**, mpaka **Ee Bwana utazame sadaka hii** husemwa na *wakonselebranti* wote kwa pamoja kwa utaratibu huu:

a) **Basi, ee Bwana tunakuomba**, husemwa wakiwa wamenyosha mikono juu ya vipaji;

b) **Nayo saa ya kutukuzwa nawe ilipofika** na **Vivyo hivyo** husemwa wakiwa wamefumba mikono;

c) Husema maneno ya Bwana wakiwa wamenyosha mkono wa kuume (wakiielekeza) juu ya mkate na juu ya kikombe, ikionekana inafaa. Lakini hostia na kikombe vinapoinuliwa juu, wanainua macho kuvitazama, na hatimaye huiinama sana;

d) Wanafumbua mikono wanaposema **Kwa hiyo, ee Bwana tunapoadhimisha**, na **Ee Bwana, uitazame sadaka hii**.

234. Maombi: **Basi sasa, ee Bwana, uwakumbuke wote**, na **Ee Baba mwema, utujalie sisi sote wanao**, inafaa yasemwe na *konselebranti* mmoja mmoja. Kila mmoja peke yake ayaseme maneno hayo, akifumbua mikono.

235. Kuhusu Sala nyinginezo za Ekaristi Takatifu zilizoidhinishwa na Kiti cha Kitume, sala hizo zizingatie kanuni zilizotolewa kwa kila moja.

**236.** *Doksolojia* ya mwisho ya Sala ya Ekaristi husemwa tu na selebranti kiongozi pamoja na wakonselebranti wote ikionekana inapendeza, na kamwe siyo na waamini walei.

### **Ibada-kanuni ya Komunyo**

**237.** Baada ya *Doksolojia* selebranti kiongozi hutoa mwaliko kabla ya Sala ya Bwana akiwa amefumba mikono. Kisha huifumbua na kusema Sala ya Bwana pamoja na *wakonselebranti* wote wakiwa wamefumbua mikono. Waamini wote husema hii Sala ya Bwana.

**238.** *Ee Bwana tunakuomba utuopoe* husemwa na selebranti kiongozi peke yake akiwa amefumbua mikono. *Wakonselebranti* pamoja na waamini; huitikia kwa shangilio mwishoni: ***Kwa kuwa ufalme ni wako.***

**239.** *Ee Bwana Yesu Kristo uliyewaambia mitume wako*, husemwa na selebranti kiongozi peke yake akiwa amefumbua mikono. Baada ya kiitikio ***Awe pia nawe***, shemasi, au kama hayupo, mmojawapo wa *wakonselebranti* huwaalika wote watakiane amani ***Tutakiane amani.*** Wote hutakiana amani. Wale walio karibu na selebranti kiongozi hupokea amani kwake, kabla ya shemasi.

**240.** Wakati ***Mwana Kondoo*** inasemwa, shemasi au mapadri kadhaa kati ya *wakonselebranti* huweza kumsaidia *selebranti kiongozi* kuzimega hostia kwa ajili ya Komunyo ya *wakonselebranti* na ya waamini.

**241.** Baada ya kuweka kipande kidogo cha hostia katika kikombe (*immixtio*) *selebranti kiongozi* peke yake, akiwa amefumba mikono, husema sala kwa sauti ndogo: ***Ee Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu mzima***, au ***Ee Bwana Yesu Kristo usikubali.***

**242.** Baada ya sala hii ya kabla ya Komunyo, *selebranti kiongozi* hupiga goti na kurudi nyuma kidogo. Hapo *wakonselebranti* hujongea mmoja mmoja katikati ya altare; hupiga goti na kutwaa kwa heshima Mwili wa Kristo altareni.



Huushika kwa mkono wa kulia na kuweka mkono wa kushoto chini yake, kisha wanarudi mahali pao. Lakini pengine *wakonselebranti* huweza kubaki mahali pao na kuletewa Mwili wa Kristo wautwae kutoka *patena* inayoshikiliwa na *selebranti kiongozi*, au mmoja wa *wakonselebranti*, (au hata na wengi kati yao), na kupitishwa mbele yao. Au pengine *patena* hupitishwa kutoka *konselebranti* mmoja mpaka mwingine, na kuendelea mpaka kufikia *konselebranti* wa mwisho.

**243.** Halafu *selebranti kiongozi* hutwaa hostia iliyogeuzwa katika Misa hiihii, anaiinua juu kidogo na kuishikilia juu ya *patena*, au juu ya kikombe. Akiwa anawaelekea watu anasema ***Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu.*** Halafu anaendelea na wakonselebranti wengine pamoja na waamini, akisema ***Ee Bwana sistahili.***

**244.** Kisha, *selebranti kiongozi* akiwa ameelekea altare husema kwa sauti ndogo: ***Mwili wa Kristo unilinde nipate uzima wa milele.*** Hapo kwa heshima anakula Mwili wa Kristo. *Wakonselebranti* wanafanya vivyo hivyo wakijikomunisha wenyewe. Baada ya hao, shemasi hupokea Mwili na Damu ya Kristo kutoka kwa *selebranti kiongozi*.

**245.** Damu ya Bwana huweza kupokelewa kwa namna hii: kwa kuinywa moja kwa moja kutoka kwenye kikombe; au kwa kuchovya; au kwa mrija; au kwa kijiko.

**246.** Ikiwa Komunyo inafanyika kwa njia ya kukinywea kikombe moja kwa moja, huwezekana kutumia namna mojawapo ya hizi zifuatazo:

a) *Selebranti kiongozi* hukitwaa kikombe na kusema kwa sauti ndogo ***Damu ya Kristo inilinde nipate uzima wa milele,*** na anakunywa Damu kidogo. Halafu anampa shemasi au *konselebranti*. Kisha huwakomunisha waamini (*rej. nn. 160-162*).

*Wakonselebranti* wanajongea altareni mmoja mmoja, au wawili wawili ikiwa vikombe viwili vinatumika. Hupiga goti na kuinywa

Damu; halafu huupangusa ukingo wa kikombe na kurudi kwenye viti vyao.

b) *Selebranti kiongozi* huinywa Damu ya Bwana akiwa amesimama katikati ya altare kama kawaida.

Lakini *wakonselebranti* huweza kubaki mahali pao wakaletewa kikombe na shemasi au na *wakonselebranti* wengine; au kupokezana kikombe wao kwa wao. Daima kikombe hupanguswa na yule aliyekinywea au na yule anayekileta. Kila mmoja baada ya kukomunika, hurudi mahali pake.

**247.** Kama kuna Damu iliyobaki, hii yote hunywewa hapo altareni na shemasi, akisaidiwa na *wakonselebranti* wengine ikihitajika. Kisha hupeleka kikombe kwenye meza ya pembeni. Hapo yeye shemasi mwenyewe, au akoliti aliyewekwa rasmi hukisafisha na kukipangusa na hukiweka vizuri ilivyo kawaida (*rej. n. 183*).

**248.** Komunyo ya *wakonselebranti* inaweza pia kufanyika kwa namna hii. Kila mmoja hutwaa Mwili wa Bwana altareni na kuupokea, na mara baadaye anakunywa Damu ya Bwana palepale altareni.

Ikiwa hivyo, *selebranti kiongozi* hupokea Komunyo katika maumbo yote mawili kama inavyofanyika kwa kawaida (*rej. n. 158*); lakini *wakonselebranti* wengine hufuata mtindo wowote ule uliochaguliwa katika kupokea kwenye kikombe.

Baada ya Komunyo ya *selebranti kiongozi*, kikombe huwekwa pembeni mwa altare juu ya *korporale* nyingine. *Wakonselebranti* mmoja baada ya mwingine husogea katikati ya altare, wanapiga goti, halafu wanapokea Mwili wa Bwana. Kisha husogea pembeni mwa altare na kuinywa Damu ya Bwana kuendana na mtindo uliochaguliwa wa kupokea kwenye kikombe, kama ilivyoelezwa huko juu.

Shemasi hukomunika na kupangusa kikombe kama ilivyoelezwa hapo juu.

**249.** Komunyo ya wakonselebranti ikifanyika kwa njia ya kuchovya, *selebranti kiongozi* hupokea Mwili na Damu ya Bwana kama kawaida, akiwa mwangalifu ili ibaki Damu ya kutosha kwenye kikombe kwa ajili ya Komunyo ya *wakonselebranti* wenzake. Kisha shemasi, au mmojawapo wa wakonselebranti huandaa, inavyopasa, kikombe pamoja na patena yenye vipande vya hostia. Hii inaweza kufanyika katikati ya altare, au pembeni juu ya korporale nyingine.

*Wakonselebranti* mmoja mmoja huiendea altare, hupiga goti, hukitwaa kipande cha hostia na kukichovya katika kikombe; hula kipande alichokichovya huku akishika *purifikatorio* chini ya mdomo. Baada ya kupokea hurudi mahali walipokuwa tangu mwanzo wa Misa.

Hali kadhalika shemasi hupokea Komunyo kwa kuchovya, akimwitikia ***Amina*** konselebranti anayemwambia: ***Mwili na Damu ya Kristo***. Lakini shemasi kwenye altare hunywa Damu yote iliyobaki, akisaidiwa na *wakonselebranti* ikiwa lazima. Kisha hukihamisha kikombe na kukipeleka kwenye meza ya pembeni ambapo yeye mwenyewe, au *akoliti* aliyewekwa rasmi, hukisafisha kikombe, hukipangusa na kukiweka vizuri, kama ilivyo kawaida.

## **Ibada-kanuni ya Kumalizia**

**250.** Sehemu iliyobaki hadi mwisho wa Misa hufanywa na *selebranti kiongozi* wakati *wakonselebranti* hubaki kwenye viti vyao.

**251.** *Wakonselebranti* kabla hawajaondoka altareni, wanaiinamia sana altare. Lakini selebranti kiongozi pamoja na shemasi wanaiheshimu altare kwa kuibusu kama ilivyo kawaida.

### III. MISA AMBAYO MHUDUMU MMOJA TU ANAHUDHURIA

**252.** Katika Misa inayoadhimishwa na kuhani *selebranti* akiwa na mhudumu mmoja tu anayemsaidia na kuitikia, hufuatwa utaratibu kama ule wa Misa ya pamoja na watu (*rej. nn. 120-169*). Mhudumu huyo huchukua nafasi ya watu kadiri inavyowezekana.

**253.** Lakini mhudumu huyo akiwa ni shemasi, yeye hutimiza majukumu yaliyo yake kama shemasi, (*rej. nn. 171-186*), na pia hushika sehemu nyingine zilizo za watu.

**254.** Kuadhimisha Misa pasipo kuhudhuriwa hata na mhudumu mmoja au walau na mwamini mmoja kusifanyike isipokuwa kwa sababu halisi na maalumu. Katika Misa ya namna hiyo, maamkio na mawaidha ya mwanzo wa Misa, na Baraka ya mwisho wa Misa huachwa.

**255.** Kabla ya Misa vifaa vinavyohitajika huandaliwa juu ya meza ya pembeni, au juu ya altare upande wa kulia.

#### **Ibada-kanuni ya mwanzo**

**256.** Kuhani huijongea altare, na, baada ya kuiinamia sana pamoja na mhudumu, anaiheshimu kwa kuibusu, na kwenda kwenye kiti. Vinginevyo huweza kuchagua kubaki altareni. Akichagua hivyo, Misale pia iwe imekwisha wekwa altareni. Hapo mhudumu, au kuhani mwenyewe anasema Antifona ya kuingia.

**257.** Kisha, kuhani akiwa amesimama na mhudumu hufanya ishara ya Msalaba akisema ***Kwa jina la Baba***. Anamwelekea mhudumu na kumwamkia kwa kutumia mojawapo ya fomula zilizopendekezwa.

**258.** Halafu hufanya sala ya toba, ikifuatwa na ***Bwana Utuhurumie***, pamoja na ***Utukufu*** ikiwa unatakiwa na *rubrika*.

**259.** Kisha husema **Tuombe**, akiwa amefumba mikono. Hukaa kimya kwa muda mfupi wa kufaa, halafu anafumbua mikono na kusema **Kolekta**. Mwishoni mhudumu anaitikia. **Amina**.

### **Liturujia ya Neno**

**260.** Ni vema kadiri inavyowezekana, masomo yasomwe kwenye mimbari au kwenye lekterni (kosomeo).

**261.** **Kolekta** ikiisha somwa, mhudumu husoma Somo la Kwanza na Zaburi; halafu Somo la Pili kama lipo, pamoja na aya ya Aleluya au Wimbo mwingine.

**262.** Baada ya hayo kuhani huinama na kusema **Ee Mungu Mwenyezi unitakase moyo wangu** na kusoma Injili. Mwishoni husema **Hilo ndilo Neno la Bwana**. Mhudumu hujibu **Sifa kwako, ee Kristo**. Kisha kuhani hutoa heshima kwa kitabu kwa kukibusu, akisema kwa sauti ndogo **Dhambi zetu ziondolewe**.

**263.** Halafu kuhani na mhudumu husema Kanuni ya Imani, ikiwa inatakiwa na rubrika.

**264.** Hufuata maombi kwa wote ambayo huweza kusemwa hata katika Misa za namna hii. Kuhani huanzisha na kufunga maombi; mhudumu hutaja nia za maombi hayo.

### **Liturujia ya Ekaristi Takatifu**

**265.** Katika Liturujia ya Ekaristi, yote hufanyika kama katika Misa ya Pamoja na Watu, isipokuwa haya yafuatayo.

**266.** Baada ya shangilio mwishoni mwa Embolismo inayofuata baada ya Sala ya Bwana, kuhani husema sala **Ee Bwana Yesu Kristo uliyewaambia**. Ikiisha, huongeza: **Amani ya Bwana iwe daima nanyi**. Na, mhudumu huitikia **Iwe pia nawe**. Ikiwa inafaa kuhani humpatia mhudumu amani.

**267.** Kisha, kuhani anaposema **Mwana Kondoo** pamoja na mhudumu, wakati huohuo humega hostia juu ya patena. Baada ya kumaliza **Mwana Kondoo wa Mungu**, anatia kipande

kidogo cha hostia katika kikombe akisema kwa sauti ndogo:  
***Huku kuchanganya.***

**268.** Baada ya hayo, husema kwa sauti ndogo sala ***Ee Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu mzima au Ee Bwana Yesu Kristo usikubali.*** Kisha hupiga goti, na kuchukua hostia. Na ikiwa mhudumu hupokea Komunyo, humgeukia akiwa ameinua hostia kidogo juu ya patena au juu ya kikombe, na kusema ***Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu.*** Wote wawili kwa pamoja wanaongeza mara moja ***Ee Bwana sistahili.*** Kisha hugeuka altareni na kula Mwili wa Kristo. Lakini ikiwa mhudumu hashiriki Komunyo, kuhani akisha piga goti; akiwa anaelekea altare, husema mara moja kwa sauti ndogo: ***Ee Bwana sistahili,*** na ***Mwili wa Kristo unilinde nipate uzima wa milele,*** na hapo huupokea Mwili wa Kristo. Kisha huchukua kikombe na kusema kwa sauti ndogo: ***Damu ya Kristo inilinde nipate uzima wa milele*** na kuipokea Damu.

**269.** Kabla ya kumpa mhudumu Komunyo, mhudumu au kuhani mwenyewe husoma Antifona ya Komunyo.

**270.** Kuhani husafisha kikombe altareni au kwenye meza ya pembeni. Iwapo anakisafisha kikombe kwenye altare, anaweza kukiweka pembeni juu ya altare, au mhudumu anaweza kukihamishia kwenye meza ya pembeni.

**271.** Baada ya kusafisha kikombe, inafaa kuhani akae kwa muda mfupi katika ukimya; halafu baadaye aseme Sala Baada ya Komunyo.

## **Ibada-kanuni ya Kumalizia**

**272.** Ibada ya kumalizia hufanyika kama ilivyo katika Misa ya Pamoja na Watu, isipokuwa “Nendeni na amani” huachwa. Kuhani hutoa heshima kwa altare kwa kuibusu kama kawaida. Mwisho, yeye na mhudumu huiinamia sana altare na kuondoka.

## IV. KANUNI KUU KADHAA ZINAZOHUSU MITINDO YOTE YA MISA

### Heshima kwa Altare na Kitabu cha Injili

**273.** Kadiri ya desturi za mapokeo katika Liturujia, heshima kwa Altare na kwa Kitabu cha Injili hukamilishwa kwa kitendo cha kubusu.

Lakini pale ambapo ishara ya namna hii haipatani kabisa na mila au tabia ya nchi fulani, ni juu ya Baraza la Maaskofu kuamua itumike ishara nyingine inayofaa, badala ya hiyo, baada ya kupata kibali cha Kiti cha Kitume.

### Kupiga goti na kuinama

**274.** Kupiga goti, tendo ambalo hufanyika kwa kukunja goti la mguu wa kulia mpaka kugusa chini, humaanisha kuabudu. Ndiyo maana hufanyika tu kwa Sakramenti Takatifu, na kwa Msalaba Mtakatifu kuanzia Ibada Kuu ya Kuabudu Msalaba siku ya Ijumaa Kuu ya Mateso ya Bwana, hadi mwanzo wa Kesho la Pasaka.

Wakati kuhani anapoadhimisha Misa, hupiga goti mara tatu; yaani baada ya kuonyesha hostia, baada ya kuonyesha kikombe na kabla ya Komunyo. Mabadiliko ya kipekee yanayotakiwa kuzingatiwa kwenye Misa ya *konselebrasio* yanaonyeshwa mahali pake (*rej. nn. 210-251*).

Lakini ikiwa *tabernakulo* yenye Sakramenti Takatifu ipo patakatifuni, kuhani, shemasi na wahudumu wengine hupiga goti wanapofika altareni na wanapoondoka; ila hawafanyi hivyo wakati inapoadhimishwa Misa yenyewe.

Hali kadhalika wote hupiga goti wanapopita mbele ya Sakramenti Takatifu, isipokuwa wakipita wakiwa wanaandamana.

Wahudumu ambao kwenye maandamano wanachukua Msalaba au mishumaa, huinama kichwa badala ya kupiga goti.

**275.** Kuinama kunamaanisha heshima na taadhima inayotolewa kwa nafsi zenyewe za watu, au kwa ishara zao. Kuna namna mbili za kuinama, yaani kuinama kichwa au mwili, maana yake kiwiliwili.

a) Kuinama kwa kichwa hufanyika kila mara Nafsi Tatu za Mungu zinapotajwa pamoja, na kwa jina la Yesu, la Bikira Maria Mwenye heri, na la Mtakatifu ambaye Misa inaadhimishwa kwa heshima yake.

b) Kuinama kwa mwili, au kuinama sana hufanyika kwa kuinamisha kiwiliwili mbele ya altare; wakati wa Sala ***Ee Mungu Mwenyezi utakase moyo wangu***, na ***Ee Bwana utupokee***, na katika Ungamo la Imani kwenye maneno ***Akapata Mwili***; na katika Kanuni ya Kiroma kwenye maneno ***Ee Mungu Mwenyezi, tunakuomba kwa unyenyekevu***. Shemasi anapoomba baraka kabla ya kutangaza Injili huiinama vivyo hivyo. Aidha, kuhani huiinama vivyo hivyo wakati wa *konsekrasio* anapotamka maneno ya Bwana.

## **Kuhusu Kufukizia Ubani**

**276.** Kufukizia ubani au kutumia uvumba huonyesha hisia za taadhima na sala kama inavyojionyesha katika Maandiko Matakatifu (*rej. Zab 141:2, Ufu 8:3*).

Ubani waweza kutumiwa kwa hiari katika mitindo yote ya Misa:

a) wakati wa maandamano ya kuingia;

b) mwanzoni mwa Misa, vinapofukiziwa msalaba na altare,

c) kwenye maandamano ya Kitabu cha Injili, na kabla ya kuitangaza Injili,

d) mkate na kikombe, vikiisha wekwa altareni hufukiziwa dhabihu, halafu msalaba, altare, kuhani na pia waamini;

e) wakati hostia na kikombe vinapoonyeshwa baada ya *konsekrasio*.



**277.** Wakati kuhani anapoweka ubani katika chetezo, huubariki kwa ishara ya msalaba pasipo kusema neno.

Kabla na baada ya kufukizia ubani mwenye kufukizia hufanya inamio kubwa mbele ya mtu au kitu kinachofukiziwa, isipokuwa kwa altare na kwa vipaji vilivyoandaliwa kwa ajili ya sadaka ya Misa.

Kufukizia hufanyika kwa mapembeo kama ifuatavyo: Kwa mapembeo matatu mara tatu ya chetezo hufukiziwa Sakramenti Kuu Takatifu, masalia ya Msalaba Mtakatifu, na Sanamu za Bwana zilizowekwa kwa ajili ya ibada ya hadhara; vipaji kwa ajili ya sadaka ya Misa, msalaba altareni, Mshumaa wa Pasaka, Kitabu cha Injili, kuhani na watu.

Kwa mapembeo mawili mawili, mara tatu hufukiziwa masalia na sanamu za Watakatifu zilizowekwa kwa ajili ya ibada ya hadhara. Fukizio hili hufanyika tu mwanzoni mwa Misa baada ya kufukizia altare.

Altare hufukiziwa kwa pembeo moja moja tu la chetezo kwa namna hii:

- a) ikiwa kuna nafasi kati ya altare na ukuta, kuhani anaifukizia kwa kuizunguka;
- b) ikiwa altare imejengwa kwa kuungana na ukuta, kuhani huifukizia akipitia kwanza upande wa kulia, halafu upande wa kushoto.

Msalaba ukiwepo juu ya altare, au karibu na altare, hufukiziwa kabla ya kufukizia altare; kwa vingine kuhani anaufukizia anapopita mbele yake.

Kuhani hufukizia dhabihu kwa mapembeo matatu ya chetezo kabla ya kufukizia msalaba na altare; au anachora ishara ya Msalaba juu ya dhabihu kwa chetezo.

## **Kuhusu Kusafisha**

**278.** Kila mara vipande vidogovidogo vinapokuwa vimenata kwenye vidole, hasa baada ya kumega hostia au baada ya kugawia waamini Komunyo, kuhani apanguse vidole juu ya patena, au ikiwa lazima, anawe vidole. Hali kadhalika kama kuna vipande vilivyoanguka nje ya patena, hivi navyo avikusanye na kuvipangusia katika kikombe.

**279.** Vyombo vitakatifu husafishwa na kuhani au shemasi, au *akoliti* aliyewekwa rasmi. Hii hufanyika baada ya Komunyo, au baada ya Misa, ikiwezekana kwenye meza ya pembeni. Kikombe husafishwa kwa maji tu, au kwa divai na maji ambayo yule mwenye kusafisha huyanywa. *Patena* kwa kawaida hupanguswa kwa *purifikatorio*.

Kuwepo na uangalifu, ili ikitokea kuwa Damu ya Kristo imebaki kidogo baada ya kugawa Komunyo, hii inywewe mara moja pale altareni.

**280.** Ikiwa hostia au kipande kidogo cha hostia kimeanguka, iokotwe kwa heshima na kupokewa. Na kama Damu takatifu kidogo imemwagika chini, hapo ilipomwagikia paoshwe kwa maji ambayo baadaye yanamwagwa kwenye *sakrario* (shimo la kutupa mabaki ya vitu vitakatifu) iliyopo katika sakristia.

## **Komunyo Katika Maumbo Yote Mawili**

**281.** Komunyo takatifu inayofanyika katika maumbo yote mawili inayo sura kamilifu zaidi inayotoa ishara iliyo wazi zaidi. Kwa maana katika mtindo huu, ishara ya karamu ya kiekaristi inajitokeza kwa ukamilifu zaidi; na pia lile azimio la Mungu ambalo kwa azimio hilo Agano Jipya na la milele lilithibitishwa kwa Damu ya Bwana, linajionyesha zaidi. Hata na ule uhusiano uliopo kati ya karamu ya kiekaristi na ile karamu ya milele katika ufalme wa Baba unajieleza zaidi.<sup>105</sup>

**282.** Wachungaji wajitahidi kadiri inavyowezekana kuwakumbusha waamini wanaoshiriki ibada na wanaohudhuria ibada yale mafundisho ya kikatoliki juu ya utaratibu wa

Komunyo takatifu jinsi ulivyotolewa na Mtaguso wa Trento. Awali ya yote wawaonye waamini kwamba Imani Katoliki inafundisha kuwa Kristo yuko mzima na kamili katika kila mojawapo ya maumbo ya Ekaristi, hivyo kwamba sakramenti inapokewa hata katika umbo moja tu. Kwa hiyo, kuhusu matunda ya Komunyo, waamini wanaopokea umbo moja tu hawapunjwi, wala hawanyimwi neema yoyote itakiwayo kwa wokovu.<sup>106</sup>

Zaidi ya hayo, wachungaji hao wawaelimishe waamini kwamba kuhusu kuadhimisha Sakramenti, Kanisa linayo mamlaka ya kuweka au kubadili mambo mengine, ilimradi kiini na misingi ya Sakramenti hizo haibadilishwi. Mambo yanayoweza kubadilishwa, hutokana na tofauti za mazingira, nyakati au mahali. Kanisa hufanya hivyo linapoonna kuwa mabadiliko hayo yataongeza heshima kwa sakramenti hizo na kuleta manufaa kwa wale wanaozipokea.<sup>107</sup> Lakini wakati huohuo, waamini wahimizwe kutamani sana kushiriki lile tendo takatifu la kupokea katika maumbo mawili, ambamo ishara ya karamu ya kiekaristi hung'ara kwa uwazi zaidi.

**283.** Kupokea Komunyo katika maumbo yote mawili huruhusiwa katika nafasi nyingine licha ya nafasi zile maalum zilizotajwa katika vitabu vya lituruja:

- a) kwa makuhani wasioweza kuadhimisha wao wenyewe au wasioweza kuadhimisha Misa ya *konselebrasio*;
- b) kwa shemasi na wengine ambao hutimiza kazi fulani katika Misa;
- c) kwa wanajumuiya katika Misa ya Shirikani, au katika ile Misa iitwayo ya *Jumuiya*; kwa wanafunzi seminarini; kwa wote wanaoshiriki mazoezi ya kiroho; au wanaohudhuria mkutano wa kiroho, au wa kichungaji.

Askofu-Jimbo anaweza kuweka sheria kuhusu Komunyo katika maumbo yote mawili kwa jimbo lake, ambazo zitafuatwa pia katika makanisa ya watawa na katika makundi madogo

madogo. Hali kadhalika, Askofu-Jimbo anayo mamlaka ya kuruhusu Komunyo itolewe katika maumbo yote mawili, kila mara kuhani anayeadhimisha anapona ni jambo la kufaa, mradi tu waamini wawe wameelimishwa vizuri. Na tena anapofanya hivyo, isiwepo hatari yoyote ya kukufuru Sakramenti, au ya kuifanya ibada kuwa ngumu zaidi, kutokana pengine na wingi wa wanaoshiriki, au kwa sababu nyingine yoyote.

Lakini, kuhusu namna ya kutoa Komunyo ya maumbo mawili kwa waamini, na pia kuhusu upanuzi wa mamlaka ya kufanya hivyo, hilo linayaangukia Mabaraza ya Maaskofu, ambayo yanaweza kutunga sheria ambazo zitahitaji kuidhinishwa na Kiti cha Kitume.

**284.** Komunyo inapotolewa katika maumbo mawili, yazingatiwe yafuatayo:

a) huduma ya kikombe kwa kawaida ni ya shemasi. Au kama hayuko, padri aifanye. Inaweza pia kufanywa na *akoliti* aliyedhinishwa rasmi; au mhudumu mwingine wa dharura wa Komunyo takatifu; au kutokana na shida maalum, mwamini wa kawaida anaweza kukabidhiwa huduma hiyo kwa wakati huo;

b) ikitokea kwamba Damu ya Kristo imebaki kidogo, inywewe pale altareni na padri, au na shemasi, au na *akoliti* aliyewekwa rasmi ambaye alikihudumia kikombe na ndiye atakayevisafisha, kuvipangusa na kuvipanga vizuri vyombo vitakatifu, kama inavyotakiwa.

Kwa waamini ambao huenda wakataka kushiriki kwa kupokea umbo la mkate tu, Komunyo takatifu itolewe kwao kwa namna hiyo.

**285.** Kwa ajili ya kutoa Komunyo katika maumbo yote mawili yaandaliwe yafuatayo:

a) ikiwa Komunyo ya damu hufanyika kwa kunywa moja kwa moja kutoka kwenye kikombe, kiandaliwe kikombe chenye ujazo wa kutosha, au vikombe kadhaa, ila kuwe na uangalifu

daima ili isije ikabaki Damu ya Kristo kupita kiasi, ambayo ni lazima inywewe mwishoni mwa adhimisho;

b) ikiwa inafanyika kwa kuchovya, iangaliwe hostia zisiwe ndogo mno wala nyepesi mno, bali ziwe nene na nzito kidogo kuliko kawaida, ili ziweze kutolewa kwa urahisi baada ya kuchovya sehemu katika Damu ya Bwana.

**286.** Ikiwa Komunyo ya Damu imefanyika kwa kukinywea kikombe, mshiriki, baada ya kuupokea Mwili wa Kristo, humwendea mhudumu wa kikombe na kusimama mbele yake. Mhudumu husema: ***Damu ya Kristo***. Mshiriki huitika: ***Amina***. Mhudumu humtolea kikombe, ambacho mshiriki hukisogeza mwenyewe mdomoni kwa mikono yake. Hunywa kidogo kutoka kikombeni; hukirudisha kwa mhudumu, halafu hurudi mahali pake. Mhudumu hupangusa ukingo wa kikombe kwa purifikatorio na kuwa tayari kumpokeza mshiriki anayefuata.

**287.** Ikiwa Komunyo ya kikombe inafanyika kwa kuchovya, mshiriki hushika patena chini ya mdomo wake, halafu humjongea kuhani ambaye huwa ameshika chombo chenye hostia, na kando yake yuko mhudumu aliyeshika kikombe. Kuhani hutwaa hostia na kuchovya sehemu yake kwenye kikombe; na, kwa kumwonyesha mpokeaji akisema: ***Mwili na Damu ya Kristo***. Mpokeaji huitika: ***Amina***, na kupokea Sakramenti mdomoni, halafu anaondoka.

## Sura ya Tano

# YANAYOHUSU MAANDALIZI NA MAPAMBO YA MAKANISA KWA AJILI YA KUADHIMISHA EKARISTI TAKATIFU

### I. KANUNI ZA JUMLA

**288.** Kwa ajili ya kuadhimisha Ekaristi takatifu, watu wa Mungu kwa kawaida hukusanyika katika kanisa, au kama hakuna kanisa, au kama kanisa lililopo ni dogo mno, hukutanika mahali pengine palipo nadhifu, na penye hadhi ya kuadhimishia fumbo hili kuu. Kwa hiyo makanisa, au mahali pengine, ni lazima pawe ni pa kufaa kwa kutimizia tendo hili takatifu, pamoja na kurahisisha ushiriki hai wa waamini. Aidha, majengo matakatifu na vitu vyote vinavyohusika na ibada takatifu viwe na ustahivu wa kweli; pia viwe vizuri na vyenye kuweza kuwa ishara na mfano wa mambo ya mbinguni.<sup>108</sup>

**289.** Ndiyo maana Kanisa daima hutafuta msaada wa sanaa bora, na hukubali kutumia vielelezo vya sanaa za mataifa yoyote na nchi zozote.<sup>109</sup> Kwa sababu hiyo Kanisa hujitahidi kuhifadhi kazi za sanaa na hazina zilizorithishwa tangu zamani za kale;<sup>110</sup> na kadri inavyowezekana huzilinganisha na mahitaji ya kisasa. Pia huendeleza na kukuza mambo mapya yanayopatana na utamaduni wa kila kizazi.<sup>111</sup>

Kwa hiyo, katika kuwaelekeza wasanii na kuchagua kazi za sanaa zinazoruhusiwa kwa matumizi katika kanisa, sharti kuangalia uzuri halisi wa sanaa zinazoimarisha imani na uchaji, na zenye kuendana na ukweli wa ishara na lengo linalokusudiwa.<sup>112</sup>

**290.** Makanisa yote yatabarukiwe, au walau yabarikiwe. Lakini, makatedrali na makanisa ya kiparokia yanatakiwa yatabarukiwe kwa ibada kuu.

**291.** Yeyote anayehusika katika mipango ya ujenzi, marekebisho au ukarabati wa makanisa, hupaswa kushauriana na Kamati ya Jimbo ya Liturujia, na ya Sanaa ya Mambo ya Dini. Naye Askofu Jimbo atumie ushauri na msaada wa kamati hiyo anapotoa miongozo juu ya mambo haya, au anapoidhinisha ramani za majengo mapya, au kila anapotoa uamuzi kwa masuala mengine magumu.<sup>113</sup>

**292.** Mapambo kanisani yawe na lengo la kuleta heshima na unadhifu kuliko fahari ya kujivunia. Katika kuchagua vitu vya msingi vinavyohusikana na kutia nakshi, ni lazima kuzingatia ukweli wa vitu, na mambo yathibitiwe hivyo kwamba yatachangia malezi ya waamini na kukuza heshima ya pote patakatifu.

**293.** Mpangilio mzuri wa kanisa na makandokando yake ambao unaendana barabara na nyakati zetu, unadai kushughulikia siyo tu vitu vile vinavyohusika moja kwa moja na adhimisho la ibada takatifu, bali pia kufikiria kabla, vile vitu vinavyowafanya waamini wawe na starehe na utulivu, ambavyo kwa kawaida vinatazamiwa viwepo popote watu walipozoea kukusanyika.

**294.** Taifa la Mungu linalokusanyika kwa ajili ya Misa, lina muundo unaofungamana, na wa *kihierarkia*. Muundo huu unadhihirishwa kwa huduma na matendo mbalimbali yanayofanywa katika sehemu mbalimbali za adhimisho la Misa. Kwa hiyo, mpangilio wa jumla wa jengo takatifu, unatakiwa uonyeshe wenyewe kwa namna fulani, picha ya jumuiya inayokusanyika humo. Vilevile mpangilio huo uruhusu nafasi inayofaa kwa wote, pamoja na kuwawezesha kila mmoja kutekeleza majukumu yake, kama inavyotakiwa.

Waamini na kikundi cha waimbaji watakuwa na mahali pao patakorahisisha ushirikiano wao kuwa hai zaidi.<sup>114</sup>

Kuhani *selebranti*, shemasi na wahudumu wengine wawe na nafasi zao katika patakatifu. Papo hapo viandaliwe viti kwa ajili ya *wakonselebranti*. Lakini ikiwa idadi yao ni kubwa, viti vyao viwekwe katika sehemu nyingine ya kanisa karibu na altare.

Mambo haya yote, ingawa yanapaswa kuonyesha mpangilio wa *kihierarkia* na tofauti za majukumu, ni lazima wakati wote yaunde fungamano lililokamilika kutokana na sehemu zake mbalimbali, fungamano ambalo linaonyesha kwa dhati umoja wa taifa lote takatifu la Mungu. Kwa yakini, umbo na uzuri wa mahali, pamoja na nakshi zake zote sharti zikuze na kusitawisha moyo wa sala, na kuonyesha utakatifu wa mafumbo yanayoadhimishwa mahali hapo.

## **II. MAANDALIZI YA PATAKATIFU KWA AJILI YA KUSANYIKO LA KIIBADA**

**295.** Patakatifu ndipo mahali inapokaa altare, panapotangaziwa Neno la Mungu, wanapokaa kuhani, shemasi na wahudumu wengine wanapotimizia majukumu yao. Sehemu hii itofautiane na sehemu za kukaa watu (**aula**), kwa namna ya kufaa. Inaweza kutofautiana kwa kuinuka juu kidogo, au kwa umbo na nakshi maalum. Pawe na nafasi ya kutosha ili adhimisho la Ekaristi liweze kufanyika kwa raha, na liweze kuonekana bila shida.<sup>115</sup>

### **Altare na mapambo yake**

**296.** Altare, ambapo hufanyika uwepo wa sadaka ya msalaba kwa ishara za kisakramenti, ni pia meza ya Bwana. Taifa la Mungu huitwa kushiriki meza hii linapokusanywa katika Misa. Kwa hiyo altare ni kiini cha tendo la shukrani, ambalo hutimizwa kwa njia ya Ekaristi Takatifu.

**297.** Adhimisho la Ekaristi Takatifu, kwenye mahali patakatifu, yapasa lifanywe juu ya altare; lakini pia laweza kufanywa nje ya mahali patakatifu, hata juu ya meza inayofaa, ila ni lazima daima kutumia kitambaa na *corporale*; msalaba na mishumaa.

**298.** Katika makanisa yote inafaa pawepo na altare iliyosimikwa imara mahali pake ambayo kwa namna iliyo wazi zaidi na ya kudumu inamwashiria Kristo Yesu aliye Jiwe lililo hai (*1Pet 2: 4; rej. Efe 2:20*). Hata hivyo mahali pengine palipotengwa kwa ajili



ya kuadhimishia matakatifu panaweza kuwekwa altare ya kuhamishwa.

Altare iliyosimikwa imara mahali pake ni ile iliyojengwa kwa kuunganika na sakafu hivyo kwamba haiwezi kuhamishwa au kusogezwa kutoka mahali hapo ilipo. Altare isiyosimikwa ni ile inayoweza kusogezwa na kuhamishiwa mahali pengine.

**299.** Kila inapowezekana inafaa Altare ijengwe hivyo kwamba imetengwa kutoka kwenye ukuta ili wahudumu waweze kuizunguka kwa urahisi; nayo Misa iweze kuadhimishwa waselebranti wakiwa wamewaelekea watu.

Altare iwekwe mahali ambapo, kwa yakini ni pa katikati, hivyo kwamba fikra za jamii yote ya waamini waliokusanyika ziweze kuelekea altare hiyo kwa urahisi.<sup>116</sup> Kwa kawaida iwe imesimikwa imara na kutabarukiwa.

**300.** Altare yoyote, iwe iliyosimikwa imara, au isiyosimikwa, itabarukiwe kulingana na maelezo ya Ibada-kanuni ya *Pontifikale* ya Kiroma. Lakini altare isiyosimikwa inaweza hata kubarikiwa tu.

**301.** Kuendana na mapokeo ya Kanisa na maana yenyewe ya altare, kwa kawaida, meza ya altare iliyosimikwa hupaswa kuwa ya jiwe asilia. Lakini huweza pia kutengenezwa na kitu kingine kilicho thabiti, imara na kinachofaa, kwa kibali cha Baraza la Maaskofu . Miguu au sehemu ya chini huweza kutengenezwa kwa kitu chochote kinachofaa na kilicho thabiti na imara.

Altare isiyosimikwa huweza kutengenezwa kwa vitu vya thamani na vyenye hadhi ya juu na vigumu, vinavyofaa kwa matumizi ya liturujia kuendana na mapokeo na desturi za nchi mbalimbali.

**302.** Desturi ya kuweka masalia ya Watakatifu hata kama si wafiadini, chini ya altare inayotabarukiwa inafaa iendeleo. Lakini kuwe na tahadhari ya kuhakikisha uhalisi wa masalia hayo.

**303.** Katika kujenga makanisa mapya, ni jambo bora sana kujenga altare moja tu, ambayo katika kusanyiko la waamini huashiria Kristo aliye mmoja, na Ekaristi moja ya Kanisa.

Lakini kuhusu makanisa yaliyokwisha jengwa, ikiwa kuna altare ya zamani ambayo husababisha ugumu waamini wanapohudhuria Misa, na wala haiwezi kuhamishwa bila madhara makubwa kwa tunu za sanaa, basi ijengwe altare nyingine ya kusimikwa. Hii itengenezwe kwa ufundi stadi na itabarukiwe kulingana na ibada hiyo. Halafu maadhimisho yote matakatifu yawe yanafanyika hapo tu. Tena, ili mawazo ya waamini yasivutwe mbali na hiyo altare mpya, ile ya zamani isipambwe kwa namna ya kipekee.

**304.** Kwa ajili ya kuonyesha heshima ya pekee kwa adhimisho la Ukumbusho wa Bwana, na kwa Karamu ambamo Mwili na Damu ya Bwana hutwaliwa, juu ya altare ambapo adhimisho hili hufanywa patandikwe kitambaa cheupe angalau kimoja. Kitambaa hicho kilandane na muundo wa altare mintarafu umbo, vipimo na mapambo.

**305.** Katika kuipamba altare kuweko na kiasi.

Kipindi cha Majilio, altare hupambwa maua kwa kiasi kinachotakiwa na tabia ya kipindi hicho, isije ikatokea kuwa furaha yote ya Kuzaliwa Bwana imetangulizwa kabla ya muda wake. Kipindi cha Kwaresima altare haipambwi kwa maua. Lakini inaruhusiwa kuipamba katika Dominika ya **Laetare** (ya Nne ya Kwaresima), katika Sherehe, na Sikukuu.

Mapambo ya maua daima yawe na kiasi, na hasa yawekwe kandokando ya altare kuliko juu ya meza ya altare.

**306.** Juu ya meza ya altare vyaweza kuwekwa tu vile vitu vinavyotakiwa kwa adhimisho la Misa, yaani: Kitabu cha Injili, tangu mwanzo wa adhimisho hadi wakati wa kuitangaza Injili. Tangu kuleta vipaji mpaka kusafisha vyombo, inawezekana kuweka kikombe pamoja na *patena*, (na *siborio* kama inahitajika), *korporale*, *purifikatorio*, na Misale.

Viwekwe pia (kwa hadhari) vifaa ambavyo huenda vikahitajika kwa ajili ya kupazia sauti ya kuhani.

**307.** Vinara vya mishumaa vinavyotakiwa (*rej. n. 117*) kwa ajili ya kila tendo la kiliturujia, kwa sababu ya kukuza heshima na shangwe kisikukuu, viwekwe juu ya altare, au kandokando yake, kutegemeana na umbo la altare yenyewe, na pia jinsi patakatifu palivyojengwa. Viwekwe kwa namna ya kufaa hivi kwamba waamini hawatazuiwa kuona kwa urahisi vitu vilivyowekwa juu ya altare, au matendo yanayofanyika juu ya altare.

**308.** Hali kadhalika, juu ya altare, au karibu nayo, pawe na msalaba wenye sanamu ya Kristo Msulibiwa – msalaba wenye kuonekana vizuri kwa watu waliokusanyika. Inafaa sana msalaba huo, wenye kuwakumbusha waamini Mateso ya Bwana yaliyotuletea wokovu, ubaki karibu na altare hata nje ya maadhimisho ya kiliturujia.

## **Mimbari**

**309.** Ustahivu na ukuu wa Neno la Mungu huhitaji pawepo mahali katika Kanisa, panapofaa kwa kutangazia Neno hilo; na ambapo, waamini hujisikia kwa msukumo wa ndani kupaelekezea mioyo yao kwa urahisi wakati wote wa Liturujia ya Neno.<sup>117</sup> Kwa kawaida inafaa mahali pa namna hiyo pawe na mimbari imara, siyo kosomeo (**legile**) cha kusogezwasogezwa tu. Mimbari, katika kanisa lenye muundo wowote ule, inapaswa kujengwa kwa namna ambayo wahudumu wenye Daraja, na wasomaji wengine, huweza kuonekana na kusikika vizuri na waamini.

Kwenye mimbari husomwa Masomo, Zaburi za kuitikizana, na Mbiu ya Pasaka tu. Vivyo hivyo kwenye mimbari, huweza kutolewa homilia na nia za maombi kwa watu wote. Hadhi ya mimbari inadai kuwa mhudumu wa Neno peke yake akwee mahali hapo.

Inafaa mimbari mpya ibarikiwe kabla ya kuanza kutumika katika liturujia. Ndivyo inavyotakiwa kulingana na Ibada-kanuni ilivyoelezwa katika *Rituale* ya Kiroma.<sup>118</sup>

### **Kiti kwa ajili ya kuhani *selebranti* na viti vingine**

**310.** Kiti cha kuhani *selebranti* kinapaswa kudokeza jukumu lake la kusimamia mkusanyiko, na kuongoza sala. Kwa hiyo mahali pake panapofaa zaidi ni sehemu ya mbele ya Patakatifu kuwaelekea watu, isipokuwa muundo wa jengo au makandokando mengine yameweka kizuizi, kwa mfano, ikiwa mawasiliano kati ya kuhani na watu yatakuwa ya shida kwa sababu ya umbali; au kama tabernakulo iko katikati, nyuma ya altare. Aina yoyote inayoelekea mtindo wa “kiti cha enzi” imekatazwa.<sup>119</sup> Inafaa kiti hiki kibarikiwe kabla ya kuanza kutumiwa katika Liturujia, kama inavyotakiwa na ibada-kanuni katika *Rituale* ya Kiroma.<sup>120</sup>

Hali kadhalika, katika patakatifu viwepo viti vingine kwa ajili ya makuhani wakonselebranti na pia kwa ajili ya mapadri wengine wanaohudhuria adhimisho wakiwa wamevaa mavazi ya kikwaya (**veste choral**) hata kama hawashiriki *konselebrasio*.

Kiti cha shemasi kiwe karibu na kiti cha kuhani *selebranti*. Viti vya wahudumu wengine viwekwe kwa namna ya kuvitenga na vile vya *makleri*, waweze kutimiza kwa urahisi majukumu yao.<sup>121</sup>

## **III. MPANGILIO WA KANISA**

### **Mahali pa waamini**

**311.** Mahali pa waamini paandaliwe kwa uangalifu hivi kwamba waweze ipasavyo kushiriki vema katika maadhimisho matakatifu kwa macho yao na mioyo yao. Basi, kama ilivyo kawaida, waamini wawekewe mabenchi au viti. Walakini desturi ya kuwawekea watu fulani fulani binafsi nafasi “za kipekee”, imepigwa marufuku.<sup>122</sup> Kwa hiyo, hasa katika makanisa mapya yanayojengwa, mabenchi au viti vipangwe hivi kwamba, kwa

urahisi waamini wataweza kukaa inavyotakiwa kuendana na sehemu tofauti za adhimisho, na kuweza kwenda kupokea Komunyo takatifu kwa urahisi.

Kuwepo na uangalifu pia ili isiwe kwamba waamini wanamwona tu kuhani, au shemasi na wasomaji; bali pia wawezeshwe kuwasikia vizuri kwa kutumia vyombo vya teknolojia ya kisasa.

### **Mahali pa kikundi cha kwaya na ala za muziki**

**312.** Kwa kuzingatia muundo wa kila kanisa, kikundi cha waimbaji kipangiwe mahali ambapo panaonyesha waziwazi umuhimu wa kikundi hicho, na kwamba ki sehemu ya jumuiya ya waamini waliokusanyika, na kinalo jukumu maalum la kutekeleza. Tena kipewe misaada ili huduma zake za kiliturujia zitekelezwe kwa urahisi. Hali kadhalika, kila mwanakwaya apewe fursa ya kushiriki sakramenti kikamilifu katika Misa bila shida.<sup>123</sup>

**313.** Kinanda na ala za muziki zilizokubaliwa kihalali ziwekwe mahali panapofaa, kusudi ziweze kuwasaidia waimbaji na waamini wanaoimba. Isitoshe, kama ala hupigwa peke yake, zipigwe hivyo kwamba zinasikika vizuri na watu wote. Inafaa kinanda kibarikiwe kabla ya kuanza kukitumia katika Liturujia, kulingana na ibada-kanuni zilivyoielezwa katika Rituale ya Kiroma.<sup>124</sup>

Wakati wa Majilio, kinanda na ala nyingine za muziki zitumike kwa kiasi ambacho kinaendana na roho ya kipindi hicho, ili isije ikatokea kwamba furaha kuu ya Sherehe ya Kuzaliwa Bwana imewasilishwa kabla ya wakati wake.

Wakati wa Kwaresima kinanda na ala nyingine vinaruhusiwa tu vitumike kwa namna ya kutegemeza nyimbo. Lakini hupigwa katika Dominika ya **Laetare** (ya Nne ya Kwaresima), Sherehe na Sikukuu.

## Mahali pa kuhifadhia Ekaristi takatifu

**314.** Kuendana na umbo lolote la kanisa, na kulingana na desturi mahalia zilizoidhinishwa, Ekaristi Takatifu ihifadhiwe kwenye tabernakulo katika sehemu ya kanisa iliyo na hadhi kubwa, yenye ustahivu, inayoonekana kwa urahisi, iliyopambwa vizuri, na yenye kufaa kwa ajili ya sala.<sup>125</sup>

Kwa kawaida *tabernakulo* iwe ni moja tu, isiyosogezeka, iliyojengwa imara na thabiti, isiyoruhusu mtu aliye nje aweze kuona vilivyoko ndani (non transparenti); na iwe imefungwa kwa namna ya kuhakikisha kuwa hakuna hatari ya kunajisiwa.<sup>126</sup> Inafaa *tabernakulo* ibarikiwe kabla ya kuanza kuitumia katika Liturujia, kulingana na ibada-kanuni ilivyoelezwa katika *Rituale* ya Kiroma.<sup>127</sup>

**315.** Ili kuonyesha zaidi maana ya ishara, inafaa sana juu ya altare ambapo Misa huadhimishwa, kusiwepo tabernakulo ambamo huhifadhiwa Ekaristi Takatifu.<sup>128</sup>

Kwa hiyo, kutegemeana na maagizo ya Askofu-jimbo, *tabernakulo* inafaa iwekwe ifuatavyo:

a) iwekwe katika patakatifu, nje ya altare ya kuadhimishia Misa, pamoja na kuzingatia umbo lake na mahali pa kufaa zaidi, pasipo kusahau ile altare ya zamani ambayo haitumiwi tena kwa maadhimisho (*rej. n. 303*);

b) au hata katika kikanisa cha pembeni kifaacho kwa ajili ya kuabudu na kusali kwa waamini wakati wa faragha,<sup>129</sup> ila kikanisa hicho kiwe ni sehemu kamili ya umbo la kanisa lenyewe, na kuonekana wazi kwa waamini.

**316.** Kutokana na desturi iliyopokewa, karibu na *tabernakulo* iwepo taa maalum inayowaka daima, ilishwayo kwa mafuta au nta. Kwa njia ya taa hiyo, uwepo wa Kristo unaashiriwa na kuheshimiwa.<sup>130</sup>

**317.** Na tena, kamwe yasisahaulike yale mengine yote yaliyoagizwa kwa mujibu wa sheria kuhusu kuihifadhi Ekaristi Takatifu.<sup>131</sup>

### **Sanamu/picha takatifu**

**318.** Katika Liturujia ya duniani, Kanisa hushiriki na kuionja ile Liturujia ya mbinguni inayoadhimishwa katika mji mtakatifu wa Yerusalemu, ambako linaelekea kama mhujaji. Huko, Kristo ameketi kuume kwa Mungu. Tena likiwa linawakumbuka Watakatifu kwa heshima, linatumaini kupata nafasi ya kuwa na ushirika pamoja nao.<sup>132</sup>

Kwa sababu hiyo, sanamu au picha za Bwana, za Bikira Maria mtakatifu, na za Watakatifu, kwa kulingana na mapokeo ya zamani sana ya Kanisa, ziwekwe katika majengo matakatifu, ili waamini wapate kuziheshimu.<sup>133</sup> Humo, zipangwe kwa utaratibu hivyo kwamba zitawasindikiza waamini kwenye mafumbo ya imani yanayoadhimishwa humo. Kwa sababu hiyo, kuwe na tahadhari ili idadi ya sanamu/picha isije ikaongezeka bila busara, yaani ziwekwe kwa utaratibu unaotakiwa ili zisije zikatawanya mawazo ya waamini wakati wa adhimisho lenyewe.<sup>134</sup> Wala kwa kawaida, zisiwekwe sanamu/picha zaidi ya moja ya mtakatifu yuleyule. Kwa kawaida, katika kupamba na kuandaa kanisa, tunapofikiria sanamu, mambo ya kuzingatiwa ni moyo wa ibada wa jumuiya nzima, pamoja na uzuri na ustahivu wa hizo sanamu zenyewe.

## Sura ya Sita

### VIFAA VINAVYOHITAJIKA KWA KUADHIMISHA MISA TAKATIFU

#### I. KUHUSU MKATE NA DIVAI KWA KUADHIMISHA EKARISTI TAKATIFU

**319.** Kwa kufuata mfano wa Kristo mwenyewe, Kanisa daima limetumia mkate na divai pamoja na maji kwa ajili ya kuadhimisha Karamu ya Bwana.

**320.** Mkate kwa ajili ya kuadhimisha Ekaristi Takatifu unapaswa kuwa wa ngano tu, uliokwa karibuni, na usiochachwa. Haya ni kulingana na mapokeo ya Kanisa la Kilatini.

**321.** Maana halisi ya ishara hutaka kuwa kitu kinachotumiwa kuadhimishia Ekaristi Takatifu kionekane kweli kama chakula. Kwa hiyo inafaa sana mkate wa Ekaristi Takatifu, ingawa haukuchachwa na kuokwa katika umbo la kimapokeo, utengenezwe hivyo kwamba kuhani katika kuadhimisha Misa pamoja na watu ataweza kweli kuimega hostia katika vipande na kuwagawia walau waamini kadhaa. Kama kuna idadi kubwa ya watakaokomunika, au kama kuna sababu nyingine za kichungaji, hostia ndogo hazikataliwi hata kidogo. Lakini tendo la “kumega mkate”, kama Ekaristi Takatifu ilivyojulikana nyakati za Mitume, linaonyesha kwa uwazi zaidi, nguvu na uzito wa ishara ya umoja wa wote katika mkate huu ulio mmoja, na ya mapendo ambayo hutoka katika huo mkate mmoja, unaogawiwa kati ya ndugu.

**322.** Divai ya kuadhimishia Ekaristi Takatifu inapaswa kuwa ile itokanayo na mazao ya mzabibu (*rej. Lk 22:18*), halisi na isiyoghushiwa, yaani isiwe imechanganywa na kitu kingine chochote.

**323.** Lazima kuwa na uangalifu mkubwa ili mkate na divai kwa ajili ya kuadhimishia Ekaristi Takatifu vihifadhiwe katika hali



kamilifu kabisa, yaani divai isichachuke, wala mkate usiharibike au kuwa mgumu mno kiasi cha kutoweza kuvunjika kwa urahisi.

**324.** Kama, kuhani baada ya *konsekrasio*, au anapokomunika, hutambua kuwa ni maji yaliyowekwa katika kikombe badala ya divai, basi amwage maji hayo katika chombo kingine, halafu aweke divai pamoja na maji katika kikombe, na kuigeuza kwa kusema tu ile sehemu ya Sala ya Ekaristi inayohusu divai, pasipo kulazimika kugeuza tena mkate.

## **II. MAPAMBO YA IBADA KWA UJUMLA**

**325.** Kama ilivyo katika ujenzi wa makanisa, ndivyo ilivyo kuhusu mapambo yote ya ibada. Kanisa hukubali mtindo wa usanii wa kila nchi, na kuzipokea sanaa bora zinazoendana na ustadi na mapokeo ya kila taifa, mradi zinatoshleza matumizi yaliyokusudiwa na mapambo hayo ya ibada yenyewe.<sup>135</sup>

Hata katika kuchagua mapambo ni lazima kuangalia unadhifu ulio bora na unaoambatana vizuri kabisa na usanii wa kweli.

**326.** Katika kuchagua vitu vya kutengenezea mapambo ya ibada, licha ya vile vilivyokubaliwa kutokana na mapokeo, vyaweza kukubaliwa pia vitu ambavyo kadiri ya mtazamo wa nyakati hizi zetu, ni bora, vinavutia, ni vya kudumu na vinaweza kuundika vizuri kwa ajili ya matumizi ya ibada. Ni juu ya Baraza la Maaskofu la kila nchi kuamua juu ya jambo hili (*taz. n. 390*).

## **III. KUHUSU VYOMBO VITAKATIFU**

**327.** Kati ya vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kuadhimisha Misa, viko vyombo vitakatifu vinavyostahili heshima ya pekee. Na kati ya hivyo, ni kikombe na patena ambamo divai na mkate vinatolewa, vinageuzwa na kupokewa.

**328.** Inapasa vyombo vitakatifu vitengenezwe kwa madini yenye thamani. Ikiwa vilitengenezwa kwa madini ya aina ya chuma ambayo huweza kupata kutu, au madini isiyo na thamani kubwa kama dhahabu, inabidi vipakwe dhahabu walau kwa ndani.

**329.** Kwa kutegemea uamuzi wa Baraza la Maaskofu, ambao umeidhinishwa na Kiti cha Kitume, vyombo vitakatifu vinaweza kutengenezwa pia kwa vitu vigumu na bora kulingana na vigezo vya kawaida vya kila mahali, kama vile mpingo, au miti mingine migumu, ilimradi iwe ya kufaa kwa ajili ya matumizi matakatifu. Ikiwa hivyo, daima zichaguliwe na kupendelewa dutu zisizovunjika kwa urahisi au kuharibika. Na hili lifanyike kwa vyombo vyote vinavyotazamiwa kutumika kwa ajili ya hostia, kama vile, *patena*, *siborio*, *theka*, *monstransi*, na vingine vya aina hiyo.

**330.** Kuhusu vikombe na vyombo vingine vya kuwekea Damu ya Bwana, viwe na bakuli iliyotengenezwa kwa dutu isiyonyonya kitu cha majimaji (kitu kisichonyonya majimaji). Kikalio chake kinaweza kutengenezwa kwa kitu kingine kigumu na chenye heshima.

**331.** Kwa ajili ya kugeuza hostia, inawezekana kutumia patena kubwa zaidi inayoweza kushika mkate wa kuhani, wa shemasi, hata na wa wahudumu wengine na waamini.

**332.** Kuhusu umbo la vitu vitakatifu, ni kazi ya fundi kuvitengeneza kwa umbo linalopendeza zaidi, ambalo linalingana na utamaduni wa kila nchi peke peke, mradi vyombo hivyo vifae kwa matumizi ya Liturujia kama ilivyonuiwa. Tena vitofautiane kabisa na vile vinavyotumiwa kwa shughuli za kawaida.

**333.** Katika kuvibariki vyombo vitakatifu zifuatwe ibada-kanuni zilizotolewa katika vitabu vya kiliturujia.<sup>136</sup>

**334.** Desturi ya kujenga *sakrario* katika sakristia ambamo humwagwa maji yaliyotumika kuoshea vyombo vitakatifu na kufulia vitambaa, idumishwe (*rej. n. 280*).

#### **IV. MAVAZI YA IBADA**

**335.** Katika Kanisa, ambalo ni Mwili wa Kristo, viungo vyote havifanyi kazi ileile. Tofauti hii ya majukumu katika adhimisho la Ekaristi Takatifu, inaonyeshwa kwa nje kwa tofauti ya mavazi ya

ibada, ambayo kwa njia hiyo hupaswa kuwa alama ya kudhihirisha jukumu maalum la kila mhudumu. Mavazi hayo ya ibada yanapaswa kuongeza hadhi ya hilo adhimisho takatifu lenyewe. Mavazi yanayovaliwa na makuhani, mashemasi, hata yale ya wahudumu walei, yafaa yabarikiwe kabla ya kuanza kutumiwa katika Liturujia, kulingana na ibada-kanuni za Rituale ya Kiroma.<sup>137</sup>

**336.** Vazi la ibada la kawaida kwa wahudumu wote wenye Daraja, pamoja na wale walioteuliwa rasmi katika ngazi zote ni *alba* inayofungwa kwa mshipi kiunoni, isipokuwa kama mshono wake hauhitaji mshipi wa kuibana kiunoni. Kabla ya kuvaa alba, kama shingo hubaki wazi, ivaliwe kwanza *amisi*. Alba isifanyiwe mbadala kwa sulpisi, wala kwa kanzu, kama kasula au dalmatika inavaliwa; wala ikiwa kadiri ya kanuni, stola huvaliwa peke yake bila kasula au dalmatika.

**337.** Vazi rasmi la kuhani *selebranti*, katika Misa au ibada takatifu nyingine zinazounganika moja kwa moja na Misa, ni *kasula* au *planeta*, ambavyo huvaliwa juu ya alba na stola, isipokuwa kama imeelekezwa vingine.

**338.** Vazi rasmi la shemasi ni Dalmatika inayovaliwa juu ya alba na stola. Hata hivyo, dalmatika huweza kuachwa ikiwako sababu, au ikiwa kiwango cha sherehe ni kidogo tu.

**339.** Waakoliti, wasomaji na wahudumu wengine walei wanaweza kuvaa alba au vazi jingine lililokubaliwa kisheria na Baraza la Maaskofu wa mahali pale (*rej. n. 390*).

**340.** Stola huvaliwa na kuhani shingoni ikining'inizwa kifuaani pake. Lakini shemasi huivaa stola juu ya bega la kushoto na kuining'iniza chini ya kwapa la mkono wa kulia, ambapo hufungwa vizuri na kutua pale.

**341.** Pluviale, au joho, huvaliwa na kuhani wakati wa maandamano mengine, kulingana na rubrika maalum za kila ibada-kanuni.

**342.** Mabaraza ya Maaskofu huweza kuchagua na kupendekeza kwa Kiti cha Kitume marekebisho yanayohusu mtindo wa mavazi ya ibada yatakayotumika, kulingana na mahitaji na desturi za kila nchi.<sup>138</sup>

**343.** Katika kushona mavazi ya ibada, zaidi ya vifaa vilivyozeleka, inawezekana pia kutumia vifaa vinavyopatikana kila mahali panapohusika, iwe vinatokana na nyuzi za asili, au nyuzi zilizotengenezwa viwandani. Lakini vinatakiwa vionyeshe hadhi ya matendo matakatifu na ya wanaohudumia patakatifu. Ni juu ya Baraza la Maaskofu wa nchi husika kuamua jambo hili.<sup>139</sup>

**344.** Uzuri na hadhi ya mavazi ya ibada visitafutwe katika wingi wa mapambo, bali katika vitu vilivyotumika na umbo la mavazi hayo. Nakshi zionyeshe sura, au picha, au ishara zinazoelekeza kwenye matumizi matakatifu ya mavazi yenyewe. Mengine yote yasiyofaa kwa matumizi matakatifu yaondolewe.

**345.** Mavazi matakatifu ni ya rangi mbalimbali. Rangi hizo huonyesha tabia ya pekee ya mafumbo ya wokovu yanayoadhimishwa. Aidha, huonyesha vizuri zaidi kwa nje hatua mbalimbali za maendeleo ya maisha ya kikristo katika mwaka wa Liturujia.

**346.** Kuhusu rangi ya mavazi ya ibada ufuatwe utaratibu uliopokelewa, yaani:

a) Rangi Nyeupe itumike katika Sala ya Ofisio na Misa wakati wa Pasaka na wa Kuzaliwa Bwana. Pia, itumike katika maadhimisho ya Bwana yasiyohusu Mateso yake, Maadhimisho ya Bikira Maria Mtakatifu, Malaika Watakatifu, Watakatifu wasio Wafia-dini, Watakatifu wote (1 Novemba), na ya Mtakatifu Yohane Mbatizaji (Juni 24), katika Sikukuu ya Mt. Yohane Mwinjili (27 Desemba), ya Ukulu wa Mt. Petro (22 Februari) na Kuongoka kwa Mt. Paulo (25 Januari).

b) Rangi Nyekundu itumike Dominika ya Matawi na Ijumaa Kuu, Dominika ya Pentekoste; katika maadhimisho ya Mateso ya

Bwana, katika Sikukuu za kuzaliwa mbinguni Mitume na Wainjili na katika maadhimisho ya Watakatifu Wafia-Dini.

c) Rangi ya Kijani kibichi itumike katika Sala ya Ofisio na Misa za kipindi “*cha mwaka*”.

d) Rangi ya Urujuani itumike wakati wa Majilio na Kwaresima. Inaweza kutumika pia katika Sala ya Ofisio na Misa za wafu.

e) Rangi nyeusi huweza kutumika katika Misa za wafu, kama ni desturi ya mahali hapo.

f) Rangi ya Waridi inaweza kutumika katika Dominika ya **Gaudete** (ya Tatu ya Majilio) na ya **Laetare** (ya Nne ya Kwaresima) pale ambapo ni desturi.

g) Katika Sikukuu na maadhimisho makubwa zaidi huwezekana kutumia mavazi ya ibada ya kisikukuu zaidi au ya kifahari zaidi, hata kama si ya rangi ya siku hiyo.

Kwa upande mwingine Mabaraza ya Maaskofu yanaweza kuamua juu ya rangi za kiliturujia, na kuzipendekeza kwa Kiti cha Kitume, yakiwa ni marekebisho yanayolingana na mahitaji na utamaduni wa watu wao.

**347.** Katika Misa za kuadhimisha Sakramenti hutumika mavazi ya rangi inayolingana na Sakramenti inayoadhimishwa, au rangi nyeupe, au rangi ya sikukuu. Katika Misa kwa ajili ya mahitaji mbalimbali hutumika mavazi ya rangi ya siku hiyo, au ya kipindi cha wakati huo; au hata ya rangi ya urujuani, kama Misa ina tabia ya toba; kwa mfano, na. 31: Misa wakati wa vita; na. 33: Misa wakati wa njaa; na. 38: Misa kwa maondoleo ya dhambi. Katika Misa za kuchagua hutumika mavazi ya rangi inayoendana na Misa iliyochaguliwa; au pia rangi ya siku hiyo, au ya kipindi hicho.

## V. ZANA NYINGINE ZINAZOTUMIKA KANISANI

**348.** Licha ya vyombo vitakatifu na mavazi ya ibada ambayo hayana budi kutengenezwa kutoka vitu maalum, vifaa vingine

ambavyo hutumika katika Liturujia,<sup>140</sup> au kwa namna moja au nyingine hutumika Kanisani, havina budi kuwa na hadhi inayolingana na lengo la matumizi ya kila kimojawapo.

**349.** Kwa namna ya pekee, vitabu vya kiliturujia, hasa Kitabu cha Injili na Kitabu cha Masomo, (yaani **Evangeliarium** na **Lectionarium**), vitunzwe kwa uangalifu mkubwa. Vitabu hivi hutumiwa kwa ajili ya kutangaza Neno la Mungu, na kwa sababu hiyo vinastahili heshima ya kipekee. Tena, vitabu hivi ambavyo katika matendo ya kiliturujia, ni alama na ishara ya mambo ya mbinguni, viwe kweli vyenye ustahivu, visafi, na vizuri.

**350.** Zaidi tena, vile vifaa ambavyo vinahusiana na altare moja kwa moja, na vinatumika katika adhimisho la Ekaristi, vitunzwe kwa uangalifu mkubwa. Vifaa hivi ni kama Msalaba wa altare, na ule Msalaba unaotumika katika maandamano.

**351.** Vilevile kuwe na uangalifu katika mambo madogo madogo, ili sheria za sanaa na ufundi ziheshimiwe inavyotakiwa. Daima urari wenye heshima usiozidisha mapambo, uunganishwe na usafi.

## Sura ya Saba

### KUCHAGUA MISA NA SEHEMU ZAKE

**352.** Ufanisi wa utendaji wa kichungaji utaongezeka sana kutokana na adhimisho la Misa, ikiwa kadiri inavyowezekana, matini za masomo, za Sala, na za nyimbo, hulingana na mahitaji, maandalizi ya kiroho, pamoja na vipaji vya kiakili vya wale wanaoshiriki. Lengo hili litafikiwa kwa kutumia vema uwezekano mpana wa kuchagua, kama itakavyoelezwa hapa chini.

Kwa hiyo kuhani, katika kuandaa Misa, azingatie manufaa ya kiroho ya taifa lote la Mungu, kuliko kufuata maelekeo yake mwenyewe. Zaidi ya hayo akumbuke kwamba chaguo la aina hii la sehemu mbalimbali za Misa halina budi kufanyika kwa kuwahusisha wale wanaotimiza sehemu fulani za adhimisho hilo, pasipo kuwasahau waamini wengine kwa jumla, kuhusu zile sehemu ambazo huwahusu wao moja kwa moja.

Kwa kuwa kuna uwezekano wa aina nyingi wa kuchagua sehemu mbalimbali za Misa, kuna ulazima kabla ya adhimisho lolote, shemasi, wasomaji, mwimba-zaburi, mwimbaji-kiongozi, mtoa-maelezo, kikundi cha waimbaji, kila mmoja afahamu kikamilifu sehemu yake inayomhusu; na kisifanyike chochote bila maandalizi. Mpango wenye utaratibu mzuri na utekelezaji mzuri wa ibada-kanuni, unachangia sana katika kuziandaa nyoyo za waamini waweze kushiriki adhimisho la Ekaristi Takatifu inavyotakiwa.

### I. KUCHAGUA MISA

**353.** Katika Misa za Sherehe kuhani sharti afuate kalenda ya Kanisa la mahali anapoadhimisha.

**354.** Kuhusu Siku za Dominika, siku za juma katika vipindi vya Majilio, Kuzaliwa Bwana, Kwaresima na Pasaka, Sikukuu na Kumbukumbu za lazima, utaratibu ni huu ufuatao:

a) kama Misa huadhimishwa pamoja na watu, kuhani afuate kalenda ya Kanisa la pale anapoadhimisha;

b) kama kuhani huadhimisha Misa pamoja na mhudumu mmoja tu, huweza kufuata kalenda ya mahali pale, au kalenda ya Kanisa zima.

**355.** Kuhusu Misa za Kumbukumbu za hiari, utaratibu ni huu ufuatao:

a) katika siku za juma za kipindi cha Majilio, kuanzia 17 mpaka 24 Desemba; katika siku za Oktava ya Noeli, na katika siku za juma za kipindi cha Kwaresima, isipokuwa Jumatano ya Majivu na katika Juma Kuu, kuhani huadhimisha Misa ya siku hiyo. Lakini katika Kumbukumbu ambayo pengine huenda iliwekwa siku hiyo katika kalenda ya Kanisa zima, kuhani anaweza kuchukua kolekta, ilimradi haiangukii Jumatano ya Majivu, au katika Juma Kuu. Katika siku za juma za kipindi cha Pasaka, kumbukumbu za Watakatifu huweza kuadhimishwa zote nzimanzima zilivyo katika utaratibu wake;

b) katika siku za juma za kipindi cha Majilio kabla ya 17 Desemba; katika siku za juma kipindi cha Noeli kuanzia 2 Januari, na katika siku za juma za kipindi cha Pasaka huwezekana kuchagua kuadhimisha Misa ya siku hiyo, au Misa ya Mtakatifu, au ya mmojawapo wa Watakatifu wanaokumbukwa siku hiyo; au Misa ya Mtakatifu mwingine anayekumbukwa tarehe hiyo katika Kalenda ya Watakatifu (**Martyrologium**);

c) katika siku za juma kipindi cha mwaka kuhani huweza kuchagua Misa ya siku hiyo, au Misa ya Kumbukumbu ya hiari kwa siku hiyo, au Misa ya Mtakatifu mwingine anayekumbukwa tarehe hiyo katika Kalenda ya Watakatifu, au Misa kwa ajili ya shida mbalimbali, au Misa ya kuchagua.

Iwapo kuhani anaadhimisha Misa pamoja na watu, awe mwangalifu asiache mara nyingi na bila sababu ya kutosha, masomo ya Misa yaliyochaguliwa katika Kitabu cha Masomo



kwa ajili ya siku za juma. Kwa sababu Kanisa linatamani sana waamini waandaliwe meza ya Neno la Mungu, lenye utajiri mwingi zaidi na zaidi.<sup>141</sup>

Kwa sababu hiyohiyo, kuhani atumie ukadiri katika kuchukua Misa za wafu, kwani kila Misa hutolewa kwa ajili ya walio hai, na waliokufa; na tena katika Sala ya Ekaristi, wafu hukumbukwa daima.

Pale palipo na waamini wenye moyo wa kufanya kumbukumbu za hiari za Bikira Maria au Watakatifu, watimiziwe ibada hii yao halali.

Pale ambapo kuna fursa ya kuchagua kati ya kumbukumbu mojawapo katika Kalenda ya Kanisa zima na mojawapo katika Kalenda ya jimbo, au ya Shirika la kitawa, ichaguliwe kumbukumbu iliyo katika Kalenda maalumu, baada ya kuangalia mambo mengine, na mwelekeo wa mapokeo.

## II. KUCHAGUA SEHEMU ZA MISA

**356.** Katika kuchagua matini za sehemu mbalimbali za Misa, iwe katika kipindi maalumu au katika kumbukumbu ya Watakatifu, kanuni zifuatazo zizingatiwe.

### Masomo

**357.** Katika siku za Dominika na Sherehe yamepangwa masomo matatu, yaani kutoka maandiko ya Manabii, maandiko ya Mitume, na Injili. Kwa njia ya masomo haya taifa la Kikristo linalelewa kutambua maendeleo ya matendo ya wokovu kadiri ya azimio la ajabu la Mungu. Masomo haya matatu ni lazima yasomwe. Katika kipindi cha Pasaka, kuendana na mapokeo ya Kanisa, husomwa somo kutoka Matendo ya Mitume badala ya lile la Agano la Kale.

Nazo Sikukuu zina masomo mawili. Lakini sikukuu ikikwezwa na kuwa na ngazi ya Sherehe kulingana na sheria, huongeza somo la tatu, ambalo linachukuliwa kati ya yale ya kawaida (**de Communi**).

Katika kumbukumbu za Watakatifu, kama hakuna masomo ya pekee, huwa yanasomwa masomo ya siku ya juma. Mara kadhaa huwa na masomo maalum ambayo hutilia mwanga tabia ya maisha ya kiroho, au kazi ya kitume ya Mtakatifu anayehusika. Lakini, kutumia masomo haya si jambo la kuisitizwa sana, isipokuwa kama sababu za kichungaji zinaelekeza iwe hivyo.

**358.** Katika Kitabu cha Masomo ya siku za juma, masomo kwa kila siku ya wiki kwa wiki zote za mwaka yanapendekezwa. Kwa hiyo masomo hayo kwa kawaida yafuatwe kwa kila siku, kama ilivyopangwa, isipokuwa kama kuna sherehe, au sikukuu, au kumbukumbu yenye masomo maalumu kutoka Agano Jipya, ambapo ni lazima pia kumtaja Mtakatifu anayekumbukwa.

Lakini ikiwa pengine mfululizo wa masomo unakatizwa wakati wa juma, kwa ajili ya Sherehe fulani, au sikukuu mojawapo, au kwa ajili ya adhimisho la kipekee, kuhani, akizingatia mpango mzima wa masomo ya juma lote anaruhusiwa kuunganisha sehemu zile zilizoachwa na sehemu nyingine; au kuamua ni matini zipi zinafaa zaidi kusomwa.

Katika Misa kwa ajili ya makundi ya kipekee, kuhani anaweza kuchagua matini zenye kufaa zaidi kwa ajili ya adhimisho hilo la kipekee, mradi azichague kutoka matini za Kitabu cha Masomo kilichoidhinishwa.

**359.** Zaidi ya hayo, Kitabu cha Masomo kina mkusanyo maalum kutoka Maandiko Matakatifu kwa ajili ya Misa za kuadhimisha Sakramenti (**Missae Rituales**). Katika Misa hizo, Sakramenti au Visakramenti vinaingizwa. Pia yapo masomo kwa ajili ya Misa kwa ajili ya shida mbalimbali (**Missae pro variis necessitatibus**).

Kwa hiyo Vitabu vya Masomo vya namna hii vimewekwa, ili, waamini kwa kusikiliza Neno la Mungu kwa namna inayowafaa zaidi, wawezeshwe kufahamu kwa undani zaidi mafumbo ambayo wanashiriki, na hivyo wazidi kujengwa katika kulipenda Neno la Mungu kwa hamu kubwa zaidi.

Basi, matini zinazosomwa katika maadhimisho zichaguliwe kwa kufikiria vema lengo la kufaa la kichungaji, na pia kutumia vizuri uwezekano huu wa kuchagua katika jambo hili.

**360.** Mara nyingine hutolewa matini ndefu na matini fupi ya somo lilelile moja. Katika kuamua ni matini ipi ichukuliwe, daima vigezo vya kichungaji viwekwe maanani. Aidha, ni muhimu kuweka maanani uwezo wa waamini wa kusikiliza kwa manufaa yao somo lililo refu au lililo fupi; pia uwezo wao wa kuisikiliza matini iliyo timilifu zaidi itakapoelezwa katika homilia.<sup>142</sup>

**361.** Ruhusa inapotolewa ya kuchagua somo moja au jingine kati ya masomo yaliyotolewa, au yaliyopendekezwa tu, ni lazima kuwa na uangalifu mintarafu manufaa ya wale wanaohudhuria. Yaani hapa inatakiwa kuchagua matini iliyo rahisi zaidi, au ya kufaa zaidi kwa jumuiya iliyokusanyika; au pale matini inapopaswa kurudiwa au kubadilishwa kama matini maalumu kwa adhimisho fulani; au huchaguliwa nyingine kati ya zile za hiari, kila mara manufaa ya kichungaji yanapoonyesha kuwa inafaa kufanya hivyo.<sup>143</sup>

Na hii inaweza kutokea, iwapo inapasa kurudia matini ileile siku zilizo karibu, kwa mfano, Dominika na Jumatatu inayofuata; au kama kuna hofu kwamba matini fulani inaweza kuzusha matatizo fulani katika jumuiya husika ya waamini. Hata hivyo, lazima kuwe na tahadhari, ili katika kuchagua matini za Maandiko Matakatiifu, sehemu zake nyingine zisije zikaachwa kabisa kabisa.

**362.** Licha ya uwezekano wa kuchagua matini zenye kufaa zaidi kama ilivyofafanuliwa hapo juu, ruhusa inatolewa kwa Mabaraza ya Maaskofu, katika mazingira maalumu, Mabaraza hayo yaweze kuelekeza kufanywe marekebisho fulani fulani kuhusu masomo, yaani zichaguliwe matini kutoka Kitabu cha Masomo kilichoidhinishwa rasmi, lakini ifanyike kulingana na sheria.

## **Kuhusu Sala za Misa**

**363.** Katika Misa yoyote ile Sala zinazosemwa ni zile za Misa hiyohiyo, isipokuwa imeelezwa vingine.

Katika Kumbukumbu za Watakatifu, husemwa *Kolekta* maalum, au kama haipo, inasemwa Kolekta kutoka kwenye kawaida husika ya watakatifu. Lakini Sala ya Kuombea Dhabihu na Sala Baada ya Komunyo zaweza kuchukuliwa kutoka kawaida ya Watakatifu, au zile za Siku za Kipindi kilichopo, isipokuwa kama zipo sala za pekee.

Katika siku za kawaida za mwaka, licha ya Sala za Dominika iliyotangulia, hata Sala za Dominika nyingine zinaweza kutumiwa, au mojawapo kutoka sala kwa ajili ya shida mbalimbali, ambazo zimeorodheshwa katika Misale. Hata hivyo, inaruhusiwa kuchukua kutoka Misa hizo hata *Kolekta* peke yake tu.

Kwa njia hiyo, kumetolewa utajiri mwingi zaidi wa matini ambazo zinalisha maisha ya sala ya waamini kwa wingi zaidi.

Katika vipindi vikuu zaidi vya mwaka, matengenezo haya tayari yamefanyika kwa njia ya zile Sala maalum zilizopo katika Misale, ambazo ni za kipekee kwa vipindi hivyo na kwa kila siku ya juma.

## **Sala ya Ekaristi**

**364.** Tangulizi nyingi, au *Prefasio*, zinazoipamba na kuitajirisha Misale ya Kiroma zimekusudiwa kuzifafanua kwa uwazi zaidi hoja za tendo la shukrani, jinsi zilivyo katika Sala ya Ekaristi; nazo dhamira mbalimbali za fumbo la wokovu zijionyeshe kwa mwanga mkubwa zaidi.

**365.** Katika kuchagua kati ya Sala za Ekaristi zinazopatikana katika Kanuni ya Misa, sheria hizi zifuatwe:

a) **Sala ya Kwanza ya Ekaristi**, au Kanuni ya Kiroma, ambayo huweza kutumiwa kila wakati, husemwa hasa siku zile zilizowekewa *Tushirikiane* za pekee, au katika Misa zilizowekewa *Kwa hiyo* za pekee; hali kadhalika katika

maadhimisho ya Mitume au ya Watakatifu wale wanaotajwa katika hii Sala yenyewe. Vilevile hutumika katika siku za Dominika, isipokuwa Sala ya Ekaristi ya Tatu, hupendelewa zaidi kwa sababu za kichungaji.

b) **Sala ya Ekaristi ya Pili**, kwa sababu ya muundo wake wa pekee, hufaa katika siku za kawaida za juma, au katika mazingira mengine ya pekee. Ingawa Sala hii inao Utangulizi wake, hata hivyo huweza kutumiwa pia na Tangulizi nyingine, hasa zile Tangulizi zinazoonyesha kwa namna ya muhtasari fumbo la wokovu, kwa mfano, Tangulizi za Kawaida. Inapoadhimishwa Misa kwa ajili ya marehemu fulani, huweza kutumiwa fomula ya pekee iliyowekwa mahali pake, yaani kabla ya ***Uwakumbuke pia.***

c) **Sala ya Ekaristi ya Tatu**, yaweza kutumika pamoja na Utangulizi wowote ule. Itumiwe hasa siku za Dominika na Sikukuu. Iwapo Sala hii hutumiwa katika Misa ya wafu, yaweza kutumiwa fomula ya pekee kwa ajili ya marehemu kwa kuiweka mahali pake, yaani baada ya maneno ***Uwakusanye kwako wanao wote waliotawanyika popote duniani.***

d) **Sala ya Ekaristi ya Nne**, ina Utangulizi usiobadilika, na inaonyesha muhtasari mkamilifu wa historia ya wokovu. Yaweza kutumiwa pale Misa inapokuwa haina Utangulizi wa pekee, na katika Dominika “za Mwaka”. Katika Sala hii, kwa sababu ya muundo wake wa pekee, haiwezekani kusema fomula ya pekee kwa ajili ya marehemu.

## **Nyimbo**

**366.** Nyimbo zilizopo katika Kanuni ya Misa haziwezi kamwe kupewa mbadala, mathalani, ***Mwanakondoo wa Mungu***, haiwezi kubadilishwa kamwe na wimbo mwingine wowote.

**367.** Mintarafu kuchagua nyimbo zilizopo kati ya masomo, vilevile nyimbo za mwanzo, matayarisho ya vipaji na Komunyo, zishikwe kanuni zilizowekwa mahali pake (*rej. nn. 40-41, 47-48, 61-64, 74, 86-88*).

## Sura ya Nane

### MISA NA SALA KWA SHIDA MBALIMBALI NA MISA ZA WAFU

#### I. MISA NA SALA KWA SHIDA MBALIMBALI

**368.** Kwa kuwa Liturujia ya Sakramenti na ya Visakramenti inayo nguvu ya kufanya kazi hivyo kwamba, kwa waamini walio na nia njema, karibu matukio yote ya maisha yao yanaweza kutakatifuzwa kwa neema ya kimungu inayotiririka kutoka Fumbo la Pasaka;<sup>144</sup> na pia kwa kuwa Ekaristi Takatifu ndiyo Sakramenti Kuu ya Sakramenti zote, basi Misale imeandaa mifano ya Misa na Sala ambazo zinaweza kutumika kwa nafasi mbalimbali za maisha ya kikristo, kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya ulimwengu mzima, au ya Kanisa lote, hata na ya Kanisa mahalia.

**369.** Kwa kuangalia mapana ya ruhusa iliyotolewa ya kuchagua masomo na sala, inafaa Misa kwa ajili ya mahitaji mbalimbali zitumiwe kwa kiasi, yaani pale panapokuwa na hitaji kweli la lazima.

**370.** Katika Misa zote kwa ajili ya shida mbalimbali, isipokuwa imeangalishwa vingine, masomo ya siku za wiki yanaweza kutumiwa, na hata nyimbo za katikati ya masomo hayo, ikiwa haya yanapatana na adhimisho lenyewe.

**371.** Miongoni mwa hizo Misa, zinajumlishwa Misa za Kuadhimisha Sakramenti, Misa kwa ajili ya Shida mbalimbali, na Misa za Kuchagua.

**372.** Misa za kuadhimisha Sakramenti zinaunganishwa na adhimisho la Sakramenti fulani au kisakramenti fulani. Misa hizi hukatazwa katika Dominika za Majilio, za Kwaresima na za Kipindi cha Pasaka, katika maadhimisho ya Sherehe, katika siku za Oktava ya Pasaka, katika Kumbukumbu ya Marehemu wote, Jumatano ya Majivu na katika siku za Juma Kuu. Zaidi ya

hayo, kanuni zilizowekwa katika vitabu vya *Rituale*, au katika Misa zenyewe lazima zizingatiwe.

**373.** Misa kwa ajili ya mahitaji mbalimbali au “**Missae ad Diversa**” hutumika katika matukio fulani fulani mara yanapotokea, au nyakati ambazo hurudia kutokea. Kutoka Misa hizo huweza kuchaguliwa na mwenye mamlaka husika Misa kwa ajili ya maombezi maalumu ambazo zimepangwa na Baraza la Maaskofu katika mzunguko wa mwaka.

**374.** Kukitokea shida fulani yenye uzito wa kipekee, au manufaa makubwa ya kichungaji, Misa inayolingana na tatizo hilo inaweza kuadhimishwa kwa amri au rufusa ya Askofu-jimbo. Misa ya namna hiyo inaweza kuadhimishwa siku yoyote isipokuwa Sikukuu za Sherehe, Dominika za Majilio, za Kwaresima, za Kipindi cha Pasaka, Siku za Oktava ya Pasaka, Kumbukumbu ya Marehemu wote, Jumatano ya Majivu na Siku za Juma Kuu.

**375.** Misa za Kuchagua (**Missae votivae**) za mafumbo ya Bwana, au za kumheshimu Bikira Maria, au Malaika, au Mtakatifu mmojawapo, au Watakatifu wote, huweza kuadhimishwa kwa ajili ya kukuza moyo wa ibada ya waamini katika siku za juma katika mwaka, hata kama ni kumbukumbu ya hiari. Lakini Misa zinazohusiana na mafumbo ya maisha ya Bwana, au ya Bikira Maria Mtakatifu haziwezi kuadhimishwa kama Misa za kuchagua, isipokuwa Misa ya Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, kwa sababu adhimisho la Misa hizo ni sehemu halisi ya mzunguko wa mwaka wa kiliturujia.

**376.** Kisheria, Misa kwa shida mbalimbali na Misa za kuadhimisha Sakramenti na Visakramenti zimekatazwa siku ambazo kunaadhimishwa kumbukumbu ya lazima, au siku za Majilio mpaka tarehe 16 Desemba, Kipindi cha Noeli tangu Januari 2, na Kipindi cha Pasaka baada ya Oktava ya Pasaka. Lakini, kukiwa na shida fulani ya kweli, au manufaa ya kichungaji yakidai hivyo, basi, katika adhimisho la pamoja na waamini huweza kutumiwa Misa inayolingana na hitaji hilo au

manufaa hayo. Uamuzi huu unamtegemea mkuu wa Kanisa, au hata kuhani mwenye kuadhimisha.

**377.** Siku za kawaida za mwaka zinapofanywa kumbukumbu za hiari au inaposomwa Sala ya Vipindi vya Ofisio (**Officium**) ya siku, Misa yoyote yaweza kuadhimishwa, au sala yoyote kwa shida mbalimbali yaweza kusemwa, isipokuwa Misa za kuadhimisha Sakramenti.

**378.** Kwa namna ya pekee huagizwa ifanyike kumbukumbu ya Bikira Maria Mtakatifu siku ya Jumamosi (**sabato**), kwa kuwa Mama wa Mkombozi katika liturujia ya Kanisa hupewa heshima ya kwanza miongoni mwa Watakatifu wote.<sup>145</sup>

## II. MISA ZA WAFU

**379.** Kanisa hutolea Sadaka ya Kiekaristi ya Pasaka ya Kristo kwa ajili ya marehemu kusudi wengine waombewe msaada wa kiroho, na wengine waletewe kitulizo cha matumaini, maana viungo vyote vya mwili wa Kristo vimeunganika kati yao.

**380.** Kati ya Misa za wafu, Misa ya mazishi inachukua nafasi ya kwanza. Misa hii inaweza kuadhimishwa siku yoyote isipokuwa siku za Sherehe ya amri, Alhamisi Kuu, Siku Tatu Kuu za Pasaka (**Triduo Paschali**), Dominika za Majilio, za Kwaresima, na za Pasaka. Pia yazingatiwe mengine yote yanayopasa kulingana na kanuni zilizotolewa.<sup>146</sup>

**381.** Misa ya wafu baada ya kupokea taarifa ya kifo, au Misa baada ya kumaliza matanga, au Misa ya wafu baada ya kutimia mwaka – Misa hizi zote zaweza kuadhimishwa hata siku za Oktava ya Noeli, siku za kumbukumbu za lazima, au siku ya kawaida ambayo si Jumatano ya Majivu au siku ya Juma Kuu.

Misa nyingine za wafu, au zile ziiwazo Misa za wafu za kila siku (**cotidiana**), zinaweza kuadhimishwa siku za kawaida za mwaka zilizo kumbukumbu ya hiari, au inaposemwa sala ya Ofisio ya siku ya juma (**feria**), mradi ziwe kweli kwa ajili ya wafu.



**382.** Katika Misa ya mazishi kwa kawaida hutolewa homilia fupi, lakini kamwe isiwe ni hotuba ya aina ya wasifu wa marehemu anayezikwa.

**383.** Waamini waalikwe, hasa ndugu za marehemu, kushiriki sadaka ya Ekaristi inayotolewa kwa ajili ya marehemu. Washiriki pia kwa njia ya kupokea Komunyo.

**384.** Ikiwa Misa ya mazishi inaunganishwa moja kwa moja na maziko, ibada-kanuni ya kuhitimisha Misa inaachwa, na ikiisha semwa Sala baada ya Komunyo, ibada ya kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu inianza. Ibada hii haifanywi isipokuwa maiti iko pale.

**385.** Katika kupanga na kuchagua zile sehemu za Misa ya wafu zinazoweza kubadilika, hasa ikiwa ni Misa ya maziko (k.m. sala, masomo, maombi ya waamini), inafaa kuweka maanani kadiri inavyowezekana, vipengele au sababu za kichungaji kumhusu marehemu mwenyewe, familia yake na wale wanaohudhuria.

Zaidi ya hayo, kwa namna ya pekee wachungaji wawafikirie wale ambao kwa ajili ya maziko huhudhuria maadhimisho ya Liturujia hiyo, au wanaisikia Injili. Wawajali hawa - wawe wasio wakatoliki, au wakatoliki wasioshiriki kamwe maadhimisho ya Ekaristi Takatifu, au wanaohudhuria mara chache tu, au hata wale wanaoonekana wamepoteza imani. Sababu ni kwamba makuhani ni wahudumu wa Injili ya Kristo kwa watu wote.

## Sura ya Tisa

### MAREKEBISHO YALIYO CHINI YA MAMLAKA YA MAASKOFU NA MABARAZA YAO

**386.** Matengenezo mapya ya Misale ya Kiroma (**instauratio**) yaliyofanywa nyakati hizi zetu kulingana na *dikrii* za Mtaguso Mkuu wa Vatikano II yamezingatia kwa uangalifu mkubwa kuwawezesha waamini wote wapate kushiriki kwa utimilifu, kwa ufahamu na utendaji hai katika adhimisho la Ekaristi Takatifu, kama inavyotakiwa na hulka ya liturujia yenyewe, hata na haki na wajibu za waamini wenyewe – haki walizo nazo kutokana na misingi ya hali yao ya Ukristo.<sup>147</sup>

Ili adhimisho hili lipate kulingana na kiwango cha utimilifu unaotakiwa na sheria na roho ya Liturujia takatifu, katika Uratibu huu Mkuu, na katika Kanuni ya Misa (**Ordo Missae**), yamependekezwa marekebisho mengine ya ziada, ambayo yamewekwa chini ya uamuzi wa Askofu wa Jimbo au wa Mabaraza ya Maaskofu.

**387.** Askofu wa jimbo, ambaye inapasa apokelewe kama kuhani mkuu wa kundi lake, na ambaye maisha ya waamini wake katika Kristo, kwa namna fulani hutoka kwake, na humtegemea,<sup>148</sup> hupaswa kulea, kusimamia na kuongoza maisha ya kiliturujia katika jimbo lake. Kwa mujibu wa maelekezo haya makuu, anapewa jukumu la kuweka utaratibu wa nidhamu ya *konselebrasio* (*rej. 202, 374*); kutoa miongozo jinsi ya kumtumikia kuhani altareni (*rej. n. 107*); utaratibu wa kugawa komunyo katika maumbo mawili (*rej. n. 283*); kuweka mpango wa ujenzi wa majengo ya makanisa na kusimamia ujenzi wenyewe (*rej. n. 291*). Lakini, kwanza kabisa, ni juu yake Askofu mwenyewe, hasa hasa, kulisha na kukuza roho ya Liturujia takatifu katika mapadri wake, mashemasi na waamini.

**388.** Marekebisho yanayozungumziwa hapa chini, ambayo yanadai kiwango kikubwa cha uratibishaji, yanapaswa kuamuliwa na Baraza la Maaskofu kwa kufuata kanuni za kisheria.

**389.** Awali ya yote, ni juu ya Mabaraza ya Maaskofu kuandaa na kuidhinisha toleo la Misale hii ya Kiroma katika lugha mahalia zilizokubalika, ili baada ya kukubaliwa rasmi kwa tamko la Kiti cha Kitume, iweze kutumiwa katika nchi husika.<sup>149</sup>

Misale ya Kiroma ni lazima ichapishwe yote nzima, iwe ni katika lugha ya Kilatini, au lugha za mahali.

**390.** Ni juu ya Mabaraza ya Maaskofu kuamua juu ya marekebisho hayo, na baada ya kupata idhini rasmi (**recognitio**) kutoka Kiti cha Kitume, huyaingiza katika Misale yenyewe. Marekebisho hayo ni haya yaliyoonyeshwa katika Uratibu huu Mkuu, na yatawekwa katika Kanuni ya Misa (**Ordo Missae**):

- jinsi waamini wanavyokaa na hali yao ya kiwiliwili (*rej. n. 43*);
- kitendo cha kuiheshimu altare na Kitabu cha Injili (*rej. n. 273*);
- matini za nyimbo za kuingia, za matoleo na za komunyo (*rej. nn. 48, 74, 87*);
- masomo kutoka Maandiko Matakatifu ya kutumiwa katika mazingira ya kipekee (*rej. n. 362*);
- aina ya ishara ya kutakiana amani; (*rej. n. 82*)
- namna ya kupokea Komunyo takatifu (*rej. nn. 160, 283*);
- dutu (**materia**) inayotumika kutengenezea altare na zana takatifu, hasa vyombo vitakatifu; pia dutu, maumbo na rangi za mavazi ya kiliturujia (*rej. nn. 301; 326, 329, 339, 342-346*).

Lakini ifahamike kuwa Miongozo na Maagizo ya kichungaji yanayoamuliwa na Mabaraza ya Maaskofu kwamba yanafaa, baada ya kupata idhini rasmi ya Kiti cha Kitume, yanaweza kuingizwa katika Misale ya Kiroma mahali pake panapotakiwa.

**391.** Mabaraza hayohayo yanapaswa kuwa na uangalifu wa kipekee juu ya tafsiri za matini za Biblia ambazo hutumika katika adhimisho la Misa. Maana, kutoka Maandiko Matakatiifu ndimo huchukuliwa masomo ya kusomwa na kufafanuliwa katika homilia, pia zaburi zinazoimbwa; na kutokana na uvuvio na msukumo wake hutolewa maombi, sala na nyimbo za kiliturujia. Hali kadhalika kutoka Maandiko Matakatiifu matendo na ishara hupata maana yake.<sup>150</sup>

Lugha inayolingana na uwezo wa waamini itumiwe, na iwe ya kufaa kutamkwa hadharani. Hili lifanyike kwa kuzingatia mitindo mbalimbali ya misemo jinsi inavyotumika katika vitabu vya Biblia.

**392.** Hali kadhalika, Mabaraza ya Maaskofu yanapaswa kuandaa kwa makini sana tafsiri za matini nyinginezo kwa namna ambayo, pamoja na kuhifadhi tabia ya kila lugha, umaana wa matini asilia za Kilatini unatolewa kwa utimilifu na uaminifu. Katika kutimiza kazi hiyo, ni muhimu kuzingatia tanzu za fasihi zinazotumika katika Misa, kama vile, sala za kuhani kiongozi (*selebranti*), antifona, mashangilio, viitikizano, maombi ya kilitania, n.k.

Kuwe na angalisho kwamba tafsiri za matini hizo zisifanyike kwanza kwa lengo hasa la tafakari, bali hasa kwa ajili ya kutamkwa kwa sauti au kuimbwa katika utekelezaji wa adhimisho lenyewe.

Lugha iliyozoeleka kwa waamini husika itumike, na papo hapo kuzingatia vipengele vya ustahivu na ufasaha wa lugha. Kwa vyovyote, daima kutakuwa na haja ya katekesi fulani yenye kueleza maana za kibiblia na za Kikristo za maneno na sentensi kadha wa kadha.

Ingefaa sana, kadiri inavyowezekana katika nchi zenye lugha ileile, iwepo tafsiri ileile ya matini zote za kiliturujia, hasa ya zile matini za kibiblia na za Kanuni ya Misa.<sup>151</sup>

